**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA MANISPAA – MPANDA**



**MKUTANO WA KWANZA WA BARAZA LA MADIWANI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 UTAKAOFANYIKA KWENYE UKUMBI WA MIKUTANO WA MANISPAA YA MPANDA TAREHE 25/10/2018 KUANZIA SAA 4:00 ASUBUHI**

# TAARIFA ZA KATA

**Imetayarishwa na**:


OFISI YA MKURUGENZI WA MANISPAA,
HALMASHAURI YA MANISPAA,
S.L.P. 216,
MPANDA
SIMU NA 025-252957128,

FAX NA 025-252957129

Email: md@mpandamc.go.tz


**OKTOBA, 2018**

AGENDA ZA MKUTANO WA BARAZA LA MADIWANI WA TAREHE 25.10.2018 KUJADILI UTEKELEZAJI WA SHUGHULI MBALIMBALI KUTOKA KWENYE KATA

1) KUFUNGUA MKUTANO

2) KUSOMA NA KURIDHIA AGENDA ZA MKUTANO

3) KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA MKUTANO ULIOPITA

4) KUSOMA NA KUJADILI YATOKANAYO NA MKUTANO ULIOPITA

5) TAARIFA ZA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI MBALIMBALI KUTOKA KWENYE KATA

6) MENGINEYO KWA IDHINI YA MWENYEKITI

7) KUFUNGA MKUTANO

MUHTASARI WA MKUTANO WA NNE WA BARAZA LA MADIWANI ULIOFANYIKA KWENYE UKUMBI WA MIKUTANO WA HALMASHAURI YA MANISPAA YA MPANDA TAREHE 30/07/2018

**WAJUMBE WALIOHUDHURIA**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | MHE.WILLIAM P. MBOGO | DIWANI KATA YA MAJENGO | MWENYEKITI |
| 2. | NDG.MICHAEL F. NZYUNGU | MKURUGENZI WA MANISPAA | KATIBU |
| 3. | MHE.KANONI LUCAS | DIWANI KATA YA SHANWE | MJUMBE |
| 4. | MHE.MATONDO KANYEPO | DIWANI KATA YA MISUNKUMILO | ,, |
| 5. | MHE.BAKARI KAPONA | DIWANI KATA YA NSEMULWA | ,, |
| 6. | MHE.PHILIP J. KALYALYA | DIWANI KATA YA MAGAMBA | ,, |
| 7. | MHE.CARITAS MANGWANGWA | DIWANI VITI MAALUM | ,, |
| 8. | MHE.TOSIGWEGE MWAKYUSA | DIWANI KATA YA ILEMBO | ,, |
| 9. | MHE.NURU A. MKANA | DIWANI VITI MAALUM | ,, |
| 10 | MHE.CHRISANT MWANAWIMA | DIWANI KATA YA KASOKOLA | ,, |
| 11 | MHE.EDITRUDA M. KAMINDA | DIWANI VITI MAALUM | ,, |
| 12 | MHE.ELIAS MWANISAWA | DIWANI KATA YA KAZIMA | ,, |
| 13 | MHE.PIUS M. BUZUMALLE | DIWANI KATA YA KAWAJENSE | ,, |
| 14 | MHE.STEPHANO A MWAKABAFU | DIWANI KATA YA UWANJA WA NDEGE | ,, |
| 15 | MHE.WILLIAM LIWALI | DIWANI KATA YA MPANDA HOTEL | ,, |
| 16 | MHE.ROSE J. KOMBA | DIWANI VITI MAALUM | ,, |
| 17 | MHE.GEORGINA S. KISALALA | DIWANI VITI MAALUM | ,, |
| 18 | MHE.KALIPI KATANI | DIWANI KATA YA MWAMKULU | ,, |

**WATAALAM WALIOKUWEPO**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | NDG.DEODATUS C. KANGU | MKUU WA IDARA YA UTUMISHI NA UTAWALA |
| 2. | NDG. ELENIA LUTUNGULU | MKUU WA IDARA YA ELIMU SEKONDARI |
| 3. | DR.OBED MAHENGE | MKUU WA IDARA YA AFYA NA USTAWI WA JAMII |
| 4. | NDG .ASUBISYE MWANG’ONDA | KAIMU MKUU WA IDARA KILIMO NA USHIRIKA |
| 5. | NDG .LUCAS NDOMBELE | MKUU WA IDARA YA FEDHA NA BIASHARA |
| 6. | NDG .OSWALD RWEZAULA | KAIMU MKUU WA KITENGO CHA UCHAGUZI |
| 7. | ENG.MOHAMED ULENGA | KAIMU MKUU WA IDARA YA UJENZI |
| 8. | NDG .MARIETHA MLOZI | MKUU WA IDARA YA MAENDELEO YA JAMII |
| 9. | NDG .FESTO KATANTI | KAIMU MKUU WA IDARA YA MAJI |
| 10. | NDG .GEOFREY T. SIWEZI | KAIMU MKUU WA IDARA YA MIFUGO NA UVUVI |
| 11. | NDG .GISBERT MSEMWA | KAIMU MKUU WA IDARA YA MIPANGO MIJI,ARDHI NA MALIASILI |
| 12. | NDG .PULKERIA J. MAKUNGU | AFISA USAFIRISHAJI |
| 13. | NDG . GRACE KUNCHELA | AFISA AFYA |
| 14. | NDG .MARY A KANUMBA | MCHUMI |
| 15. | NDG .PHILIPO KAROL | MKUU KITENGO CHA UKAGUZI WA NDANI |
| 16. | NDG .MARY F. LUHULULA | MKUU WA IDARA YA MIPANGO ,SERA NA UFUATILIAJI |
| 17. | NDG . SAID MANDUA | AFISA MAZINGIRA |
| 18. | NDG HOBOKELA MWAKAGAMBA | KAIMU MKUU WA KITENGO CHA MANUNUZI |
| 19. | NDG .OMARY ZOBANO | AFISA BIASHARA |
| 20. | NDG .ALEX SEMWALI | MKUU WA USAFISHAJI NA MAZINGIRA |
| 21. | NDG.BENSON NG’AMILO | KATIBU TSC |
| 22. | NDG.PIUS DONALD | AFISA HABARI |
| 23. | NDG.GILBERT BAYAGA | KAIMU KATIBU TAWALA WILAYA |
| 24. | NDG.EZEKIA BICHURO | AFISA TARAFA YA KASHAULILI |

**WAALIKWA WALIOHUDHURIA**

1. NDG.ABELI KIMAZI MWENYEKITI WA CCM WILAYA YA MPANDA
2. NDG.LILIAN KITTA KAIMU MKUU WA USALAMA WILAYA
3. NDG.JOHN D. SALANGA MTENDAJI KATA YA MAJENGO
4. NDG.MARY T. NGOMALUFU MTENDAJI KATA YA KASHAULILI
5. NDG.DONALD KUSEKWA MTENDAJI KATA YA MPANDA HOTEL
6. NDG. EMIL KATENDELE MTENDAJI KATA YA ILEMBO
7. NDG. EMMANUEL CHAULA MTENDAJI KATA YA KASOKOLA
8. NDG.JOHARI A. JUMA MTENDAJI KATA YA MAGAMBA
9. NDG.ANNA G. KAPONDO MTENDAJI KATA YA UWANJA WA NDEGE
10. NDG.REUBEN. W. KASOMO MTENDAJI KATA YA KAKESE
11. NDG.MUSA KITEKA KAIMU MTENDAJI KATA YA MAKANYAGIO
12. NDG.GEORGE ILESHA MTENDAJI KATA YA MWAMKULU
13. NDG.RASHID MSYETE KAIMU MTENDAJI KATA YA KAZIMA
14. NDG.REVOCATUS NGOMENI MTENDAJI KATA YA NSEMULWA
15. NDG.ANGELO KATWANA KAIMU MTENDAJI KATA YA KAWAJENSE
16. NDG.JANUARY KAYUNGILO MTENDAJI KATA YA MISUNKUMILO
17. NDG.EMIL KATENDELE MTENDAJI WA KATA YA ILEMBO
18. NDG.FULGENCE MKULILA MTENDAJI WA KATA YA SHANWE
19. NDG.ARAM NDIMUBENYA MWENYEKITI WA CHAMA CHA CUF WILAYA
20. NDG. CYRILVIVIANUS MSHYOTA KATIBU WA ACT WAZALENDO WILAYA
21. NDG. RAFAEL B. SANGU KATIBU WA CHAMA TLP
22. NDG. SAID R. KASHINDYE MWENYEKITI WA CHAMA CHA UDP
23. NDG.ABRAHAM MAPUNDA MWENYEKITI WA CHAMA CHA CHADEMA
24. NDG. ABDUL S. SIGERA MWENYEKITI WA CHAMA CHA NCCR-MAGEUZI WILAYA
25. NDG.ADABUU JUMA KATIBU WILAYA WA CHAMA CHA ADC
26. NDG.LINUS SIWEZI KATIBU WA WILAYA WA CHAMA CHA UMD
27. NDG.FAUSTINE MWANAKATWE KATIBU WA MBUNGE WA JIMBO LA MPANDA MJINI
28. NDG.DEO CREDO MWANDISHI WA HABARI –TBC
29. NDG.REBECCA KIJA MWANDISHI WA HABARI-MPANDA REDIO
30. NDG.ZILPA JOSEPH MWANDISHI WA HABARI- ITV

**SEKRETARIETI**

NDG.WILLY MKANGA- KATIBU WA KAMATI

**MUHT: MMC/BARAZA/04/2017/2018: Agd:01: KUFUNGUA KIKAO**

Kabla ya kumkaribisha Mwenyekiti, Katibu alitoa maelezo kuwa Mkutano ulikuwa wa Nne kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ambapo taarifa za utekelezaji wa shughuli kutoka kwenye kata na shughuli zilizotekelezwa na idara mbalimbali zilipangwa kujadiliwa, pia akidi ya wajumbe waliokuwa wanahitajika katika Mkutano huo ilikuwa inatosha kutoa maamuzi.

Baada ya utangulizi huo alimkaribisha Mwenyekiti ambaye kabla ya kufungua kikao alianza kwa kutoa shukurani kwa Madiwani, Wataalam na Wananchi wote kwa kuhudhuria kwenye Mkutano huo.

Mwenyekiti alifungua mkutano mnamo Saa 05.10 Asubuhi

**MUHT: MMC/BARAZA/04/2017/2018:Agd:02: KURIDHIA AGENDA ZA MKUTANO**

Katibu alizisoma agenda zifuatazo;

1) KUFUNGUA KIKAO
2) KURIDHIA AGENDA ZA KIKAO
3) KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA MKUTANO WA TATU WA BARAZA LA MADIWANI
4) KUSOMA NA KUJADILI YATOKANAYO NA UTEKELEZAJI WA MKUTANO WA TATU WA BARAZA LA MADIWANI
5) TAARIFA ZA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI MBALIMBALI KUTOKA KWENYE KATA
6) MENGINEYO KWA IDHINI YA MWENYEKITI
7) KUFUNGA MKUTANO

Baada ya kusomwa agenda hizo, mkutano uliridhia zijadiliwe.

**MUHT:MMC/BARAZA/04/2017/2018:Agd:03: KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA NNE WA BARAZA LA MADIWANI**

Muhtasari wa Mkutano wa tatu wa baraza la madiwani ulisomwa na kuridhiwa na hivyo kutiwa saini kuwa kumbukumbu sahihi ya mkutano huo.

**MUHT: MMC/BARAZA/03/2017/2018:Agd:04: KUSOMA NA KUJADILI YATOKANAYO NA UTEKELEZAJI WA MAAGIZO YA MKUTANO ULIOPITA**

Mkutano uliridhia utekelezaji wa maagizo ya mkutano uliopita.

**MUHT:MMC/BARAZA/04/2017/2018:Agd:5:TAARIFA ZA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI KUTOKA KWENYE KATA.**

Mwenyekiti aliwakaribisha wenyeviti wa vikao vya Maendeleo ya kata (WDC) kuwasilisha taarifa ambapo kata zote 15 ziliwasilisha taarifa za utekelezaji

Baada ya taarifa zote kuwasilishwa na kujadiliwa, mkutano uliazimia kwamba, **kila Kata ihakikishe inaandaa taarifa inayoonesha idadi ya vikao vilivyofanyika katika robo husika.**

**MUHT: MMC/BARAZA/04/2017/2018:Agd:06: MENGINEYO KWA IDHINI YA MWENYEKITI**

Mwenyekiti aliagiza watendaji wa kata kuwasilisha taarifa mapema ili waandaji waweze kukamilisha makablasha kwa wakati.

**MUHT: MMC/BARAZA/03/2017/2018:Agd:7: KUFUNGA MKUTANO**

Katibu aliwashukuru wajumbe kwa ushiriki wao katika Mkutano. Alimkaribisha Mwenyekiti ambaye kabla ya kufunga Mkutano walizishukuru na kuzipongeza Kata ambazo ziliandaa taarifa vizuri.

Baada ya maelezo hayo aliwashukuru wajumbe na wananchi wote waliohudhuria Mkutano. Alifunga mkutano mnamo saa 7.48 Mchana.

**Umethibitishwa na kusainiwa na:-**

| | |
|---|---|
| **…………………………….** | **……………………………..** |
| **KATIBU** | **MWENYEKITI** |
| **Jina…………………………..** | **Jina……………………..** |

**Tarehe………………………………….**

**YATOKANAYO NA MKUTANO WA BARAZA LA MADIWANI KATA MKUTANO WA TAREHE 30.07.2018**

| AGENDA | AGIZO | MTEKELEZAJI | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| **MUHT:MMC/BARAZA/04/2017/2018:Agd:5** | kila Kata ihakikishe inaandaa taarifa inayoonesha idadi ya vikao vilivyofanyika katika robo husika. | MKURUGENZI | Agizo limetekelezwa<br><br>Taarifa za kata taarifa zote idadi ya vikao imeoneshwa. |

**KATA YA ILEMBO**
**TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA KAZI ZA MAENDELEO KATA YA ILEMBO KWA KIPINDI CHA JULAI – SEPTEMBA 2018 KATIKA KIKAO CHA BARAZA LA MADIWANI WA HALMASHAURI YA MANISPAA MPANDA**

**1. A UTANGULIZI**

Kata ya Ilembo ni miongoni mwa Kata **15** zilizomo katika Halmashauri ya Manispaa Mpanda, katika Wilaya ya Mpanda Mkoani Katavi.

**B. MIPAKA YA KATA**

Kata ya Ilembo imepakana na Kata zifuatazo:-

i. Upande wa Kusini imepakana na Kata ya Magamba
ii. Upande wa Magharibi imepakana na Kata ya Misunkumilo
iii. Upande wa Kaskazini imepakana na Kata ya Mpandahotel
iv. Upande wa Mashariki imepakana na Kata ya Kapalala.

**C. MAENEO YA UTAWALA**

Kata ya Ilembo ina mitaa **3**
(i) Mtaa wa Mapinduzi (ii) Mtaa wa Kasimba (iii) Mtaa wa Ilembo

**D. IDADI YA WATU**

Kwa mujibu wa sensa ya watu na maendeleo ya makazi ya mwaka **2012** kata ya Ilembo inajumla ya Kaya zenye Idadi ya watu kwa mchanganuo ufuatao:-

| **MITAA** | **KAYA** | **IDADI YA WATU** | | | **WENYE UWEZO** | | | **WASIO NA UWEZO** | | | **WALEMAVU** | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **ME** | **KE** | **JML** | **ME** | **KE** | **JML** | **ME** | **KE** | **JML** | **ME** | **KE** | **JML** |
| MAPINDUZI | **204** | 522 | 540 | **1062** | 363 | 439 | **802** | 256 | 266 | **522** | 2 | 3 | **5** |
| KASIMBA | **338** | 519 | 604 | **1123** | 368 | 396 | **764** | 176 | 183 | **359** | 1 | 2 | **3** |
| ILEMBO | **374** | 548 | 612 | **1160** | 358 | 437 | **795** | 175 | 192 | **367** | 3 | 1 | **4** |
| JUMLA | **916** | 1607 | 1738 | **3345** | 1089 | 1272 | **2361** | 1249 | 641 | **1248** | 6 | 6 | **12** |

**E. SHUGHULI ZA KIUCHUMI**

Wananchi wakazi wa Kata hii wanafanya shughuli zifuatazo:-

i. Wafanya biashara na wajasiriamali
ii. Wakulima wadogo na wafugaji
iii. Watumishi wa Serikali na wafanya kazi wa mashirika.
iv. Wachimbaji wadogo wa madini mbalimbali.

**F. HUDUMA ZA KIJAMII**

Kata ya Ilembo ina huduma za Kijamii kama zifuatazo:-

(a) Shule za Msingi (i) S/M Mapinduzi (ii) S/M Ilembo
(b) Shule za Sekondari (i) Kasimba Sekondari (ii) Sun Sekondari
(c) Shule za Awali (i) Motherland (ii) Sumbilo
(d) Ushauri na tiba (i) Kituo cha Afya Kasimba.

**G. HALI YA UONGOZI**

Kata ya Ilembo ina viongozi wafuatao kwa nyazifa zao:-

(i) Diwani wa Kata (ii) Afisa Mtendaji Kata (iii) Wenyeviti wa Mitaa
(iv) Afisa Mtendji Mtaa (v) Wataalam wa kada mbalimbali.

### H. IDADI YA WATUMISHI KILA IDARA

| IKAMA | UTAWALA | SEKONDARI | MSINGI | KILIMO | AFYA | JAMII |
|---|---|---|---|---|---|---|
| MAHITAJI | 4 | 35 | 30 | 2 | 2 | 1 |
| WALIOPO | 2 | 29 | 27 | 1 | - | 1 |
| PUNGUFU | 2 | 6 | 3 | 1 | 2 | 1 |

**TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA ZA MIRADI YA MAENDELEO JULAI – SEPTEMBA 2018**

Kwa kipindi cha **Julai – Septemba 2018** Kata ilipokea fedha za maendeleo **Tshs. 400,000,000/=** na kutumia kiasi cha shilingi **68,465,000/=** sawa na **99%** ya makadilio ya fedha za maendeleo **Tshs. 453,000,000/=**

| MTAA | AINA YA MRADI | CHANZO CHA FEDHA | FEDHA | | | UTEKELEZAJI | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | TOLEWA | TUMIKA | BAKI | | |
| Kasimba | Ujenzi wa maabara, wodi ya wazazi, nyumba ya mtumishi, jengo la upasuaji na jengo la kuhifadhi maiti | Halmashauri | 400,000,000/= | 68,465,000/= | 331,535,000/= | Ujenzi wa majengo yote umefikia hatua ya kufunga renta | Tumeagiza saruji toka Mtwara katika kiwanda cha DANGOTE mifuko 1200 |
| Ilembo | Ujenzi wa matundu 20 ya vyoo S/M Ilembo | - Mfuko wa jimbo<br>-Wananchi | 4,000,000/=<br>1,000,000/= | 4,000,000/=<br>1,000,000/= | -<br>- | Ujenzi wa matundu 10 yamekamilika na kuanza kutumika bado matundu 10 | Tunahitaji fedha za ujenzi wa matundu 10 Tshs. 10,000,000/= |
| Kasimba | Ujenzi wa kivuko cha mto Kawalyowa | Mbunge wa Jimbo | 1,000,000/= | 1,000,000/= | - | Ujenzi wa nguzo 4 umekamilika bado hatua za kufunika juu ya kivuko hicho kazi imesimama | Tarehe 28/9/2018 wananchi walikubali kuchanga Tshs. 1,000/= kila kaya |

## 2A. DIRA MAALUM

Ili kufanikisha utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo lazima kuwepo na malengoya mpango shirikishi utakaoiongoza jamii.

i. Kukusanya takwimu za mazingira, kitaalam, nyakati, kijamii na kiuchumi.
ii. Kuweka vipaumbele katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.
iii. Kuweka malengo shabaha na kubuni mikakati ya ufumbuzi katika utekelezaji.
iv. Kupitisha na kuthibitisha rasmu ya mpango wa maendeleo katika utekelezaji.
v. Kuweka taratibu za utekelezaji wa mpango kabambe ulio azimiwa na wananchi.
vi. Kufuatilia na kufanya tathimini ya mpango ulio kuwa umeandaliwa kwa maendeleo.
vii. Kuwepo na bajeti itakayoongoza utekelezaji wa mpango huu maalum.
viii. Kutoa taarifa ya mapato na matumizi ya utekelezaji wa mpango.

**3A.VIKAO NA MIKUTANO**

Kwa kipindi cha**Julai– Septemba 2018** Kata hii imeendesha vikao vya kamati ya maendeleo **2**kikao maalumu **17/07/2018,** kikao cha kisheria **05/10/2018,** ambapo mikutano ya hadhara ilifanyika Mtaa wa Ilembo **08/09/2018**na Mtaa wa Kasimba katika eneo la Kawalyowa tarehe **28/09/2018**kuwahamasisha wananchi katika utekelezaji wa kazi za maendeleo.

B. **RATIBA YA USAFI WA MAZINGIRA**

| S/N | ENEO LA USAFI | WASIMAMIZI | MSIMAMIZI MKUU |
|---|---|---|---|
| 1. | Kufanya usafi wa mazingira katika maeneo ya stendi kuu ya mabasi na Mtaa wa Ilembo | Ester Athanael (MEO) | Grace Kunchela (EHO) |
| 2. | Kufanya usafi katika maeneo ya kituo cha Afya Ilembo na Mtaa wa Kasimba | Jennifer Boaz (MEO) | Bisetsa Joseph (AEK) |
| 3. | Kufanya usafi mazingira Mtaa wa Mapinduzi | Joyce Peter (WCDO) | Herieth Mhanda (WAEO) |

**C. DHAMIRA HALISI**

i. Kuondoa migogoro kati ya Wakulima na Wafugaji ili kudumisha amani.
ii. Kuimarisha ulinzi shirikishi wa jamii kwa maendeleo ya wananchi.
iii. Kukaguwa usafi wa mazingira katika maeneo ya makazi na Biashara.
iv. Kuendelea kuwabaini wageni wanaoingia na kutoka katika mitaani.
v. Kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa shughuli za kijamii na kiuchumi.
vi. Kusimamia uundaji wa vikundi vya kiuchumi kati ya vijana / wanawake.
vii. Kuratibu na kusimamia mapambano dhidi ya rushwa na madawa kulevya.
viii. Kuendesha vikao na mikutano ili kutatua matatizo yanayo wakabili wananchi.

**4A.SEKTA YA AFYA KINGA**

Kwa kuzingatia kanuni za Afya bora kila mtu ameelekezwa yafuatayo:-

i. Kuwaelimisha wananchi juu ya ujenzi wa vyoo bora vinavyotumia maji.
ii. Kuwahamasisha wananchi kufanya usafi wa mazingira katika maeneo yao.
iii. Kuendelea kuwaelimisha wananchi kujiunga na mfuko wa Bima ya Afya CHF.
iv. Kuwahamasisha walengwa wa TASAF kujiunga na Tiba kwa kadi(matibabu)

**B. SEKTA YA MAJI**

Kata hii inakabiliwa na tatizo la Maji kwa kiasi kikubwa kwa kuwa maji toka Ikolongo yanapatikana mara **3** kwa wiki katika Mtaa wa Ilembo ambapo Mtaa wa Mapinduzi hakuna maji kabisa. Aidha visima **2** kilichopo S/M Mapinduzi na S/M Ilembo vyote vilishaharibika. Hivyo tunaomba mamlaka ya maji safi na usafi wa mazingira watengeneze visima ili viweze kutoa hudumma kwa wananchi.

**C. SEKTA YA UTAWALA**

i. kusimamia na kuimarisha ulinzi shirikishi jamii wa raia na mali zao.
ii. Kusimiamia na kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo
iii. Kusimamia na kufuatilia utendaji kazi wa wataalamu wote
iv. Kusimamia utawala bora kwa kuzingatia sheria zilizopo
v. Kusimamia n kushiriki katika zoezi la usafi wa mazingira
vi. Kusimamia na kudhibiti utoro na mimba kwa wanafunzi shuleni
vii. Kusimamia utendeshaji wa vikao vya ndani na mikutano ya hadhara
viii. Kusuluhisha na kutatua migogoro mbalimbali inayojitokeza.

**D. SEKTA YA ELIMU S/M NA SEKONDARI**

(i) **Kata hii ina shule 3 ambapo 2 S/M na 1 Shule ya Sekondari**.

| SHULE | **AWALI** | | | **WALIMU** | | | **WANAFUNZI** | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **WV** | **WS** | **JML** | **MH** | **WP** | **PF** | **WV** | **WS** | **JML** |
| Ilembo | 274 | 140 | 134 | 22 | 17 | 05 | 365 | 400 | 765 |
| Mapinduzi | 61 | 32 | 29 | 13 | 10 | 05 | 120 | 119 | 239 |
| Sek-Kasimba | - | - | - | 32 | 26 | 06 | 370 | 380 | 750 |
| **Jumla** | **335** | **172** | **163** | **67** | **53** | **14** | **855** | **899** | **1754** |

**(ii) Takwimu halisi ya miundombinu ya shule S/M & Seki**

| **SHULE** | **MADARASA** | | | **NYUMBA** | | | **VYOO** | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **HT** | **YP** | **PF** | **HT** | **YP** | **PF** | **HT** | **YP** | **PF** |
| Mapinduzi | 10 | 5 | 5 | 10 | 1 | 9 | 14 | 8 | 6 |
| Ilembo S/M | 19 | 7 | 12 | 17 | 1 | 16 | 36 | 18 | 18 |
| Kasimba Sek | 20 | 12 | 8 | 26 | 3 | 23 | 39 | 18 | 21 |
| **Jumla** | **49** | **24** | **25** | **53** | **5** | **48** | **89** | **44** | **45** |

**E. SEKTA YA MAENDELEO JAMII**

Kata hii ina vikundi vya wajasiria mali **8** kama:-
**(i)** Morning Star **(ii)** Twikalane Group **(iii)** Jioneegroup **(iv)** Muungano **(v)** Development Front line **(vi)** Alfa Group **(vii)** Vijana group **(viii)** Change Revolution ambao bado wanadaiwa kurejesha mkopo. Aidha shughuli zilizofanyika katika idara.

i. Kuendelea kuwahamasisha wananchi kuunda vikundi na kusajili.
ii. Kuratibu na kutoa elimu juu ya uendeshaji wa miradi.
iii. Kusimamia uibuaji wa miradi ya kilimo na mifugo.
iv. Kuendelea kutoa elimu juu ya kudhibiti maambukizi mapya ya VVU.
v. Kutoa Elimu ya kudhibiti mimba za ututoni kwa wanafunzi.
vi. Kufuatilia urejeshaji wa mikopo ya fedha kwa vikundi.

**F. SEKTA YA UTUNZAJI MAZINGIRA**

Kwa kipindi hiki kazi zilizofanyika ni pamoja na

i. Kuwahamasisha wananchi kutunza vyanzo vya maji.
ii. Kuendelea kutoa elimu juu ya ufugaji wa kutumia zizi.
iii. Kuwashauri wafugaji kuupunguza idadi ya mifugo yao.
iv. Kutoa elimu juu ya wafugaji kudhibiti uzurulaji wa mifugo.
v. Wafyatuaji wa matofari kupata vibali na kuchangia tofari.

**G. SEKTA YA KILIMO NA MIFUGO**

Katika sekta kilimo, mifugo na ushirika kazi zilizofanyika ni pamoja na

i. Kuwahamasisha wakulima juu ya kulima mazao ya kinga ya njaa viazi na mhogo.
ii. Kuwepo shamba darasa na shamba la mfano kwa kuwafundisha wakulima
iii. Kuwaandaa wananchi kuwa tayari kuanza maandalizi ya kulima mashamba.
iv. Kutoa mafunzo ya kujenga uwezo kwa vikundi vya wakulima na wafugaji
v. Kutoa maelekezo juu ya matumizi sahihi ya pembejeo za kilimo na mifugo.
vi. Kupiga chapa ng'ombe **704** za wafugaji **18** na kutoa chanjo ya mapafu.

**vii. 5A. DIRA YA TAIFA YA MAENDELEO 2015 – 2025**

i. Kuimarisha mshikamano, amani na utulivu kwa maendeleo
ii. Kuimarisha uchumi imara unaohimili ushindani
iii. Kuondoa umaskini uliokithiri katika maisha ya kila siku
iv. Kuwa jamii iliyoelimika na inayohitaji kujifunza zaidi
v. Kupunguza tofauti ya kipato kati ya walionacho na wasiokuwanacho
vi. Kuwa na maisha bora na mazuri yenye Afya kwa nguvu kazi
vii. Kuimarisha utawala bora kwakuzingatia sheria katika jamii.

**B. SEKTA YA AFYA TIBA**

Kata ya Ilembo ina Kituo 1 cha Afya kinachoendelea kutoa huduma kwa Wananchi ambapo huduma zinazotolewa ni pamoja na:-

i. Huduma za upimaji wa Afya (Maabara)
ii. Huduma za wagonjwa wa nje (OPD)
iii. Hudma za chanjo mbalimbali
iv. Huduma za mama na mtoto (RCH)

**C.UPIMAJI WA VIWANJA**

Kata hii ilipokea Makampuni binafsi **2** ya upimaji ambapo **Ndg. JUDE SHILIMA**ni msimamizi wa Kampuni ya **GREEN AFRICA LAND CONSULTANT** ambayo imepima eneo la Kasimba Darajani kazi bado inaendelea na **Ndg. GEOFREY NJERU** ni msimamizi wa Kampuni ya **SOUTH PEAK & MACPANDO CROSSLAND SURVEYING** ambayo inaendelea kufanya kazi ya upimaji viwnaja katika eneo la Kawalyowa.

Aidha Makampuni haya mawili **(2)** yote yanataka kupima viwanja eneo la Sentamatrubai ambapo Ofisi ya Kata iliwaelekeza Kamati ya Upimaji kwa niaba ya Wananchi wa eneo hilo kuwa wasubiri maelekezo toka Idara ya Ardhi.

**E. ULINZI NA USALAMA**

Katika kutekeleza suala la ulinzi na usalama wa raia na mali zao Kata ya Ilembo tumefanya vikao **2** vya kamati ya ulinzi na usalama na kuendesha mikutano ya hadhara **2** kuwahamasisha wananchi kushiriki ulinzi shirikishi Jamii. Ambapo kipindi cha **Julai –Septemba 2018** vikundi vya mitaa ya Kasimba, Ilembo, Mapinduzi pamoja na eneo la Kawalyowa ulinzi uliimalika ambapo vikudi vilifanya kazi kikamilifu na ulisaidia sana kupunguza uharifu mitaani kwa sasa vikundi vimesambalatika na kupelekea kujitokeza kwa vibaka na wezi mitaani. Hivyo jitihada zinafanyika za kuunda upya vikundi vya ulinzi shirikishi. Ambapo kamati 3 za utekelezaji zimeshaundwa

1. Kamati ya kutatua migogoro kati ya wakulima na wafugaji yenye wajumbe 15 wafugaji 3, wakulima 3, wenyeviti wa mitaa 3, watendaji wa mitaa 2, wajumbe wa mitaa 3, na afisa mtendaji wa kata 1.
2. Kamati za usimamizi wa miradi ya maendeleo katika Kituo cha Afya Ilembo
   Kamati ya manunuzi 8, kamati ya mapokezi 7, kamati ya ujenzi 10
3. Kamati ya miundombinu ya amani (usalama) wenyeviti 3, wataalam 5, watendaji wa mitaa 2, viongozi wa dini 3, wafanyabiashara 4, mtendaji wa kata 1

**F. SEKTA YA UKIMWI**

Kwa kipindi cha Januari – Septemba 2018 kazi zilizofanyika katika sekta hii ni pamoja na

i. Kuendesha vikao vya ndani na nje katika kuwahamasisha wananchi kupima afya.
ii. CBHS Kuwatembelea wagonjwa majumbani kujua afya zao zinavyoendelea.
iii. Kutoa elimu juu ya kukinga familia zao zilizoko katika mazingira hatarishi.
iv. Kuhamasisha na kutoa elimu juu ya upimaji wa hiari katika kituo cha Afya.

v. Kufuatilia walengwa (WAVIU) walioacha dawa na kuwarudisha CTC.

**CHANGAMOTO**

i. Barabara toka Kata ya Ilembo hadi Kata ya Itenka ni chakavu na mbovu sana.
ii. Kukatika kwa Daraja linalotenganisha mtaa wa Aitel na Kawalyowa ni shida.
iii. Migogoro kati ya wakulima na wafugaji (mifugo kuhalibu mazao ya wakulima)
iv. Upungufu wa vitendea kazi na watumishi katika kituo cha Afya Ilembo.
v. Uhaba wa maji ya kunywa katika mtaa wa Mapinduzi kumewaathiri wananchi.
vi. Uwepo wa mapagara na viwanja visivyo endelezwa unasababisha wezi na vibaka.
vii. Wananchi wanaoishi eneo la Misengeleni hawataki kuhudhuria mikutano ya hadhara
viii. Ukosefu wa kisima cha maji katika kituo cha Afya Ilembo kunachelewesha ujenzi.
ix. Ukosefu wa vyombo vya usafiri kama Pikipiki kunasababisha utekelezaji wa majukumu kutofanyika kwa wakati.

**MAPENDEKEZO**

i. Halmashauri ya Manispaa Mpanda iwanyang'anye wamiliki wa mapagala na viwanja
ii. Mhandisi wa ujenzi awasiliane na tarula ili waweze kutengeneza barabara na Daraja
iii. Mamraka ya maji safi na usafi wa mazingira wapeleke bomba za maji Mapinduzi

**MHE. TUSIGWEGE MWAKYUSA**
DIWANI WA KATA ILEMBO

**KATA YA KASHAULILI**

**TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 KWA KIPINDI CHA ROBO YA KWANZA KUANZIA JULAI – SEPTEMBA, 2018**

**UTANGULIZI.**

Kata ya Kashaulili ni miongoni nwa Kata tisa (**9**) zilizomo Tarafa ya Kashaulili Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda, Wilaya ya Mpanda Mkoa wa Katavi.

Kata ya Kashaulili inajumla ya wakazi wapatao **8546** wakiwemo wanaume **3858**na wanawake **4688** kaya **1016.**

| KATA | IDADI YA WATU WOTE | | | WENYE UWEZO WA KUFANYA KAZI | | | WASIO NA UWEZO WA KUFANYA KAZI | | | WALEMAVU | | | WATOTO WANAOISHI MAZINGIRA HATARISHI | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1016 | **ME** | **KE** | **JML** | **ME** | **KE** | **JML** | **ME** | **KE** | **JML** | **ME** | **KE** | **JML** | **ME** | **KE** | **JML** |
| | 3885 | 4688 | 8546 | 2282 | 2751 | 5033 | 1597 | 1728 | 3325 | 32 | 31 | 63 | 61 | 64 | 125 |

**<u>MIPAKA YA KATA</u>**

Kata ya Kashaulili imepakana na Kata za:-

- Upande wa Mashariki imepakana na Kata ya Nsemulwa.
- Upande wa Kaskazini imepakana na Kata ya kawajense.
- Upande wa Magharibi imepakana na Kata ya Makanyagio.
- Upande wa Kusini imepakana na Kata ya Majengo.

**<u>SHUGHULI ZA KIUCHUMI</u>**

Wananchi wa Kata hii ya Kashaulili wanajishughulisha na shughuli za biasharaya kubwa na wajasiliamali wadogo wakulima kwa kulimia nje ya Kata hii wanafanya shughuli zao za kilimo kwa Kata za Kakese, Mwamnkulu, Magamba n.k. Pia ni wachimbaji wa madini kwa kutumia Kata zenye madini. Watumishi mafundi wa fani mbalimbali.

**<u>IDADI YA WATUMISHI KWENYE KATA</u>**

| IDARA | MAHITAJI | WALIOPO | PUNGUFU | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|
| UTAWALA | 4 | 3 | 1 | Tunahitaji mtendaji wa Mtaa 1 |
| ELIMU | 24 | 34 | 57 | Walimu hawatoshi kulingana na idadi |
| AFYA | 1 | 1 | - | Kata moja na anafanya kazi vizuri |
| KILIMO | 1 | 1 | - | Anaudumia Kata Nne (4) |
| MAENDELEO YA JAMII | 1 | 1 | - | Anaudumia Kata mbili (2) |
| UVUVI | 1 | 1 | - | Anaudumia Kata mbili (2) |

**VIONGOZI WALIOPO KATIKA KATA**

| VIONGOZI WA KUCHAGULIWA | MAHITAJI | WALIOPO | PUNGUFU | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|
| WAH. MADIWANI | 2 | 2 | - | Wa Kata 1 viti maalumu 1 |
| WENYEVITI WA MITAA | 3 | 2 | 1 | Wote wametoka chama tawala CCM |
| WAJUMBE SERIKALI ZA MTAA | 15 | 13 | 2 | Wamehama |

**HUDUMA ZA JAMII ZILIZOPO**

Kata ya Kashaulili ina huduma za jamii kama ifuatavyo:-

1. **SHULE ZA MSINGI TATU, AMBAZO NI**
   (i) Shule ya msingi Kashaulili
   (ii) Shule ya msingi Mwangaza
   (iii) Shule ya msingi Uhuru

2. **MASOKO.**
   (i) Soko la Kuu
   (ii) Soko la Buzogwe

3. **KITUO KIDOGO CHA MABASI**
4. **HUDUMA ZA KIBENK.**
   **(i) NMB, POSTA N.K**
3. **IDADI YA WANAFUNZI KATIKA SHULE**.

| SHULE | WALIMU | | | WANAFUNZI | | | MADARASA | | | MADARAJA | | | VYOO | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | ME | KE | JML | ME | KE | JML | HIT | TAP | PUNG | HIT | TAP | PUNG | HIT | TAP | PUNG |
| Kashaulili | 6 | 15 | 21 | 552 | 615 | 1167 | 27 | 8 | 21 | 365 | 365 | - | 44 | 10 | 34 |
| Mwangaza | - | - | - | 614 | 608 | 1222 | 27 | 10 | 17 | 357 | 357 | - | 42 | 16 | 26 |
| Uhuru | 8 | 10 | 18 | 528 | 516 | 1039 | 16 | 3 | 13 | 316 | 276 | 40 | 37 | 10 | 27 |
| **JUMLA** | **23** | **34** | **57** | **1508** | **1099** | **3137** | **70** | **21** | **51** | **1038** | **998** | **40** | **123** | **36** | **87** |

- **TAARIFA ZA MAPOKEZI YA FEDHA ZA RUZUKU ZA SHULE ZA MSINGI KATIKA ROBO YA KWANZA KUANZIA JULAI – SEPTEMBA, 2018**

| SHULE | JUALI | AGOST | SEPTEMBA | JUMLA |
|---|---|---|---|---|
| KASHAULILI | 912,229.61 | 912,229.61 | 912,229.61 | 2,736,688.83 |
| MWANGAZA | 681651.03 | 681651.03 | 681651.03 | 2,044,953.09 |
| UHURU | 609,576.01 | 609,576.01 | 609,576.01 | 1,828,728.03 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **JUMLA** | **2,203,456.65** | **2,203,456.65** | **2,203,456.65** | **6,610,369.95** |

**WANAFUNZI WALIOFANYA MTIHANI WA DARASA LA VII**

| SHULE | WALIOSAJILIWA | | | WALIOFANYA MTIHANI | | | AMBAO HAWAKUFANYA | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | WAV | WAS | JML | WAV | WAS | JML | WAV | WAS | JML |
| UHURU | 42 | 40 | 82 | 41 | 37 | 78 | 1 | 3 | 4 |
| KASHAULILI | 46 | 48 | 94 | 42 | 46 | 88 | 4 | 2 | 6 |
| MWANGAZA | 48 | 55 | 103 | 45 | 52 | 97 | 3 | 3 | 6 |
| **JUMLA** | **136** | **143** | **297** | **128** | **135** | **263** | **8** | **8** | **16** |

- **UTORO SHULENI**

Swala la utoro kwa wanafunzi limepungua kidogo baada ya wazazi wa watoto kuchukuliwa hatua za Kisheria bado upo mtoro mdogo wa rejareja,

| WAZAZI WALIOFIKISHWA BARAZA LA KATA WALIOFIKISHWA | WALIO HUKUMIWA | FAINI AU ADHABU WALIYOPEWA |
|---|---|---|
| 17 | 4 | TSH. 200,000/= WENGINE WALIPEWA ONYO UTORO ULIKUWA WA SIKU MBILI AU TATU |

Baada ya kufikisha kesi hizo Baraza la Kata, ilionekana watoto sugu walikuwa 4, waliyokuwa wamehama 3 na 10 waliletwa kimakosa utoro wao ni siku mbili au tatu. Mwalimu alikiri kuwa hawakuchambua vizuri.

**ORODHA NA IDADI YA WAZAZI WA WATOTO WATORO SHULE YA MSINGI UHURU.**

| S/N | JINA LA MZAZI | JINA LA MWANAFUNZI | UAMUZI WA BARAZA |
|---|---|---|---|
| 1. | SYLIVESTO DAUDI | MAIKO SYLVESTO | AMEHAMA |
| 2. | ISSA RAMADHAN | ISMAIL A. SANZAGALA | HANA HATIA |
| 3. | IDRISA KHAMIS | YASIN IDRISA | AMELIPA FAINI |
| 4. | FESLAUS GERLAD | GPDFREY GERLAD | HANA HATIA |
| 5. | ALFRED METHOD | METHOD ALFRED | HNA HATIA |
| 6. | ANGELO MSHAYI | ELIA A. MSHAYI | AMELIPA FAINI |
| 7. | ADAM A. MBOGA | ADAM A. MBOGA | HANA HATIA |
| 8. | FRANK MIKSON | DIANA FRANK | HANA HATIA |
| 9. | SAID KIANTO | NUSRA SAID | HANA HATIA |
| 10. | STEPHANO LUCAS | OBED JAFETY | HANA HATIA |
| 11. | GETRUDA JEMSI | PAULINA EMANUEL | AMEHAMA |
| 12. | STUMAI BAKARI | SALUM RAJABU | AMELIPA FAINI |
| 13. | ZAINABU SHABANI | ZAMDA HUSSEIN | AMELIPA FAINI |
| 14. | TATU MOHAMED | MIKIDADI BASHIRI | HANA HATIA |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 15. | CHARLES MAIGE | PETER CHARLES | HANA HATIA |
| 16. | ELIZABETH EDWARD | SUZANA ELIAS | AMEHAMA |
| 17. | KHAMIS KASEGEZYA | HALIMA KHAMIS | HANA HATIA |

Wazazi wengine wamepewa onyo la mdomo.

**1. AFYA**

**A. MALENGO YA IDARA;**

1. Uzoaji wa takataka katika masoko, soko kuu, soko la Buzogwe na Stendi
2. Ukaguzi wa usafi wa Mazingira katika nyumba za kuishi
3. Ukaguzi wa majengo ya biashara.

**B. KAZI ZILIZOFANYIKA;**

1. Idara imekuwa mstari wa mbele kuhakikisha barabara kuu na mifereji inakuwa safi.
2. Kusimamia ukusanyaji, uzoaji na utupaji wa taka ili kuhakikisha kata ya Kashaulili inakuwa safi.
3. Kusimamia na kuhamasisha usafi katika nyumba za kuishi katika mitaa yote.

Idara ikishirikiana na Mtendaji wa Mtaa na Kata katika Jumamosi za mwisho wa mwezi tunfanya kazi za kuhamasisha wananchi kufanya usafi katika maeneo yao na kusimamia uzoaji wa taka katika masoko.

**2. UKAGUZI WA MAJENGO YA BIASHARA**

| S/N | AINA YA BIASHARA | MAJENGO YALIYOKAGULIWA | NOTSI ZILIZOTOLEWA | MAJENGO YALIYOFUNGWA |
|---|---|---|---|---|
| 1. | MAMA LISHE | 85 | 85 | 5 |
| 2. | BUCHA | 12 | 12 | 0 |
| 3. | GUEST HOUSE | 24 | 18 | 0 |
| 4. | SALON | 18 | 3 | 0 |
| 5. | MIGAHAWA | 3 | 3 | 0 |

**C. MAFANIKIO;**

- Idara imeweza kudhibiti magonjwa ya mlipuko kwa muda mrefu, mfano; hakuna kipindupindu

- Kashaulili inaendelea kupendeza kwasababu ya kazi nzuri inayofanywa na Idara ya Afya ya kusimamia na kuhamasisha usafi ikiwa ni pamojana ushirikiano uliopo toka kwa watendaji wa kata na Mwenyeviti wa Serikali za mitaa.

- Idara ya Afya imeweza kusimamia zoezi la kupima Afya watumishi wote wanaohudhuria katika huduma za kijamii mfano. Mama lishe, Salon. Jumla ya Watu 230 wamepima Afya katika Kata ya Kashaulili katika kituo cha Afya Mwangaza. Hivyo idara imechangia kuingiza mapato **Tshs. 1,150,000/=.**

❖

**D. CHANGAMOTO**

- ❖ Pamoja na idara kuingiza pesa kupitia zoezi la kupima Afya, lakini ofisi ya Afya hakuna hata karatasi hivyo kuwa kero unapowaambia wananchi waende wakatoe kopi wao wenyewe.

- ❖ Wafanyabiashara katika masoko kutofika asubuhi ya mwisho wa mwezi kufanya usafi katika maeneo yao.

- ❖ Wafanyabiashara 18 hawakufanya usafi siku ya Jumamosi ya mwisho wa mwezi na wengine baadhi yao hawakufika kabisa tuliwafikisha Baraza la Kata na kufunguliwa kesi lakini waliomba msamaha hawatarudia tena.

**E. MAPENDEKEZO**

- ❖ Tunashauri tupewe asilimia kupitia zoezi la kupima Afya ili tununue vitendea kazi kama karatasi.

- ❖ Tunashauri gari la takataka lipatiwe mafuta kwa utaratibu maalumu ili kila siku liweze kuondosha taka ili Mji wetu uwe katika mazingira bora.

- ❖ Sheria itumike ili kudhibiti hali hiyo ya wafanyabiashara

**UHARIBIFU WA MAZINGIRA**

- Mtaa wa kotazi kuna wananchi wanao fanya shughuli za kilimo cha bustani na ufyatuaji wa tofali kwenye bonde, kwahiyo kuna wafyatuaji wanne waliopata vibali na kulipa **Tshs. 20,000/=** kwa hiyo bado kuchoma tofali zao ili tuweze kupata asilimia **7%** za tofali.

**F. SEKTA YA KILIMO;**

Shughuli zilizofanyika katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka kuanzia Julai hadi Septemba 2018 katika Idara ya Kilimo, Chakula, Viwanda na Ushirika.

1. Kuwahamasisha wakulima kuandaa mashamba na mbegu mapema

2. Kuwahamasisha kilimo cha korosho na pamba

3. Kuwahamasisha ufugaji wa kuku wa mayai na nyama na uchimbaji wa mabwawa ya samaki

4. Jumla ya wakulima **41** wametembelewa na kupewa ushauri juu ya matumizi bora ya viwatilifu

5. Zoezi la ukusanyaji wa takwimu za wakulima linaendelea kufanyika ili kuhusisha daftari la mkulima.

6. Jumla ya wakulima **34** wamepatiwa elimu juu ya matumizi bora ya pembejeo pamoja na kuzingatia kanuni bora za kilimo.

## G. MIFUGO

Kazi zilizofanyika

- Jumla ya ng'ombe wanne **(04)** wapepatiwa chanjo dhidi ya homa ya mapafu(CBPP)

- Vikundi viwili (**02**) vya wafugaji kuku wameshauriwa juu ya ujenzi bora wa mabanda ya mifugo yao.

- Jumla ya mbuzi **51**na kondoo **11** wamechinjwa na kukaguliwa na Afisa mifugo.

## SHUGHULI ZA SEKTA YA UVUVI ZILIZOTEKELEZEKA KUANZIA JULAI – SEPTEMBA 2018, KATA YA KASHAULILI.

### SHUGHULI ZILIZOTEKELEZEKA

- Ukaguzi wa dagaa zilizotoka Mwanza ambazo ni jumla ya kilogram 24,000kgs zilikaguliwa kwa gunia **308** zilifika Mpanda na kuzikagua zikiwa kwenye kiwango kizuri kwa matumizi ya walaji.

- Kukagua samaki wabichi na wakavu katika stendi na sokoni na kubaini baadhi ya matenga kuwa na samaki wadogo na kuchukua hatua za kuwaondoa sokoni.

- Kukagua wafanyabiashara wa samaki walio na leseni za biashara ya samaki na vibali vya samaki. Nakubaini baadhi ya wauza samaki kutokuwa na leseni ila ukaguzi unaendelea ili kuongeza na kufanya wauza samaki wote kuwa na leseni.

- Kufanyika kwa doria tatu katika soko kubwa na stend ili kutambua samaki zilizo sokoni zinafaa kuliwa au hapana ila samaki zinalidhisha kutokana na kuwepo kwa samaki wakubwa na zilizo na uhalali wakuliwa. Ila zoezi la doria ni endelevu.

### CHANGAMOTO

- Ukosefu wa mizani ya kupimia mizigo ya samaki inayokamatwa ili kujidhihilisha kiasi cha samaki au dagaa zisiotakiwa sokoni.

## SEKTA YA MENDELEO YA JAMII JINSIA NA WATOTO

- ***Kazi zilizotekelezwa***
  1. Kuhamisha uundaji wa vikundi katika mitaa mitatu ya Kata ya Kashaulili
     - Vikundi vilivyoundwa ni kikundi kimoja

| JINA LA KIKUNDI | IDADI | JINSI | | MTAA | SHUGHULI |
|---|---|---|---|---|---|
| | | ME | KE | | |
| BGCO | 9 | 3 | 6 | BUZOGWE | Kutoa Elimu ya Usafi wa Mazingira |

2. Kufuatilia marejesho ya mkopo kwa vikundi vilivyokopeshwa

| JINA LA KIKUNDI | KIASI CHA MKOPO | MAREJESHO | MAELEZO/ BAKI |
|---|---|---|---|
| KIKUNDI CHA GIFTSHEZA | 4,000,000/= | 336,000/= | 3,664,000/= |
| KIKUNDI CHA WAJANE | 3,000,000/= | 572,000/= | 280,000/= |
| KIKUNDI CHA SHOOTING | 3,000,000/= | 550,000/= | 1,100,000/= |
| KIKUNDI CHA AMANI | 1,000,000/= | 117,000/= | 175,000/= |

Kati ya hivyo ni kikundi kimoja cha Amani Agriculture ndicho kipo nje ya mkataba.

**VIKUNDI AMBAVYO HAVI KUREJESHA**

1. Kikundi cha RAHAMANI
2. Kikundi cha Katavi Youth

**ULINZI NA USALAMA**

- Katika kipindi cha robo ya kwanza kuanzia Julai hadi Septemba hakuna matukio makubwa yaliyotokea.
- Kilifanyika kikao kimoja cha kamati ya ulinzi na usalama cha Kata

**CHANGAMOTO**

- Usalama mdogo katika eneo la uwanja wa mpira(Azimio) hasa masaa ya usiku. Tunaomba eneo hilo liwekewe ulinzi au iwekewe mwekezaji nyumba iliyokuwa inafanyiwa biashara ya Bar eneo la Misitu.

**(i) MIUNDO MBINU – BARABARANI**

- Katika kipindi cha Julai hadi Septemba, 2018**.** Kata ya Kashaulili inaendelea na matengenezo ya barabara za Rami Km. **7.**

**VIKAO VILIVYOFANYIKA KATIKA ROBO YA KWANZA**
**JUALI – SEPTEMBA, 2018**

| TAREHE | AINA YA KIKAO | IDADI |
|---|---|---|
| 27/09/2018 | KAMATI YA UKIMWI YA KATA | 1 |
| 21/09/2018 | KAMATI YA MAZINGIRA | 1 |
| 21/09/2018 | KAMATI YA MALALAMIKO | 1 |
| 04/10/2018 | KAMATI YA MAENDELEO YA KATA | 1 |
| - | SERIKALI ZA MTAA KILA MTAA (3) | 9 |
| 04/10/2018 | ULINZI NA USALAMA | 1 |
| | ULIFANYIKA MKUTANO WA MKUU WA MKOA | |
| | ULIFANYIKA MKUTANO WA MKUU MKOA SOKO KUU | |
| | ULIFANYIKA MKUTANO MH. MBUNGE | |
| | | |

**(ii) TAARIFA YA BARAZA LA KATA KATIKA KIPINDI CHA ROBO YA KWANZA KUANZIA JULAI – SEPTEMBA, 2018 .**

Baraza lilipokea mashauri 34 aina ya mashauri.

1. Ndoa mashauri - 2
2. Madai - 3
3. Usafi wa Mazingira - 7
4. Utoro wa Mashuleni - 17

- Changamoto inayoikabili Baraza ukosefu wa askari Mgambo wa Baraza la Kata

**TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI**

Katika mwaka wa fedha **2018 – 2019** Kata imekisia kukusanya na kupokea kiasi cha **Tsh 478,476,546.5** kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo

**MAPATO**

- Kwa kipindi cha mwezi Julai hadi Septemba **2018/2019** Kata imekusanya na kupokea kiasi Tsh **10,102,869.95** kutoka vyanzo mbalimbali vya mapato sawa na asilimia makadirio yake ya Tsh **478,476,546.5.**

**MATUMIZI**

- Kwa kipindi cha Julai hadi Septemba Kata imetumia kiasi cha fedha **9,773,864.95** katika kutekeleza shughuli za maendeleo kama ifuatavyo:-

**MCHANGANUO WA MAPATO NA MATUMIZI**

| NA | KATA | MTAA | AINA YA MRADI SHUGHULI | CHANZO CHA FEDHA | FEDHA | | | HATUA YA UTEKELEZAJI | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | TOLEWA | TUMIKA | SALIO | | |
| **1.** | **KASHA ULILI** | **BUZOGWE** | Tozo ya taka Usafi wa mazingira | Wananchi | 1,409,000/= | 1,409,000/= | - | Zoezi la kusimamia uzoaji taka unaendelea | Tatizo ratiba ya gari haijakaa vizuri |
| | | **KASHA ULILI** | Tozo ya taka | Wananchi | - | - | - | Zoezi la usafi linaendelea | Tatizo ratiba ya gari haijakaa vizuri |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **KOTAZI** | Tozo ya taka | Wananchi | 1,633,500/= | 1,554,500/= | 79,000/= | Zoezi la usafi linaendelea | Tatizo ratiba ya gari haijakaa vizuri |
| | | **KASHAULILI** | Faini za Baraza la Kata | Faini | 200,000/= | 200,000/= | - | Asilimia 50 imepelekwa shuleni na asilimia 50 Baraza la Kata | Baraza linaendelea kusimamia sheria |
| | | **KASHAULILI** | Faini za uchavu wa mazingira | Faini | 250,000/= | - | 250,000/= | Zoezi la usafi linaendelea | Tunaendelea kuchukua hatua kwa wale wanaokaidi |
| | | **KASHAULILI MWANGAZA UHURU** | Fedha kwa ajili ya uendeshaji wa shule | Capitation | 6,610,369.95/= | 6,610,369.95/= | - | Fedha zote zinatumika kwa maelekezo ya Idara ya Elimu | Kuna fedha za majukumu na fedha za wanafunzi. |
| **JUMLA KUU** | | | | | **10,102,869.95/=** | **9,773,864.95** | **329,000/=** | | |

Mheshimiwa Mwenyekiti
Naomba kuwasilisha

John Matongo
**Diwani Kata ya Kashaulili**

**KATA YA KAKESE**

1. **UTANGULIZI.**

Kata ya Kakese ni kati ya Kata 15 zinazounda Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda, Tarafa ya Misunkumilo Wilaya ya Mpanda, Mkoa wa Katavi.

Kata ina jumla ya Vijiji vinne (4).

- ❖ Kijiji cha Mbugani
- ❖ Kijiji cha Kakese
- ❖ Kijiji cha Kawanzige
- ❖ Kijiji cha Kamakuka.

Pia Kata ina Vitongoji 18; ambavyo ni :-

- **Kijiji cha Mbugani**
    - Kitongoji cha Mbugani "A" Mashariki
    - Kitongoji cha Mbugani "B" Mashariki
    - Kitongoji cha Mbugani "B" Magharibi
    - Kitongoji cha Maluja
    - Kitongoji cha Mwangoye

- **Kijiji cha Kakese**
    - Kitongoji cha Mkwajuni
    - Kitongoji cha Makanisani
    - Kitongoji cha Kalofesi "A"
    - Kitongoji cha Kakese "B"

- **Kijiji cha Kawanzige**
    - Kitongoji cha Kawanzige "A"
    - Kitongoji cha Bulima
    - Kitongoji cha Mabanini
    - Kitongoji cha Jitegemee
    - Kitongoji cha Mwembeni

- **Kijiji cha Kamakuka**.
    - Kitongoji cha Kamakuka "A"
    - Kitongoji cha Kamakuka "B"
    - Kitongoji cha Ipwaga
    - Kitongoji cha Isengule

2. **WATU NA MAKAZI**

Kata ya Kakese inajumla ya Kaya **2577** na wakazi wapatao 14083, Ke **7087** Me 6988. Takwimu hii ni ya Sensa ya watu na makazi ya **2012.**

## 3. UONGOZI NA UTAWALA/ SIASA.

Kata ya Kakese ina Viongozi wa kuchaguliwa kama ifuatavyo:-

1. Mh. Diwani wa Kata- mmoja (1)
2. Wenyeviti wa Vijiji –Wanne (4)
3. Wenyeviti wa Vitongoji –(18) kumi na nane
4. Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji kwa Kata nzima 78 kwa Vijiji vinne.

Viongozi hawa ni wakuchaguliwa kutoka chama cha mapinduzi na chama cha CHADEMA.

## 4. WATAALAMAU.

Kata ya Kakese kwa sasa ina wataalamu wafuatao wanaotekeleza majukumu yao ya Serikali katika Vitongoji, Kijiji na Kata. Kama ifuatavyo:-

| Na | CHEO/NAFASI | No | NGAZI | IDARA | ENEO |
|---|---|---|---|---|---|
| | MTENDAJI KATA | 1 | KATA | UTAWALA | KAKESE |
| | AFISA AFYA | 1 | KATA | AFYA | |
| | AFISA MAENDELEO YA JAMII | 1 | KATA | MAENDELEO YA JAMII | |
| | AFISA UMWAGILIAJI | 1 | KATA | UMWAGILIAJI | |
| | AFISA KILIMO | 1 | KATA | KILIMO | |
| | AFISA MIFUGO | 1 | KATA | MIRUGO | |
| | AFISA ZANA ZA KILIMO | 1 | KATA | KILIMO | |
| | MRATIBU ELIMU KATA | 1 | KATA | ELIMU | |
| | ASKARI POLISI KATA | 1 | KATA | ULINZI NA USALAMA | |
| | WATENDAJI WA KIJIJI | 3 | KIJIJI | UTAWALA | |
| | WALIMU S/MSINGI | 68 | KIJIJI | ELIMU | |
| | WAUGUZI WA ZAHANATI | 4 | KIJIJI | AFYA | |
| | AFISA KILIMO KIJIJI | 1 | KIJIJI | KILIMO | |

## 5. VIKAO NA MIKUTANO

Ili kutekeleza shughuli za Serikali kwa kipindi cha robo ya kwanza 2018/2019 Kata imeketi vikao na mikutano ifuatayo:-

| No | VIKAO VYA KATA | KIKAO CHA KAWAIDA | KIKAO CHA DHARULA | TAREHE YA KIKAO |
|---|---|---|---|---|
| 1 | KAMATI YA VVU | 1 | 1 | 21/09/2018 |
| 2 | KAMATI YA ULINZI NA USALAMA | 1 | - | 04/10/2018 |
| 3 | KAMATI YA MALALAMIKO | 1 | 2 | 29/09/2018 |
| 4 | KAMATI YA UJENZI | 3 | 3 | 27/09/2018 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | /MAZINGIRA | | | |
| 5 | KIKAO CHA MAENDELEO YA KATA | 1 | | 05/10/2018 |
| 6 | MIKUTANO YA HADHARA | 1 | 4 | 11/10/2018 |

6. **UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA MAENDELEO.**

Kwa kipindi cha miezi mitatu ya robo ya kwanza ya **2018/2019** shughuli mbalimbali zimetekelezwa kama ifuatavyo:-

MAJI:- Kwa kipindi cha robo ya kwanza **2018/2019** huduma ya maji safi na salama imekuwa ya wastani kwa ngazi ya kaya na makazi.
Kwa kipindi hiki Jumla ya Visima vinne (4) vimechimbwa (visima virefu) hata hivyo hatua ya kufunga Pampu bado haijatekelezwa hivyo tunaomba kazi hiyo ikamilike kwa wakati ili waweze kutumika.

Nje ya Visima hivyo huduma ya maji inaendelea kutolewa kwa maeneo husika kupitia visima vilivyopo vipatavyo 12 na ambavyo vipo chini ya Jumuiya ya watumia maji ya kwa kila kijiji.

7. **ARDHI, MAZINGIRA NA NYUMBA**.

Katika kuboresha na kutekeleza shughuli za jamii, kwa robo ya kwanza 2018/2019 yafuatayo yametekelezwa.

a) Kuhamasisha jamii katika Vikao na mikutano kuendelea kuhifadhi mazingira, vyanzo vya maji, misitu, milima na mito iliyopo katika makazi ya Vijiji na Kata.
b) Kutunza shamba la miti iliyopandwa kupitia mradi wa **TASAF**
c) Kuhimiza ujenzi wa nyumba bora na hasa wakati huu ambao umeme umeanza kufika vijijini.
d) Kuratibu na kuhamasisha jamii kuepuka migogoro ya ardhi, mipaka na mashamba kwa kuwasilisha kero na malalamiko katika Kamati husika na mikutano.
e) Kuhamasisha jamii na Vijiji kupima maeneo yao ya makazi kupitia mpima binafsi ili kupunguza ujenzi holela katika makazi.

8. **UJENZI, MAWASILIANO NA UCHUKUZI.**

Kwa robo ya kwanza ya **2018/2019** kazi zilizotekelezwa ni:-

a) Kuhamasisha na kuelimisha wananchi kushiriki kutunza na kulinda miundombinu ya barabara, maji, mawasiliano na mifereji ya maji na njia za mifugo kutengwa na kuboreshwa.
b) Eneo la Kata ya Kakese bado lina changamoto kubwa ya kuchakaa na kuharibika kwa barabara zote za ndani ya Kata na Vijiji. Hivyo hatua zaidi zinahitajika ili kuondoa changamoto hii ya usafiri.

c) Eneo la Kata ya Kakese lina uhitaji mkubwa wa kuunganishwa kwa barabara za kuunganisha Kata hii na Kata jirani, Mfano. Kata ya Itenka, Mwamkulu, Kabungu ili kuinua uchumi wa Kata na Halmashauri.
d) Kupokea wataalamu wanaohakiki na kupima njia ya Reli kwa kuweka Bicon njia ya Karema-Mpanda.

9. **KAZI/AJIRA/ VIJANA NA WALEMAVU**.

Kwa robo ya kwanza **2018/2019** Kata Vijiji tu maendeleo kuratibu shughuli za Viwanda biashara na masoko kwa yafuatayo:-

- Kendelea kuhamasisha wafanyabiashara wenye mitaji kuwekeza katika maeneo yetu hasa kwenye biashara ya mazao, mifugo, misitu na ujasiliamali kwa wananchi wenye kipato cha chini na cha kati.
  Uwekezaji huu utasaidia uwepo wa ajira kwa vijana, wanawake, walemavu na makundi mengineyo.
  Hamasa ya uwekezaji huu inatokana na Fursa ya upatikanaji wa umeme katika eneo hili la Kata ambao ni kichocheo kikubwa cha maendeleo na uwekezaji.

10. **VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO.**

Kwa robo ya kwanza ya 2018/2019 kwa ngazi ya Kata na Vijiji tumeendelea kuratibu yafuatayo:-

- Kuratibu huduma ya Viwanda vidovidogo, masoko a maeneo ya uzalishaji mali, kwa kuwahakiki katika daftari la Kata la wafanyabiashara na Viwanda.
- Kukagua mashine za kusaga na kukoboa mpunga kwa kuhakiki usalama wa vifaa na vipuri kama vile:-

a) Mizani
b) Mitungi ya kuzimia moto
c) First Aid kit
d) Belts protractor
e) Usafi

Jumla ya Mashine 6 za kusaga na Mashine 8 za kukoboa mpunga zimekaguliwa.

- Kuboresha eneo la soko la kijiji cha Mbugani ili kuondoa mapagala yanayozunguka soko na kuboresha soko.

11. **ELIMU NA UFUNDI**

Katika sekta hii kazi zifuatazo zimetekelezwa

- Kuratibu na kusimamia shughuli za ufundishaji malezi kwa wanafunzi na kuzuia utoro sugu na utoro wa reja reja kwa shule zote za Msingi kwa kutumia kamati za shule, Ofisi za Vijiji na Kata.
- Kusimamia ujenzi wa vyumba vya madarasa mawili shule chipukizi ya Mbugani "A" Mashariki na kwa sasa Jengo limekamilika hatua ya Lenta.
- Kusimamia shule ya msingi Mbugani tofali zimekamilika tayari kwa kuanza ujenzi.
- Kusimamia ujenzi wa madarasa mawili shule ya Sekondari Kakese. Jengo limekamilika hatua ya Lenta. Ujenzi huu ulianza tarehe 01/06/2018 na kukamilika hatua ya Lenta **11/10/2018.**
- Kuanzisha ujenzi wa madarasa mapya mawili kwa kuanza kukusanya vifaa mawe na tofali.

**NB:-** Tunachukua nafasi hii kumshukuru Naibu waziri wa Afya **Mhe: F.Ndungulile (mb)** kwa ziara yake ya tarehe **24/01/2018** aliyotembelea mradi wa Sekondari Kakese na kushiriki na wananchi katika ufyatuaji wa matofali kwa kuchangia mifuko 43 ambayo imesaidia kufanikisha kukamilisha boma la vyumba viwili pamoja na tofali za wananchi.

## 12. AFYA NA MAZINGIRA.

Kwa kipindi cha Julai hadi Septemba **2018/2019** yafuatayo yametekelezwa:-

- Kwa kipindi hiki Kata na Vijiji tumeendelea kushiriki kuhamasisha jamii kutunza mazingira, kufanya usafi ngazi ya kaya, maeneo ya biashara, maeneo ya wazi na katika Taasisi kwa kila jumamosi ya mwisho wa mwezi na siku za katikati ya wiki.
- Serikali imeendelea kutoa chanjo ya watoto chini ya miaka 5, kutoa huduma ya kinga na tiba.
- Serikali imeendelea kusimamia na kuratibu maambukizi ya **VVU** kwa kutoa huduma ya dawa za **ARV** katika kituo cha Zahanati ya Kakese Mbugani na kutoa Elimu ya kuzuia maambukizi mapya ya **VVU**.
- Kufanya ukaguzi wa mazingira na Vyoo kwa kila kaya na vyumba vya biashara.

**TAKWIMU YA UKAGUZI.**

| NYUMBA ZA KULALA WAGENI | BAA | BUCHA | VIJIWE VYA KAHAWA | SALUNI ZA KIUME | SALUNI ZA KIKE |
|---|---|---|---|---|---|
| 8 | 10 | 4 | 4 | 17 | 3 |

**VYOO VILIVYOKAGULIWA KATIKA KAYA**

| AINA YA CHOO | A | B | C | D | X | VIBUYU CHIRIZI | VICHANJA | KARO | MASHIMO YA TAKA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| IDADI KAGULIWA | 364 | 783 | 850 | 281 | 60 | 1042 | 1787 | 1560 | 1578 |

Hivyo jumla ya kaya 2293 zimetembelewa na kukaguliwa kati ya kaya 2577 katika Kata.

13. **MIFUGO NA UVUVI.**

Kwa robo ya kwanza 2018/2019 katika Idara hii. Kazi zifuatazo zimetekelezwa:-

- Kuchimbwa bwawa la samaki katika eneo la Kijiji cha Kamakuka kupitia mradi wa TASAF. Kazi imekamilika na sasa hatua iliyobaki ni kupandikiza samaki change.
- Kukamilisha wigo wa bwawa la samaki kijiji cha Kawanzige kazi imekamilika na sasa hatua ya kupandikiza samaki itafanyika wakati wowote.
- Kuratibu na kusimamia chanjo ya ng'ombe homa ya mapafu. Jumla ya ng'ombe waliochanjwa ni 1452 na kuku 542 chanjo ya kideli.
- Kuratibu utaratibu shuguli za mnada na machinjo ya ng'ombe, Nguruwe na Mbuzi. Jumla ya Ngombe 50, Mbuzi 37, nguruwe 15 kwa robo hii.

14. **KILIMO UMWAGILIAJI NA USHIRIKA.**

Kazi zilizotekelezwa.

a) Kutoa Elimu kwa wakulima juu ya uhifadhi bora wa mazao kwa Vijiji vyote vinne.

**b)** Kuandaa wakulima walioenda kushiriki mafunzo/ sherehe za nane nane Mbeya, ambaye ni mkulima wa zao la mpunga ndugu **SAIDA SUNZULA.**

- Kuandaa wakulima watakaolima zao la pamba na korosho kwa Vijiji vya Kata ya Kakese Jumla ya wakulima 21 wameandikishwa na sawa na Ekari 50 kwa zao la pamba na wakulima 3 wa zao la korosho sawa na Ekari 6
- Kwa robo hii ya kwanza ya 2018/2019 tumekuwa na utaratibu wa vikundi mbalimbali ndani ya Kata ili kuunda **AMCOS** na kupata kikundi chenye ushirika kwa Kata ya Kakese. Zoezi la kuunganisha vikundi linaendelea kwa vikundi 24 vilivyopo, kupata Elimu na maelekezo toka Idara ya ushirika Manispaa ya Mpanda na shirika lisilo la Kiserikali la **AGRA** toka Mkoani Iringa
- Kutoa Elimu ya kuandaa mbegu za mpunga na kuandaa mashamba mapema kwa wakulima
- Kuratibu maandalizi ya umaliziaji wa Mabanio ya umwagiliaji ambayo hayakukamilika ikiwa ni pamoja na kusimamia malipo ya wazabuni.

15. **ULINZI NA USALAMA**

- Kwa kipindi cha robo ya kwanza kamati ya ulinzi na usalama imekaa vikao vitatu sawa na kikao kimoja kila mwezi
- Kwa kipindi hicho tumepata matukio 7, uhalifu mdogo (wizi) matukio 4 na shambulio la mwili matatu. Matukio yote yalishughulikiwa na kuitimishwa.
- Hali ya ulinzi na usalama ni nzuri na inazidi kuimalika zaidi kufuatia uwepo wa kitengo cha polisi ndani ya Kata.

NB:- Tunaomba kusaidiwa kupata Mbao 370 kwa ajili ya kupauwa Jengo la kituo cha polisi kilichojengwa na wananchi na kufanga Lenta.

16. **KERO, MIGOGORO NA MALALAMIKO.**

Jumla ya migogoro mitatu (3) imepokelewa na kushughulikiwa kwa wakati. Migogoro miwili imemalizika na mgogo mmoja unaendelea kushughulikiwa na Ofisi ya Kata. Ili kudumisha Mahusiano mema ya Jamii, watumishi na Viongozi wa Serikali tumeendelea kufanya mikutano na Vikao ngazi ya Kata, Vijiji na Vitongoji na kupokea kero, na malalamiko mbalimbali na kuyashughulikia kwa wakati. Jumla ya kero 4. Zimepokelewa na kutatuliwa na ngazi husika ya Kata na Vijiji.

17. **MAPATO NA MATUMIZI.**

Taarifa ya mapato na matumizi kwa kipindi cha July hadi September 2018/2019 kwa Kata ya Kakese tarehe **05/10/2018.**

Kwa kipindi cha July hadi September 2018/2019 Kata ilikisia kupokea na kukusanya kiasi cha **Tshs.56,288.6** kwa ajili ya kutekeleza shughuli za maendeleo ya Kata na Vijiji vyake vinne (4) na Vitongoji 18.

Kwa kipindi cha robo ya kwanza **2018/2019** Kata imepokea kiasi cha **Tshs. 7,204,510.68** toka Halmashauri kwa ajili ya miradi ya shule na malipo yao **TASAFTshs. 16,424,000/=** kwa kaya masikini na **Tshs. 5,518,835/=** michango ya maendeleo.

**MATUMIZI.**

Kwa kipindi cha robo ya kwanza 2018/2019 Kata imetumia kiasi cha Tshs.29,147,345.68 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi, uendeshaji wa S/Msingi na malipo ya **TASAF.**

Naambatanisha na mchanganuo wa mapato na matumizi taja hapo juu.

Naomba kuwasilisha

**..............................**

**MAGANGA SALAGANDA**

**DIWANI KATA YA KAKESE**

**KATA KAWAJENSE**

**TAARIFA YA UTEKELEZAJI SHUGHULI ZA MAENDELEO KWA MWAKA 2018/2019 KWA KATA YA KAWAJENSE KWA KIPINDI CHA JULY-SEPTEMBA 2018**

A: UTANGULIZI:

Kata ya Kawajense ni miongoni mwa kata 15 zinazounda manispaa ya Mpanda ambayo ipo Tarafa ya Kashaulili.

B: MIPAKA YA KATA.

- Upande wa Mashariki inapakana na kata ya Kazima na Nsemulwa,
- Upande wa Kaskazini inapakana na kata ya Shanwe na Kazima,
- Upande wa Magharibi inapakana na kata ya Makanyagio,
- Upande wa Kusini inapakana na kata ya Kashaulili na Nsemulwa.

C: MAENEO YA KIUTAWALA

Kata ya Kawajense ina jumla ya mitaa mitatu(3) ambayo ni:- Mtaa wa Kawajense, mtaa wa Majengo Mapya na Mtaa wa Ikulu.

D: UONGOZI ULIOPO KATIKA KATA

i. Diwani wa Kata
ii. Diwani viti maalumu
iii. Afisa mtendaji Kata
iv. Wenyeviti watatu wa mitaa
v. Wataalamu ngazi ya kata
vi. Watendaji watatu wa mitaa.

E: IDADI YA VIKAO VYA KISHERIA.

| VIKAO VYA WDC | | | VIKAO VYA MITAA | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| VIKAO HITAJIKA KWA MWAKA | VIKAO VILIVYO FANYIKA | VIKAO MAALUMU | JINA LA MTAA | VIKAO HITAJIKA KWA MWAKA | VILIVYO FANYIKA | MIKUTANO HITAJIKA | ILIYO FANYIKA |
| 4 | 4 | 3 | KAWAJENSE | 12 | 10 | 4 | 3 |
| | | | MAJENGO MAPYA | 12 | 10 | 4 | 3 |
| | | | IKULU | 12 | 10 | 4 | 2 |

F: IDADI YA KAYA NA WAKAZI WA KATA YA KAWAJENSE.

| JINA LA KATA | JINA LA MTAA | IDADI YA KAYA | IDADI YA KAYA | | | WENYE UWEZO WA KUFANYA KAZI | | | WASIO NA UWEZO WA KUFANYA KAZI | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML |
| | KAWAJENSE | 812 | 1632 | 1694 | 3326 | 418 | 436 | 2254 | 532 | 572 | 1164 |
| | MAJENGO MAPYA | 703 | 812 | 1720 | 2532 | 1147 | 1160 | 2307 | 545 | 585 | 1125 |
| | IKULU | 691 | 1686 | 1715 | 3401 | 1137 | 1157 | 2294 | 554 | 563 | 1117 |
| | JUMLA | 2206 | 5038 | 5147 | 10147 | 3402 | 3453 | 6855 | 6131 | 1715 | 3346 |

**SHUGHULI ZA KIUCHUMI**

Wananchi wa kata ya Kawajense wanajishughulisha na kazi zifuatazo:-

i. Kilimo na ufugaji mifugo,
ii. Wafanyakazi na watumishi wa mashirika,
iii. Wachimbaji wadogo wa madini mbali mbali,
iv. Wafanyabiashara wakubwa na wadogo,
v. Mafundi wa fani mbali mbali.

E: HALI YA UONGOZI

Katika kata ya Kawajense kuna ushirikiano mzuri kati ya viongozi wa serikari, vyama vya siasa na madhehebu ya dini kwa kushirikiana katika vikao vya ndani (WDC) na mikutano ya hadhara katika kuhamasisha wananchi kwa miradi ya maendeleo.

F: IDADI YA WATUMISHI KILA IDARA

| IKAMA | UTAWALA | KILIMO | AFISA AFYA | MAENDELEO | ELIMU MSINGI |
|---|---|---|---|---|---|
| MAHITAJI | 4 | 2 | 2 | 1 | 133 |
| WALIOPO | 3 | 1 | 1 | 1 | 76 |
| PUNGUFU | 1 | 1 | 1 | 0 | 57 |

TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA KIPINDI CHA JULAI-SEPTEMBEA 2018-2019 KATA YA KAWAJENSE

A. MAPATO

| S/N | JINA LA MRADI | CHANZO CHA FEDHA | MAPATO | JUMLA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | SALIO ANZIA | HALMASHAURI/WANANCHI | 1,152,585.27 | 1,152,585.27 |
| | JUMLA KUU | | 1,152,585.27 | 1,152,585.27 |

B. MATUMIZI

| S/N | JINA LA MRADI | CHANZO CHA FEDHA | FEDHA TENGWA | FEDHA TOLEWA | FEDHA TUMIKA | BAKI | MAELEKEZO |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | SALIO ANZIA | HALMASHAURI/ WANANCHI | 1,152,585.27 | 1,152,585.27 | 300,000 | 852,585.27 | Ilitumika kuandaa mapokezi ya mbunge |
| JUMLA KUU | | | 1,152,585.27 | 1,152,585.27 | 300,000 | 852,585 | |

**SEKTA YA AFYA KINGA**

Kata ya Kawajense inasimamia shughuli zifuatazo:-

i. Kusimamia usafi wa mazingira na uzoaji taka.
ii. Kuwahamasisha wananchi kutumia vyandarua vyenye viatilifu.
iii. Kutoa elimu juu ya kujikinga na VVU/Ukimwi.
iv. Kuwashauri wananchi kupima afya zao kuhusiana na VVU/Ukimwi.
v. Katika kusimamia usafi wa mazingira ratiba ya usafi imepangwa kila siku ya Jumatano kuwa siku ya usafi katika Kata.

RATIBA YA UKAGUZI WA USAFI KILA JUMATANO YA WIKI

| S/N | JINA LA MTAA NA ENEO LA KAZI | WASIMAMIZI | MFUATILIAJI |
|---|---|---|---|
| 01. | Mtaa wa Majengo mapya kuanzia barabara iendayo Ugalla mpaka njia mbili unashuka hadi barabara ya sokoni Majengo mapya hadi barabara ya Mikocheni. | Brayson Mwalugala<br>Mwl. Mkuu Nyerere<br>Patrick Mtandula | Prisca Chokola |
| 02. | Eneo kuanzia barabara ya kanisa la New Harvest (Kwa Labani) kushuka kwa baba John hadi makaburini. | Antonia Kakokere<br>Wilbroad Milambo<br>Lauliana Benard<br>Kaim mtendaji mtaa. | Asnati Dibwis |
| 03. | Mtaa wa Kawajense kuanzia Mikocheni kushuka hadi barabara ya Mkombe hadi Tanesco kwa Mayeye hadi Msakila kotazi hadi Kompoundi kwa Mkurugenzi na shule ya msingi Msakila. | William Jumapili<br>Edmund Mbunda<br>Mwl. Mkuu Msakila<br>Mary Kabeje | Mwl Joseph Sangana |
| 04. | Kutoka barabara ya Mkombe hadi kwa Mzee Mzimya kupitia kwa DSO hadi nyumbani kwa Mkuu wa Wilaya unarudi hadi Msikitini hadi kwa Betabula unapandisha hadi maeneo ya Endita “B” hadi kwa Mwanalinze | Gervas Telengula<br>Albert Kamsini<br>Anna Sundu<br>Elizabeth J. Mpigauzi | Agnes Urasa |
| 05. | Mtaa wa Ikulu<br>Eneo kuanzia Ikulu hadi barabara ya kutoka Hospitali kwa Dalla hadi Msikiti wa Madukani unashuka hadi darajani kwa Itala hadi soko la | Clement Mbamba<br>Uwezo Bacho<br>Peter Robert<br>Rehema Masoud | Gilbert Nyenyeri |

| 06. | matunda unarudi kwa Zahoro na Misasi gereji na eneo lote la soko la matunda<br><br>Mtaa wa Ikulu.<br>Kuanzia kwa marehemu Zacharia hadi kwa Kalubu unatokea kwa Betabula hadi soko la matunda hadi kisima cha maji kwa Simbao unarudi hadi Ikulu ndogo na PUB | Steven Temezya<br>Mary Kalubu<br>Onesmo Kemanzi | Pascal Peleka |
|---|---|---|---|

(A) HALI YA USAFI

Hali ya usafi inaridhisha, ratiba iliyotolewa na Halmashauri ya manispaa kwamba kila ijumaa gari ya usafi litafika kuzoa taka lakini ratiba haizingatiwi kwa wakati husika.

(B) CHANGAMOTO

i. Maeneo yasiyoendelezwa kama vile mapagala na viwanja visivyo endelezwa yanatunza uchafu na watu kutupia taka nyakati za usiku kwa kukwepa kulipa pesa ya ushuru wa taka Tshs. 2000/= kila mwezi ya umwagaji taka.
ii. Dereva anapokuja kwenye uzoaji taka anazima gari na kusema mafuta yameisha mpaka tuongeze mafuta hivyo unakuta mara nyingi inachelewesha kuisha kwa takataka.
iii. Wananchi wengi hawachangii hela ya ushuru wa taka na wenye nyumba za kupangisha wanaficha wapangaji wao na kusema kuwa ni familia moja.
iv. Eneo la kata ya Kawajense ni kubwa sana kwa kupangiwa gari ya taka siku moja inashindikana kumaliza uzoaji taka.

ELIMU NA MAFUNZO

1.1 HABARI ZA WANAFUNZI

| SHULE | JINSIA | AWALI | MADARASA | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | I | II | III | IV | V | VI | VII | JUMLA |
| NYERERE | WV | 191 | 238 | 237 | 284 | 151 | 124 | 142 | 97 | 1469 |
| | WS | 181 | 292 | 235 | 264 | 177 | 136 | 150 | 113 | 1553 |
| | JML | 372 | 530 | 472 | 548 | 328 | 260 | 292 | 210 | 3022 |
| MSAKILA | WV | 83 | 133 | 136 | 147 | 108 | 54 | 53 | 76 | 790 |
| | WS | 70 | 134 | 132 | 150 | 112 | 57 | 63 | 72 | 810 |
| | JML | 153 | 267 | 268 | 297 | 320 | 131 | 116 | 148 | 1600 |
| MIZENGO PINDA | WV | 120 | 144 | 89 | 58 | 50 | 53 | 47 | 54 | 615 |
| | WS | 112 | 99 | 80 | 53 | 40 | 57 | 52 | 48 | 541 |
| | JML | 232 | 213 | 169 | 111 | 90 | 110 | 99 | 102 | 1156 |
| JUMLA YA KATA | WV | 394 | 515 | 462 | 489 | 309 | 231 | 242 | 187 | 2874 |
| | WS | 363 | 525 | 447 | 467 | 329 | 250 | 265 | 233 | 2904 |
| | JML | 757 | 1040 | 909 | 956 | 638 | 481 | 507 | 420 | 5778 |

## 1.2 HABARI ZA WALIMU

| SHULE | MAHITAJI | | | WALIOPO | | | PUNGUFU | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML |
| NYERE | 30 | 38 | 68 | 11 | 24 | 35 | 19 | 14 | 33 |
| MSAKILA | 15 | 25 | 40 | 7 | 16 | 23 | 9 | 8 | 17 |
| MIZENGO PINDA | 8 | 17 | 25 | 6 | 12 | 18 | 2 | 6 | 8 |
| JUMLA YA KATA | 53 | 80 | 133 | 24 | 52 | 76 | 30 | 28 | 58 |

## 1.3 MAJENGO

| SHULE | MADARASA | | | VYUMBA VYA WALIMU | | | STOO | | | VYOO | | | OFISI | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | MAH | VIL | PUN | MAH | VIL | PUN | MAH | VIL | PUN | MAH | VIL | PUNG | MAH | VIL | PUN |
| NYERERE | 68 | 11 | 57 | 68 | | 68 | 3 | 2 | 1 | WV 62<br>WS 73 | WV 7<br>WS 6 | WV 55<br>WS 67 | 5 | 2 | 3 |
| MSAKILA | 40 | 6 | 34 | 40 | | 40 | 2 | 1 | 1 | WV 32<br>WS 40 | WV 11<br>WS 10 | WV 21<br>WS 30 | 5 | 2 | 2 |
| MIZENGO PINDA | 25 | 6 | 19 | 25 | | 25 | 2 | | 2 | WV 29<br>WS 21 | WV 6<br>WS 5 | WV 13<br>WS 16 | 3 | 1 | 2 |
| JML KATA | 133 | 23 | 110 | 133 | | 133 | 7 | 3 | 4 | WV 123<br>WS 134 | WV 24<br>WS 21 | WV 89<br>WS 113 | 12 | 5 | 7 |

## 1.4 SAMANI

| SHULE | MADAWATI | | | VITI | | | MEZA | | | SHUBAKA | | | KASIKI | | | KABATI | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | MAH | YAL | PUN | MAH | YAL | PUN | MAH | YAL | PUN | MAH | YAL | PUN | MAH | YAL | PUN | MAH | YAL | PUN |
| NYERERE | 1007 | 423 | 584 | 42 | 24 | 18 | 42 | 15 | 27 | 2 | 2 | | 1 | | 1 | 11 | 3 | 8 |
| MSAKILA | 533 | 235 | 298 | 33 | 15 | 8 | 25 | 10 | 15 | 3 | | 3 | 1 | | 1 | 11 | 2 | 9 |
| MIZENGO PINDA | 385 | 272 | 113 | 31 | 13 | 30 | 30 | 9 | 21 | 2 | 1 | 1 | 1 | | 1 | 8 | 2 | 6 |
| JML KATA | 1925 | 930 | 995 | 106 | 52 | 54 | 97 | 34 | 63 | 7 | 3 | 4 | 3 | | 3 | 30 | 7 | 23 |

HABARI ZA MIRADI SHULE ZA MSINGI

| SHULE | AINA YA MRADI | KUANZA KUJENGWA | HATUA ILIYOFIKIWA | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|
| NYERERE | -Ujenzi wa vyumba vitatu vya madarasa<br>-Ufyatuaji tofali za block | Bado ujenzi haujaanza | Zimefyatuliwa tofali 2000 | Bado tunaendelea na ufyatuaji wa tofali za block |
| MSAKILA | Ujenzi wa vyumba vitatu vya madarasa | Bado ujenzi haujaanza | Trip tatu za mawe zimekusanywa | Fedha inahitajika kukamilisha ukusanyaji wa mawe |
| MIZENGO PINDA | Ujenzi wa vyumba 3 vya madarasa na ofisi ya M/mkuu | Juni 2018 | Ukusanyaji wa mawe Tripu 9 na michango inaendelea<br>-Mchanga tripu tano | Ujenzi wa msingi umeanza hatua iliyofikia wametandaza mawe ¾ ya eneo lote la msingi |

TAARIFA YA ROBO YA KWANZA (1) KILIMO JULAI - SEPTEMBER 2018-2019

Malengo ya kilimo 2018-2019 tunatarajia kuwa na mazao mbalimbali kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali

| S/N | MAZAO | Hekta zitakazolimwa | Matarajio ya mavuno (Tani) |
|---|---|---|---|
| 1. | Mahindi | 6 | 15 |
| 2. | Mpunga | 0.8 | 2.5 |
| 3. | Viazi vitamu | 2.8 | 10 |
| 4. | Karanga | 4.8 | 7.2 |
| 5. | Maharage | 4 | 6 |
| 6. | Miwa | 0.8 | 1.2 |
| | JUMLA | 19.2 | 42.2 |

MBOGAMBOGA

| AINA YA MAZAO | Hekta zitakazolimwa | Mavuno (Tani) |
|---|---|---|
| Matango | 0-4 | 4 |
| Mchicha | 4 | 3.2 |
| Chinese Cabbage | 2.8 | 3.36 |
| Nyanya | 6 | 12 |
| Vitunguu | 20 | 40 |
| Bamia | 1.2 | 24 |
| JUMLA | 34.4 | 86.56 |

Jumla ya eneo lililolimwa msimu wa kilimo 2017/2018 kata ya Kawajense Hekta 65.25;

- Hali ya chakula ni nzuri mazao yanapatikana pia bei ya chakula ni nzuri mfano mahindi yanapatikana kwa Tsh. 350 1=kg

MIFUGO

| MFUGO | Ng'ombe wa kisasa | Ng'ombe wa kienyeji | Mbuzi | Kondoo | Nguruwe | Kuku | Bata | Njiwa | Mbwa |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| IDADI | 54 | 31 | 393 | 15 | 307 | 2781 | 904 | 189 | 154 |

SEKTA YA MAENDELEO YA JAMII

TAARIFA ZA MAKUNDI MAALUM KATA YA KAWAJENSE

| MTAA | WALEMAVU | | | WAZEE | | | WATOTO WAISHIO MAZINGIRA HATARISHI | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML |
| KAWAJENSE | 5 | 13 | 18 | 51 | 88 | 139 | 50 | 77 | 127 |
| IKULU | 15 | 22 | 37 | 42 | 76 | 118 | 44 | 59 | 103 |
| MAJENGO MAPYA | 6 | 1 | 7 | 51 | 54 | 105 | 7 | 8 | 15 |
| JUMLA | 26 | 36 | 52 | 144 | 222 | 362 | 101 | 144 | 245 |

Asasi zinazotoa huduma mbalimbali katika kata ya Kawajense zipo tano

| | JINA LA ASASI | SHUGHULI |
|---|---|---|
| 1 | PAMOJA TUWALEE | Inajishughulisha na uundaji wa vikundi kwa ulezi wa watoto waishio mazingira hatarishi ili kuweza kujisaidia kiuchumi |
| 2 | SHIDEPHA | Kutoa huduma kwa waathirika wa VVU na UKIMWI |
| 3 | WEVA (WOMEN EQUITABLE NA VOLUNTARY ACTION) | Kuhamasisha vijana na wanawake jinsi ya kutumia rasilimali walizonazo ili kuondokana na umasikini |
| 4 | KAODEO | Kuhamasisha jamii kutambua rasilimali walizonazo na vikwazo kuwa fursa katika kujiletea maendeleo |
| 5 | KIZAZI KIPYA (ANGLICAN) | Kutoa huduma kwa waathirika na waathiriwa wa VVU na UKIMWI |

- Jumla ya vikundi katika kata 43
  - Vikundi vya wanawake -27
  - Vikundi vya vijana -8
  - Vikundi mchnganyiko -8
- Vikundi vilivyopata mkopo jumla 12.
- Mkopo ngazi ya Halmashauri vikundi 9, wanawake 8 na vijana 1.

Mkopo ngazi ya kata vikundi 3 vya wanawake vilivyomaliza mkopo ni vitatu ambavyo ni Kwaito na Katwezye na Nakilima.

- Kati ya vikundi 12 vilivyopata mkopo vikundi 8 vimemaliza marerejesho vya wanawake na vikundi 4 bado vipo kwenye marejesho ambapo 1 cha vijana na wanawake 3.
- Day care katika kata zipo 5 ambapo 2 zimesajiliwa na 3 zipo kwenye mchakato wa usajili.

ULINZI NA USALAMA

Hali ya ulinzi na usalama ni ya kuridhisha kwani matukio ya wizi na uhalifu mwingine yamepungua. Na jamii inaendelea kuelimishwa juu ya kuanzisha vikundi vya ulinzi shirikishi ili kutokomeza kabisa wizi na uhalifu mwingine.

UKIMWI

Katika kata ya Kawajense wananchi wanaendelea kupatiwa elimu juu ya kujikinga na VVU na Ukimwi kupitia vikao na vikundi mbalimbali kama vile SHIDEPHA+ na mradi wa Anglican wa kizazi kipya wanaopita kwenye kaya mojamoja na kutoa elimu juu ya kujikinga na VVU na Ukimwi pamoja na kupima VVU/UKIMWI kwa hiyari.

Pia makundi haya yameteua watu maalumu wanaopita kwenye kaya mbalimbali na kutoa elimu na kupata taarifa za wanaoishi na VVU/UKIMWI na kuwaelimisha.

MAFANIKIO YA MAENDELEO KATIKA KATA YA KAWAJENSE

- Tumeweza kujenga madarasa matatu shule ya msingi Nyerere.
- Tumeweza kusomba mawe tripu tisa (9) shule ya msingi Mizengo Pinda.
- Tumeweza kujenga choo cha ofisi ya kata na kukikamilisha.

CHANGAMOTO

1. Upungufu wa vyumba vya madarasa mahitaji ni vyumba 133 yaliyopo 23 pungufu 110 kulingana na idadi ya wanafunzi 5778.
2. Upungufu wa vyoo vya walimu na wanafunzi mahitaji matundu 257 yaliyopo 45 pungufu 212 uwiano wa vyoo ni wasichana 1:20 wavulana 1:25.
3. Ukosefu wa nyumba za walimu kwa kata nzima ambapo mahitaji ni nyumba 133 hakuna hata moja.
4. Ukosefu wa vidhibiti mwendo katika barabara zinazozunguka shule za Msingi za Msakila, Mizengo Pinda na shule ya Msingi Nyerere hata kusababisha ajali za mara kwa mara kwa wanafunzi.
5. Mwitikio hasi wa wazazi kutochangia chakula cha mchana shuleni kwa ajili ya watoto wao.
6. Upungufu wa walimu, kata ina waalimu 76 na pungufu 58. Jumla ya wanafunzi ni 5778 hivyo kwa uwiano 1:40 tunahitaji walimu 133 waliopo ni 76 upungufu ni 58.
7. Mwitikio hasi wa wazazi/jamii katika kuchangia ujenzi wa miundo mbinu ya shule kwani pamoja na kutoa ufafanuzi kuhusu sera ya elimu bure bado kuna wazazi ambao bado wagumu kuelewa.
8. Utoro wa wanafunzi bado ni kikwazo katika kufanikisha malengo.
9. Mahitaji ya madawati kwa kata ni 1925 yaliyopo ni 930 pungufu 995 hii inasababishwa na upungufu wa madarasa.

MAONI/MAPENDEKEZO

1. Tunaomba kuongezewa walimu 57 kama inavyoelekeza kama kuna uwezekano kwa hili.
2. Tunaomba kwa mamlaka husika kuwekewa vidhibiti mwendo katika barabara zinazopita karibu na shule kupunguza ajali kwa wanafunzi.
3. Tunahitaji ujenzi wa nyumba za walimu 133 walau ujenzi wa nyumba nne kila mwaka
4. Tunaendelea kuhamasisha wazazi kuchangia chakula cha watoto wao shuleni ili kuinua kiwango cha elimu kwa watoto wao
5. Tunaendelea na mkakati wa kuhamasishana ili kila mwana-Kawajense aone umuhimu wa kuchangia na ashiriki kuchangia ujenzi wa madarasa ili watoto wote waweze kusoma inavyostahili.
6. Tunaendelea kutafuta mwarobaini kupitia WDC kukomesha utoro wa wanafunzi katika shule zetu zote za kata yetu.
7. Tutashughulikia suala la madawati tukimaliza ujenzi wa madarasa yaliyopungua
8. Tutashughulikia ujenzi wa vyoo kila nafasi itakaporuhusu na hasa tukimaliza ujenzi wa madarasa pamoja na nyumba za walimu

9. Kwa sababu kata ya Kawajense imeendelea kufanya vizuri kitaaluma katika wilaya ya Mpanda na mkoa wa Katavi kwa ujumla zaidi ya miaka minne mfululizo, tunaomba Halmashauri ya manispaa itupe tunu ya mchango katika baadhi ya changamoto tulizo nazo na hasa ujenzi wa madarasa na nyumba za walimu.

Mheshimiwa PIUS BUZUMALLE

DIWANI KATA KAWAJENSE

**KATA YA KAZIMA**

## TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA ROBO YA KWANZA YA MWAKAJULAI –SEPTEMBA 2018

### UTANGULIZI

Mh. Mstahiki Meya , kata ya Kazima ni miongoni mwa kata kumi na tano (15) zinazounda Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda Kata hii kiutawala inaundwa na mitaa mitatu (3) ambayo ni.

- Mtaa wa Kazima
- Mtaa wa Rungwa
- Mtaa wa Kapalangao

### 1.1 IDADI YA WATU NA MAKAZI.

Kata ya kazima inajumla ya wakazi wapatao **12,270**kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya zoezi kwa mchanganuo ufuatao.

| JINA LA KATA | MAJINA YA MITAA | ME | KE | JUMLA |
|---|---|---|---|---|
| KAZIMA | MTAA WA KAZIMA | 2262 | 2579 | 4841 |
| | MTAA WA KAPALANGAO | 1592 | 1939 | 3531 |
| | MTAA WA RUNGWA | 1896 | 2002 | 3898 |
| **JUMLA** | | **5750** | **6520** | **12270** |

Kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi **2012.** Kata hii ya Kazima inajumla ya kaya **2575**, Zenye wakazi **12270** ambapo kati yao wanaume **5750** na wanawake wapatao **6520**.

Katika mwaka wa fedha **2017/2018**. Kata ilikisia kukusanya na kutumia kiasi cha **Tshs 1,472,767,624** kwa ajili ya kutekeleza shughuli mbalimbali za maendeleo.

### 1.2. MAPATO.

Kwa kipindi cha mwezi **Julai** hadi **Septemba2018.** Kata imekusanya na kupokea kiasi cha **Tshs 8,983,211/=** kutoka vyanzo mbalimbali vya mapato ya ndani ya Halmashauri ambayo ni sawa na Asilimia ya makadilio ya **Tshs 8,500,000/=** kwa mwaka.

### 1.3. MATUMIZI.

Kwa kipindi cha mwezi **Julai** hadi **Septemba 2018**. Kata imetumia kiasi cha **Tshs.8,500,000/=** katika kutekeleza shughuli mbalimbali za maendeleo kwa mchanganuo ufuatao:-

### MCHANGANUO WA TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA KIPINDI CHA MWEZI JULAI HADI SEPTEMBA 2018

| NO. | JINA LA MRADI/SHUGHULI | CHANZO CHA FEDHA | FEDHA TOLEWA | FEDHA TUMIKA | FEDHA BAKI BENKI | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Ujenzi wa choo shule ya Msingi Mkapa | Mfuko wa jimbo | 1,000,000/= | 1,000,000 | | Ujenzi wa boma la choo matundu 16 umekamilika |
| 2 | Ujenzi wa vyumba vitatu (3) vya madarasa na Ofisi moja (1) | • Mfadhili SRSG MAGAMBA<br>• Maendeleo ya Kata<br>• Nguvu za | 6,000,000<br><br>1,483,216/= | 6,000,000/=<br><br>1,000,000/= | 483,216/= | Hatua ya ujenzi wa boma unaendelea |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | wananchi | 500,000/= | 500,000/= | 483,216/= | |
| | Jumla ndogo | | 7,983,216/= | 7,500,000/= | 483,211/= | |
| | **JUMLA KUU** | | **8,983,211/=** | **8,500,000/=** | **483,211/=** | |

## TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA IDARA YA MAENDELEO YA JAMII ROBO YA KWANZA JULAI HADI SEPTEMBA 2018

| NA | LENGO | SHUGHULI | UTEKELEZAJI | CHANGAMOTO /MAFANIKIO |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Utoaji wa huduma bora za kiuchumi kwa usawa | • Kutoa maelekezo ya jinsi ya kuandika barua ya maombi ya mkopo kwa vikundi<br>• Kutembelea vikundi na kukagua miradi yao | • Jumla ya vikundi **4** viliandika barua ya mkopo ambayo ni Magufuli na Maendeleo, warungwa, Faru group na Amkeni.<br>• Vikundi **4** vilitembelewa na kukaguliwa shughuli za miradi yao ambavyo ni Tumaini Agriculture na Faraja | • Vikundi hivi vinatarajia kupata mkopo tobo ya nne mwezi huu.<br>• Vikundi vingine vinafanya shughuli za kilimo mbali na nje ya Mji hivyo kuna umbali wa kufika kukagua shughuli hizo |
| | | Nimefanya ziara ya kutoa elimu ya vikundi kwa watoa huduma ngazi ya jamii ya shirika la ACT | Ziara hii ilifanyika katika Kata **15** za Manispaa kwa muda wa wiki moja. Taarifa imeambatanishwa na nipoti hii | Nilifanikiwa kutoa elimu hiyo iliyo kusudiwa na pia tuliweza kutatua changamoto mbalimbali |
| 2 | Kuimalisha huduma za utawala wa sheria na utawala bora | • Kuhamasisha wananchi kufuata sheria .<br>• Zoezi la uandikishaji wa vitambulisho vya utaifa | • Nimeelimisha viongozi mbalimbali wa Kata katika mikutano **2** ya ndani kuhusu matumizi ya sheria katika utatuzi migogoro ya kesi mbalimbali ili kuboresha utawala bora.<br>• Wananchi kwa asilimia kubwa wanauelewa juu ya utwala wa sheria kwa sababu hufika Ofisini kulipoti migogoro yao.<br>• Ambapo fomu zimeshagawiwa kwa wananchi wote wenye vigezo | Zoezi hili lilifanikiwa<br><br>Zoezi hili linaendelea<br><br>Zoezi hili lilifanikiwa |
| 3 | Kuimarisha maswala ya jinsia na utawala bora | Kaya za walengwa wa mazingira hatarishi na VVU/UKIMWI zilitembelewa | • Kaya 27 ziliweza kutembelewa<br>• Rufaa 15 zilitolewa kwa mlengwa aliye hitaji huduma tofauti tofauti | • Baadhi ya kaya wanahama kutoka sehemu mmoja kwenda nyingine bila kutoa taarifa kwa watoa huduma |
| | | Vikundi vilivyo kopeshwa vinaendelea na marejesho | • Vikundi vitatu vinaendelea na marejesho ambanyo ni:-amkeni , faruna Tushikamane ambapo kikundi kimoja kimemaliza mkpo huo ambacho ni.magufuli na maendeleo | • Zoezi la urejeshaji mikopo katiika Kata linaendelea vizuri |
| | | • Huduma mbalimbali | • Huduma hizo ni kama | • Zoezi lilifanikiwa |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | ziliweza kutolewa katika kaya 27 za watu wanaoshi katika mazigira hatarishi<br>• Nilisimamia kuunda jiwa Club ya Ukimwi nyerere | elimu ya lishe, Uchizi na usalama wa mtoto na elimu ya kujiinua kuichumi<br>• Club hiyo inajumla ya washi na ilizinduliwa na mwenge wa uhuru 2018 | • Zoezi zililifanikiwa kwa asilimia kubwa |
| 4 | Kuboresha huduma na kupunguza maambukizi ya HIV/AIDS | • Elimu ya umuhimu wa upimaji inaendelea mabapo watoa huduma ngazi ya jamii CCW hufanya upimaji kwa mtu aliyehiyari | • Baadhi ya kaya hizo wamefanya upimaji na ukikitwa na maambukizi hupewa rufaa kwenda (CCT) | • Zoezi linaendelea vizuri |

**HUDUMA ZILIZOPO**

| NA | HUDUMA ZA KIUCHUMI | HUDUMA ZA KIJAMII | SEKTA BINAFSI |
|---|---|---|---|
| 1 | Barabara | - Elimu ya Msingi/Sekondari | - Mashine za kusaga na kukoboa |
| 2 | Umeme (Nishati) | -Maji | - Maduka madogo madogo |
| 3 | Mawasiliano (Simu) | -Misikiti | - Migahawa midogo midogo |
| 4 | Soko la wakulima | -Makanisa | - Baa za pombe za kienyeji/kisasa |

## 1.4 SHUGHULI ZA KIUCHUMI WANAZOFANYA WANANCHI WA KATA HII.

2. Biashara ndogondogo
3. Kilimo
4. Ufugaji mdogomdogo
5. Ususi
6. Ufyatuaji wa matofali
7. Ushonaji na ujenzi
8. Wafanyakazi wa serikali na Mashirika.

## 1 KILIMO NA MIFUGO.

| NA: | AINA YA MAZAO | ENEO LILILOPANGWA | MAVUNO (TANI) | MAZAO YA BUSTANI | MAVUNO TANI |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | MAHINDI | 42.5 (HA) | 106.25 | PILIPILI | 0.5-0.6 |
| 2 | MPUNGA | 6.5 | 22.75 | MATANGO | 0.5-5 |
| 3 | MTAMA | 1.8 | 2.7 | MCHICHA | 0.6-0.48 |
| 4 | MIHOGO | 4.8 | 48 | CHINESE | 3.5-4.2 |
| 5 | VIAZI VITAMU | 9.5 | 95 | NYANYA | 2.5-15 |
| 6 | GIMBI | 2 | 16 | NYANYA CHUNGU | 0.2-1.4 |
| 7 | PAMBA | 1.0 | 1.3 | PAPAI | 0.9-13.5 |
| 8 | MIWA | 4.6 | 6.9 | TIKITI MAJI | 1.2-2.4 |
| 9 | KOROSHO | 2 | 2.2 | JUMLA | 6.4.18 (TANI) |
| 10 | ALIZETI | 1.5 | 2.1 | | |
| 11 | KUNDE | 1.0 | 1.1 | | |
| 12 | KARANGA | 5.7 | 8.55 | | |
| 13 | NJUGU MAWE | 1.6 | 2.56 | | |
| 14 | MAHARAGE | 5.3 | 7.95 | | |
| | **JUMLA** | **89.8** | **323.36 (TANI)** | | |

Jumla ya eneo lililolimwa msimu wa kilimo **2017/2018** Kata ya Kazima ni **106.9** hekta.
Hali ya chakula ni nzuri mazao yanaendelea kuvunwa. Pia bei ya chakula ni nzuri mfano Mahindi yanapatikana kwa Tsh. 325/= kwa kilo, shamba darasa lipo katika hatua ya kuvunwa.

**SEKTA YA MIFUGO.**
Walimu wa kata hii hujishughulisha na ufugaji wa mifugo mbalimbali kama ilivyoainishwa katika jedwali hapa chini.

| AINA YA MIFUGO | NG'OMBE WA MAZIWA KISASA | NG'OMBE WA MAZIWA KIENYEJI | MBUZI | KONDOO | NGURUWE | KUKU | MBWA | BATA | NJIWA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| IDADI | 46 | 105 | 457 | 54 | 297 | 2351 | 130 | 809 | 254 |

## 1.5 SEKTA YA MAJI.
Kata ya Kazima ina kisima kirefu kimoja kirefu na kifupi kimoja vyote hivi vipo mtaa wa kazima na gati moja la bomba la maji lililopo katika eneo la yelusallemu mtaa wa Kalangao.

**CHANGAMOTO.**
Kata ya Kazima ni moja ya eneo lenye shida kubwa ya maji ukilinganisha na idadi ya watu kama inavyoonekana katika jedwali na idadi ya watu wa makazi hivyo kuna hitajika jitihada za makusudi katika kutandaza mabomba na uchimbaji wa visima vya maji katika eneo hilo.

**SEKTA YA AFYA.**
Kata ya Kazima haina kituo cha afya wala zahanati hivyo kupelekea wakazi wa kata hii kulazimika kupata huduma za afya katika vituo vyqa watu binafsi ambavyo ni ghali sana.

**B. AFYA KINGA.**
Ofisi ya kata kwa kushirikiana na wataalamu waliopo katika kata hii pamoja na viongozi wa serikali za mitaa huratibu na kusimamia usafi wa mazingira kwa kudhibiti uchafu katika Kata. Pamoja na jitihada hizo tunaendelea kuwafundisha wakazi umuhimu wa kutunza mazingira na usafi kwa ujumbe na ujenzi wa vyoo bora.
**CHANGAMOTO.**
Maeneo mengi katika kata hii kutopimwa kupelekea kutokuwa na eneo maalum la ukusanyaji wa mifumo ya maji hapa kipindi cha mvua hususani mitaa ya kazima na Kapalangao. Kwa kuwa hatuana barabara wala mitalo hivyo tunaomba Serikali itusaidie walau kilometa **10** pamoja na mitalo yake. Aidha uhaba mkubwa wa magati ya maji nayo ni tatizo kwani kuna gati moja tu Kata nzima.

## 1.6 SEKTA YA ELIMU.
Kata ya Kazima ina shule mbili (2) Mkapa shule ya msingi na Rungwe Sekondari

**SHULE YA MSINGI MKAPA.**
**TAARIFA YA WANAFUNZI**

| SHULE | IDADI | | AWALI | | I | | II | | III | | IV | | V | | VI | | VII | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| MKAPA | WV | WS | WV | WS | WS | WV | WS | WV | WS | WV | WS | WV | WS | WV | WS | WV | WS | WV |
| | 1183 | 1289 | 149 | 201 | 270 | 276 | 228 | 219 | 161 | 188 | 112 | 131 | 109 | 99 | 88 | 104 | 65 | 71 |
| **JML** | **2,472** | | **350** | | **546** | | **447** | | **349** | | **243** | | **208** | | **192** | | **136** | |

## IDADI YA WALIMU.

| MAHITAJI | WALIOPO | PUNGUFU |
|---|---|---|
| 45 | 25 | 20 |

**MAJENGO YA SHULE /MIUNDO MBINU YA SHULE.**

| MAELEZO | MAHITAJI | YALIYOPO | PUNGUFU |
|---|---|---|---|
| MADARASA | 52 | 08 | 43 |
| NYUMBA ZA WALIMU | 25 | 01 | 24 |
| OFISI | 6 | 2 | 4 |
| MATUNDU YA VYOO | 92 | 11 | 81 |
| STOO | 2 | - | 2 |

**SAMANI ZA SHULE**

| AINA | MAHITAJI | VILIVYOPO | PUNGUFU |
|---|---|---|---|
| MEZA | 21 | 11 | 10 |
| VITI | 21 | 14 | 7 |
| MADAWATI | 686 | 566 | 120 |
| KABATI | 6 | 2 | 4 |

## (B) ELIMU YA SEKONDARI

Kata Kazima ina Shule ya Sekondari moja ambayo ni Sekondari ya Rungwa.

## IDADI YA WANAFUNZI.

| ME | KE | JUMLA |
|---|---|---|
| 598 | 461 | 1059 |

## 1.7 IDADI YA WALIMU.

Shule ya sekondari Rungwa ina walimu wafuatao.

| MAHITAJI | WALIOPO | PUNGUFU |
|---|---|---|
| 33 | 41 | - |

Katika takwimu hizi za walimu tatizo lipo kwa masomo ya Sayansi ambapo kuna upungufu wa walimu watatu **(3)**

## MIUNDOMBINU YA SHULE.

| AINA | MAHITAJI | YALIYOPO | PUNGUFU |
|---|---|---|---|
| MADARASA | 26 | 23 | 3 |
| NYUMBA ZA WALIMU | 41 | 2 | 39 |
| OFISI | - | - | - |
| STOO | 2 | - | 2 |
| MEZA/VITI | 41 | 20 | 21 |
| VITI/MEZA/WANAFUNZI | 1,041 | 894 | 147 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| VYOO MATUNDU | 33 | 20 | 13 |
| BWALO | 1 | - | 01 |
| MAKTABA | 1 | - | 01 |
| MABWENI | 2 | 2 | - |
| JENGO/UTAWALA | 01 | - | 01 |
| MAABARA | 4 | 3 | 1 |
| JIKO | 1 | 1 | - |

Changamoto upande wa Rungwa sekondari eneo ni dogo sana kiasi kwamba hakuna hata viwanja vya michezo. Hivyo tunaomba liongezwe ili kukidhi mahitaji yote yanayotakiwa katika utoaji wa elimu.
Utatuzi wa changamoto tunaishauri ofisi ya Mkurugenzi kutoa ushirikiano juu ya mgogoro wa ardhi katika eneo la Rungwa Sekondari.

**IDADI YA WATUMISHI WALIOPO KATANI.**

| **UATA WALA** | | **ELIMU/MSINGI NA SEKONDARI** | | **KILIMO /MIFUGO** | | **M/JAMII** | | **AFYA** | | **MISITU** | | **JUMLA** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| ME | KE | ME | KE | ME | KE | ME | KE | ME | KE | ME | KE | ME$KE |
| 2 | 2 | 35 | 27 | 1 | 1 | - | | - | - | - | - | 68 |

OMBI; Tunaomba tupatiwe Afisa wa Afya wa kata ya Kazima.

**1.8 ULINZI NA USALAMA.**

Hali ya ulinzi na usalama kwa kipindi hiki katika kata ni ya wastani kwani vikao vinaendelea kufanyika katika kuhamasisha ulinzi na usalama wa wananchi wamejiwekea utaratibu wa ulinzi shirikishi katika maeneo yao. Aidha kumeibuka tabiya ya wananchi kuanza kuchimba mchanga katika maeneo ya makazi na kusababisha mtu mmoja kufukiwa na kifusi na kufariki tukio hili lilitokea tarehe **29/9/2018** katika mtaa wa Kapalangao, hivyo tumejitahidi kuwahamasisha wananchi kuacha tambia hiyo mara moja. Hakuna matukio makubwa yanayojitokeza kwa kipindi hiki zaidi ya hilo.

**1.9 UTAWALA BORA.**

Kwa kipindi cha Julai hadi Septemba Vikao mbalimbali vimefanyika vikiwemo mikutano ya hadhara, katika vikao hivyo kero mbalimbali na malalamiko mbalimbali vimeshughulikiwa.

**IDADI YA VIKAO**

| **VIKAO VYA WDC** | | | **VIKAO VYA S/MITAA** | | | **MIKUTANO YA HADHARA** | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| KAWAIDA | MAALUM | JUMLA | KAWAIDA | MAALUM | JUMLA | KAWAIDA | MAALUM | JUMLA |
| 1 | - | 1 | 3 | 2 | 5 | 2 | - | 2 |

**CHANGAMOTO.**

1. Kata ya kazima haina jengo la ofisi hivyo shughuli zote za ofisi bado zinafanyika kata ya Kawajense kiasi ambacho kinapelekea wananchi kushindwa kuhudumiwa kutokana na umbali
2. Ukosefu wa miundombinu ya Barabara mifereji ya maji
3. Ukosefu wa maji safi na salama

**ELIMU YA URAIA NA UTAWALA BORA.**

Wananchi wanaendelea kupewa elimu ya uraia na utawala bora katika mikutano ili waweze kuelewa wajibu wao na majukumu ya serikali katika kuleta maendeleo. Aidha elimu ya mapambano dhidi ya madawa ya kulevya na ukimwi kupewa kipaumbele kwani serikali ya awali ;ya tano imeamua kushughulika na matatizo hayo

**RUSHWA NA UBADHIRIFU**

Wananchi kila mkutano wa hadhara wamekuwa wakielimishwa umuhimu wa kuwafichua wanaotoa na kupokea rushwa na wabadhilifu wa mali za umma.

Na wale wanaosemwa semwa hatua huchukuliwa ili wahudumie wananchi na kuwapa wananchi uhuru wa kutoa mawazo yao, na sasa hivi wananchi walio wengi wanaimani na serikali yao ya awamu ya tano (5) kwa kutoa huduma ipasavyo.

**2.0 UKIMWI.**

Viongozi na wataalamu wamefanya mikutano ya hadhara na kutembelea baadhi ya maeneo, kutoa tahadhari ya ugonjwa huu hatari ambao hauna dawa na kuwasisitiza kupima afya zao mara kwa mara na kuwa na mpenzi mmoja mwaminifu au kuacha kabisa ngono zembe na kutumia salama.

MH: MWENYEKITI NAOMBA KUWASILISHA.

**...................**

**ELIAS MWANISAWA**

**DIWANI KATA YA KAZIMA.**

**KATA YA NSEMULWA**

**TAARIFA YA UTEKEREZAJI WA SHUGHULI ZA MAENDELEO KATA YA NSEMULWA KWA KIPINDI CHA KUNZIA JULAI –SEPTEMBA 2018/2019 ROBO YA KWANZA**

## 1. UTANGULIZI

**MHE. MSTAHIKI MEYA**
Kata ya Nsemulwa na miongoni mwa kata **15** zinazounda Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda na ipo umbali wa km **4** kotoka makao Makuu ya Manispaa
**MIPAKA**

1. Kwa upande wa kusini kata imepakana na kata ya uwanja wa ndege
2. Kwa upande wa Kaskazini kata imepakana na kata ya kazima
3. Kwa upande wa Mashariki kata hii imepakana na kata ya Mtapenda iliyoko Halmashauli ya Nsimbo.
4. Upande wa magharibi kata imepakana na kiata ya Kashaulili

**UONGOZI (UTAWALA)-**Mheshimiwa Diwani wa kata yupo aliyepita kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi (CCM).
- kata hii ina mitaa **5** na kijiji **1**
- Uongozi ndani ya mitaa na kijiji upo kama ifuatavyo:-

i. Mtaa wa Nsemulwa mwenyekiti wa mtaa yupo na wajumbe wake **4** na **1** huwa hafiki kwenye kikao.
ii. Mtaa wa Tulieni mwenyekiti wa mtaa yupo na wajumbe wapo **4** na **1** alishahama
iii. Mtaa wa Kichangani mwenyekiti wa mtaa yupo wajume **3** wapo, mjumbe **1** alifariki na mjumbe **1** amejiachisha ujumbe kwa kutohudhulia vikao vya kisheria vya serikali ya mtaa zaidi ya mwaka **1**.
iv. Mtaa wa Kilimani mwenyekiti yupo na wajumbe wake wote wapo
v. Mtaa wa Migazini mwenyekiti wa mtaa yupo na wajumbe wanaofanya kazi wapo **2**
vi. Kijiji cha Shankala mwenyekiti wa kijiji yupo pamoja na wenyeviti **3** wa vitongoji wapo.

## 2. IDADI YA WATU NA MAKAZI

| IDADI YA KAYA | KAYA ZENYE UWEZO WA KUFANYA KAZI | KAYA ZISIZO NA UWEZO | IDADI YA WATU | | WATU WENYE UWEZO WA KUFANYA KAZI | | WASIO NA UWEZO WA KUFANYA KUFANYA KAZI | | WATOTO YATIMA | | WALEMAVU WA VIUNGO | | WATOTO WENGINE | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2343 | 1734 | 509 | ME | KE | ME | KE | ME | KE | ME | KE | ME | KE | ME | KE |
| | | | 4192 | 5781 | 2203 | 2539 | 430 | 642 | 2480 | 2664 | 1691 | 1231 | 2196 | 2402 |

### 3. SHUGHULI ZA KIUCHUMI WAZIFANYAZO WANANCHI WA KATA YA NSEMULWA

Kilimo cha kutumia jembe la mkono, kilimo cha kutumia matrekta pamoja na kilimo cha kutumia wanyama kazi ambapo wakulima waliowengi hufanya shughuli zao hizo za kilimo nje ya kata hii ya Nsemulwa.

### 4. HUDUMA ZA KIJAMII ZINAPATIKANA NDANI YA KATA HII

- Ipo shule ya msingi 1 inayotoa huduma kwa mitaa yote **5**.
- Misikiti **4**na makanisa **12**.
- Lipo genge **1** litumikalo kama soko maarufu kwa jina la soko la Kwarakwacha ambalo lina maelekezo ya kuhamishwa na kupelekwa eneo lililopimwa kisheria wakati wowote kuanzia sasa.

### 5. WATUMISHI WALIOPO NGAZI YA KATA

| **Na** | **IDARA** | **JINSIA** | | **JUMLA** |
|---|---|---|---|---|
| | | **ME** | **KE** | |
| 1 | UTAWALA | 1 | 0 | 1 |
| 2 | AFISA ELIMU KATA | 0 | 1 | 1 |
| 3 | AFYA | 0 | 1 | 1 |
| 4 | KILIMO, USHIRIKA NA MIFUGO | 1 | 0 | 1 |
| 5 | M/JAMII | 0 | 1 | 1 |
| 6 | ELIMU MSINGI | 12 | 12 | 24 |

### 6. VIKAO NA MIKUTANO YA KATA VYA KISHERIA NA DHARULA

| **TAREHE YA KIKAO** | **MKUTANO** | **WDC KAWAIDA** | **WDC DHARULA** |
|---|---|---|---|
| 03/07/2017 | | 1 | 1 |
| 09/08/2018 | | | 1 |
| 05/09/2018 | 4 | | |
| Jumla ya vikao vilivyofanyika | 3 | | |

| | |
|---|---|
| **MKUTANO** | **4** |
| **VIKAO** | **3** |

### 7. MIRADI YA MAENDELEO

Katika kata hii kuna miradi iliyoibuliwa na wananchi na kuanza kutekelezwa na wananchi pamoja na ofisi ya Mkurugenzi kama ifuatavyo:-

- Ujenzi wa ofisi ya Kata ambayo inajengwa Mtaa wa Kichangani na ujenzi huo ulianza mwaka **2013** hadi mwaka **2014** uliposimama kwa ukosefu wa fedha.

| **AINA YA MRADI** | **CHANZO CHA FEDHA** | **FEDHA** | | | **HATUA YA UTEKELEZAJI** | **MAELEZO** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **ILIYOPOKELEWA** | **ILIYOTUMIKA** | **ILIYOBAKI** | | |
| Ujenzi wa ofisi ya Mtendaji Kata ya | Halmashauri | 21,221,969.50 | 21,221,969.50 | - | Jengo lote limepauliwa na kuwekwa fremu | Fedha Tshs. 22,380,682.69 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Nsemulwa mwaka 2013/2014 | | | | | za madirisha na milango ya nje, fedha pungufu ni Tshs. 9,442,684.50 kwa mujibu wa mkataba wa ujenzi bado umesimama kwa kukosa fedha | zilizotumika kumlipa mkandarasi kwa kuzingatia mkataba pia kununua vifaa vya nguvu za wananchi |

| **AINA YA MRADI** | **CHANZO CHA FEDHA** | **FEDHA** | | | **HATUA YA UTEKELEZAJI** | **MAELEZO** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **ILIYOPOKELEWA** | **ILIYOTUMIKA** | **ILIYOBAKI** | | |
| Ujenzi wa ofisi 1 ya Kijiji cha Shankala | Halmashauri wananchi | 15,000,000/=<br>3,000,000/=<br>18,000,000/= | 18,000,000/= | - | Jengo lote limepauliwa na kuwekwa fremu za madirisha na milango ya nje, fedha pungufu ni Tshs. 7,000,000/= kwa mujibu wa mkataba wa ujenzi bado umesimama kwa kukosa fedha | Fedha Tshs. 7,000,000/= jengo limepauliwa lote milango na fremu za madirisha vimewekwa kasoro dilisha moja halijawekwa fremu jumla Tshs. 7,000,000/= zinatakiwa ili kumalizia jengo |
| Ujenzi wa kituo cha afya mtaa wa Kilimani | Halmashauri na Wananchi | 1,650,000/= | 1,650,000/= | - | Tripu 9 za mawe na triup 5 za mchanga ambazo ni nguvu za wananchi na Halmashauri zipo eneo la ujenzi | Uhamasishaji juu ya uchangiaji nguvu za wananchi unaendelea |
| **Jumla Kuu** | | **1,650,000/=** | **1,650,000/=** | | | |

## 8. UJENZI WA VYUMBA VIWILI VYA MADARASA YA SHULE YA MSINGI NSEMULWA

| **AINA YA MRADI** | **CHANZO CHA FEDHA** | **FEDHA** | | | **HATUA YA UTEKELEZAJI** | **MAELEZO** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **ILIYOPOKELEWA** | **ILIYOTUMIKA** | **ILIYOBAKI** | | |
| Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa ya shule ya msingi Nsemulwa mwaka 2017/2018 Tshs. 25,00,000/= | PAR FUND Halmashauri M,Jimbo Ofisi DC | 2,000,000/=<br>11,540,000/=<br>4,566,000/=<br>200,000/=<br>350,000/= | 2,000,000/=<br>11,540,000/=<br>4,566,000/=<br>200,000/=<br>350,000/=<br>Nguvu kazi | -<br>-<br>363,000/= | Jengo lote limepauliwa fedha pungufu ni Tshs. 3,000,000/= | Fedha Tshs. 11,540,000/= zilizotumika kwa malipo ya fundi ujenzi ununuzi wa |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Wananchi | Nguvu kazi | | | ujenzi unaendelea vizuri | vifaa vya ujenzi |
| Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa pamoja na ofisi 1 ya walimu | Mfuko wa jimbo | 3,000,000/= | | - | Ujenzi wa boma umeanza | Kuta za boma zimeanza kuinuliwa |
| Ruzuku ya mapunjo ya uendeshaji wa ofisi za mitaa pamoja na mapunjo ya mradi wa maendeleo | Halmashauri ya Manispaa | 701,495 | 460,000/= imetumika kwa<br>(i) Mchanga tripu 3 S/M Nsemulwa Tshs. 70,000@<br>(ii) 203,000/= zimetumika kwa ajili ya shughuli ya ofisi za Mitaa<br>(iii) Kokoto tripu 1 Tshs. 250,000/= | 38,495/= | | |
| **SALIO LILILOPO BENK** | | | | **2,231,521.37** | | |

## 9. MAPATO

| Na | JINA LA MRADI CHANZO CHA FEDHA | CHANZO CHA FEDHA | MAPATO | JUMLA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | SALIO ANZIA | HALMASHAURI WANANCHI | 3,856,026.37 | 3,856,026.37 |
| 2 | RUZUKU KUTOKA MMC | HALMASHAURI | 701,495/= | 701,495/= |
| | **JUMLA KUU** | | | **3,856,026.37** |

**MATUMIZI**

| NA | JINA LA MRADI | CHANZO CHA FEDHA | FEDHA TENGWA | FEDHA TOLEWA | TUMIKA | BAKI | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Salio anzia | Halmashauri Wananchi | 3,856,026.37 | 3,856,026.37 | 1,663,000/= | 2,231,521.37 | (i) 460,000/= imetumika kwa<br>(ii) Mchanga tripu 3 S/M Nsemulwa Tshs. 70,000@<br>(iii) 203,000/= zimetumika kwa ajili ya shughuli ya |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | ofisi za Mitaa<br>(iv) Kokoto tripu 1 Tshs. 250,000<br><br>Katika salio anzia ya Tshs. 3,856,026.37 kiasi cha Tshs. 1,000,000/= kimetumika kununua mifuko 50 ya cementi ya kujengea boma S/M Nsemulwa kila mfuko umegharimu Tshs. 20,000/= |

## 10. SEKTA YA MAENDELEO YA JAMII

i. Kushiriki katika mkutano wa hadhara, mtaa wa Migazini, katika mkutano huu elimu ilitolewa kwa wazazi/walezi kupenda kuongea na watoto wao hasa wa jinia ya kike ili kuwakinga na mimba za utotoni na kupenda kukagua madaftari ili kuona maendeleo yao.

ii. Kutembelea kiundi cha chaki, na kuwahimiza kufanya marejesho yao ya mkopo na pia kuwahamasisha kujishughulisha na kuacha kujibetweka.

iii. Kushirikiana na watendaji wa mitaa wa Kichangani na Tulieni katika kutatua kesi mbalimbali za kijamii zilizowasilishwa ofisi. Kesi hizi zilitatulika kwa kutoa ushauri wa kitaaluma.

iv. Kukutana na walemavu ambao wapo kwenye mchakato wa kuunda kikundi kwa kuwapa maelekezo yanayohitajika ili kufanikiwa kuunda kikundi chao na kukisajili.

v. Kushiriki katika mkutan wa hadhara na Mhe. Meya wa Manispaa ya Mpanda. mkutano ulifanyika lengo ikiwa ni kusikiliza kero za wananchi na kuzitatua, wananchi walishiriki kwa wingi na kuwasiisha kero zao kwa msitahiki Meya ambae alizitolea ufafanuzi.

vi. Kushiriki katika kikao cha WDC kilichofanyika Ofisi ya Kata Nsemulwa kwa ajili ya kujadili maendeleo ya Kata.

vii. Kutembelea na kuongea na kikundi cha vijana kwa ajili ya kuwapa maelezo ya kukamilisha kusajili kikundi chao cha vijana.

viii. Kushiriki katika kikao cha WDC kilichofanyika kwa ajili ya kutatua malalamiko yaliyowasilishwa na ACT ofisini, malalamiko hayo yalifanyiwa kazi na walalamikaji walilidhia na majibu ya wajumbe.

Ifutayo ni taarifa ya marejesho kwa vikundi vinavyodaiwa Kata ya Nsemulwa kwa robo hii ya July-Septemba.

| **JINA LA KIKUNDI** | **MTAA KILIPO** | **BIASHARA WANAZOFANYA** | **MKOPO WALIOPEWA KIASI** | **KIASI KILICHORE JESHWA** | **DENI LILILOBAKI** |
|---|---|---|---|---|---|
| FEVAM GROUP | KICHANGANI | KUSINDIKA WINE NA KUTENGENEZA SHANGA | 3,300,000/= | 2,203,000/= | 1,097,000/= |
| TWIJUMILE | KILIMANI | | 2,200,000/= | 1,800,000/= | 400,000/= |
| MWIZA GROUP | NSEMULWA | KUSINDIKA WINE NA | 5,500,000/= | 918,000/= | 4,582,000/= |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | KUTENGENEZA UNGA WA LISHE | | | |
| COOPERATION GROUP | MGAZINI | KUTENGENEZA CHAKI | 11,000,000/= | 459,000/= | 10,541,000/= |

Pia Kata hii ya Nsemulwa ina vikundi viwili ambavyo ni vidaiwa sugu

| JINA LA KIKUNDI | MTAA KILIPO | BIASHARA WANAZOFANYA | MKOPO WALIOPEWA | KIASI KILICHOREJESHWA | DENI LILILOBAKI |
|---|---|---|---|---|---|
| KENAMADEVA | NSEMULWA | | 1,100,000/= | 1,063,000/= | 37,000/= |
| AMANI | NSEMULWA | | 1,320,000/= | 442,500/= | 877,500/= |

## 11. SEKTA YA KILIMO USHIRIKA NA MIFUGO

| Na | SHUGHULI ZILIZOFANYIKA | MAHALI | WAHUSIKA |
|---|---|---|---|
| 1 | Kuhamasisha kilimo cha pamba na korosho kwa wananchi wote Kata ya Nsemulwa kupitia mikutano ya hadhara | Kata na Mitaa yote | • Afisa kilimo<br>• Watendaji wote wa Mitaa yote<br>• Pamoja na wananchi |
| 2 | Ukaguzi wa vyama, nguruwe 3 na mbuzi 1 | • Nsemulwa<br>• Kichangani | • Afisa kilimo na mifugo<br>• Muuza nyama aliyekaguliwa |
| 3 | Kuwasajili wakulima 19 wanaohitaji mbegu za pamba na wakulima 5 wanaohitaji mbegu za korosho lakini bado zoezi linaendelea la kuwasajili | • Kata nzima | • Afisa Kilimo<br>• Wananchi wanao jisajili |
| 4 | Kuandaa taarifa za kazi za robo, mwezi na mwaka za Kata ya Nsemulwa | • Kata | • Afisa kilimo |
| 5 | Tiba kwa mifugo, nguruwe 3 na mbuzi 1 | • Kilimani<br>• Kichangani | • Afisa kilimo na mifugo<br>• Mwananchi aliyetibiwa mifugo |
| 6 | Kuhasi mifugo, mbwa 1 na Nguruwe 2 | • Kichangani | • Afisa kilimo na mifugo<br>• Mwananchi ambaye mifugo yake ilihasiwa |
| 7 | Chanjo ya mifugo, CBPP (Homa ya mapafu) Ng'ombe waliochangwa kwa Kata nzima wapo 895 | • Kata nzima | • Wataalamu wa mifugo kutoka Manispaa wakishirikiana na Kampuni ya Baclema co. LTD |

## 12. SEKTA YA UVUVI

**TAARIFA YA SHUGHULI ZA UVUVI KATA YA NSEMULWA**

Idadi ya Mabwawa **3** yaliyo na samaki aina ya sato yenye ukubwa wa eneo **391**$m^2$

**SHUGHULI ZILIZOFANYIKA**

i. Kusimamia uvunaji wa samaki katika mabwawa
ii. Kutoa elimu ya ufugaji wa samaki kwa wananchi
iii. Kutoa elimu ya uuzaji wa samaki kwa wafanyabiashara **4** katika soko la Kwalakwacha

**CHANGAMOTO**

i. Ukosefu wa usafiri kutokana na kuwa na eneo la kazi zaidi ya moja
ii. Shajala
iii. Ukosefu wa vitendea kazi

## 13. SEKTA YA AFYA

**AFYA YA UTEKELEZAJI JULY-SEPTEMBER 2018 KWA KAZI ZILIZOFANYIKA IDARA YA AFYA KATA YA NSEMULWA**

| NA | SHUGHULI | HALI YA UTEKELEZAJI | CHANGAMOTO | MPANGO MKAKATI |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Kuratibu na kusimamia kampeni ya kitaifa ya usafi wa mazingira | • Elimu imetolewa juu ya umuhimu wa kila kaya kuwa na choo bora na kukitumia Elimu imetolewa katika mtaa wa Nsemulwa na Kilimani.<br>• Zoezi linaendelea katika Mitaa ya Kichangani, Migazini na Kijiji cha Shankala | Zoezi la kutoa Eliu na ukaguzi linaendelea kwa ukubwa wa kata hii tunaendelea na zoezi | Ukaguzi wa Mitaa yote kuhusu ujenzi wa vyoo bora na matumizi ya vyoo kwa Kaya zote Katani |
| 2 | Ukaguzi wa majengo ya biashara na viwanda vyote Katani Nsemulwa | Majengo yote ya biashara yamekaguliwa na wananchi wamepewa elimu juu ya utunzaji wa vyakula salama | Hali ya wafanyabiashara wengi ni wajasiliamali Taratibu nyingi zinahitaji mtaji katika uwekezaji | Kutoa elimu kwa wafanyabiashara ya vyakula ili kuzingatia sheria/taratibu za vyakula |
| 3 | Kudhibiti uchafu na uchafuzi wa mazingira | Kuainisha madampo yote na kuyaondosha mitaani | Usafilishaji wa taka hizo kwani hali ya mgari ya taka ni mabovu | Kuondoa hali hiyo mara moja magari yatakapotengemaa |
| 4 | Kuzuia magonjwa ya mlipuko | Elimu kwa wananchi juu ya matumizi sahihi ya kutumia maji salama ya kunywa, kunawa mikono baada ya kutoka chooni | Uelewa mdogo wa wananchi juu ya matumizi shihi ya maji salama ya kunywa | Kuelimisha na kusimamia juu ya mtumizi sahihi ya maji salama ya kunywa. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 5 | Kusimamia usafi wa kila jumamosi ya mwisho wa mwezi | Kuhakikisha wananchi wanajitokeza kwa wingi siku hiyo kufanya usafi | Baadhi ya wananchi kutohudhuria katika zoezi hilo la usafi | Kuwachukulia hatua wananchi wote wasiojitokeza kwenye usafi |

**14. SEKTA YA ELIMU MSINGI**

Mpaka taarifa hii inaandaliwa hakuna taarifa yoyote iliyoletwa kutoka S/M Nsemulwa licha ya Mratibu elimu kata kupewa taarifa muda mrefu wa kuwasilisha taarifa hii katani.

**15. UJENZI WA VYUMBA BORA**

- Katika kukabiliana na ujenzi holela wa makazi ofisi ya Mkurugenzi imeshatuma timu ya wataalam wa ardhi kwa ajili ya upimaji wa mradi wa viwanja awamu ya pili mtaa wa Tulieni ambapo zoezi hilo linaendelea mpaka sasa.
- Pia katika kudhibiti ujenzi holela wa nyumba wananchi wameshuliwa kutonunua viwanja visivyopimwa maarufu kwa jina la (vishamba vidogo vidogo). Pamoja na hayo kampuni ya Makipando pia ilipata kibali kutoka ofisi ya Mkurugenzi kwa ajili ya upimaji pamoja na urasimishaji wa viwanja mtaa Tulieni.

**16. ONYAKA**

Katika kukabiliana na ujenzi wa nyumba bora wananchi wameelimishwa wanapojenga nyumba watumie tofali za kuchoma na wapaue kwa kutumia bati na sio nyasi.

**17. ULINZI NA USALAMA**

Kwa kipindi cha kuanzia **July - September2018** katika kata hii kumetokea vitendo vya uharifu iiwemo wizi na taarifa hizo zilifikishwa kituo cha polisi na hatua zilichukuliwa pia wananchi wameelemishwa juu ya umhimu wa kujitokeza katika ulinzi shirikishi (polisi jamii) kupitia mikutano ya hadhara.

Wenyeviti wa mitaa pamoja na watendaji wa mitaa wamefanya agenda hiyo ya ulinzi na salama kuwa ya kudumu kila wanapoitisha mikutano ya hadhara kuizungumzia.

**18. HALI YA MAJANGA**

Kwa kipindi cha **Julai - September 2018** hakuna janga lolote lililojitokeza katika Kata hii.

**19. MATUKIO KATANI JULAI – SEPTEMBER 2018**

Kwa kipindi cha **Julai - September 2018** kumetokea tukio moja la kujinyonga mwananchi mmoja katika eneo la Mtaa wa Migazini alitumia mti ulio kuwa kando kando ya reli iendayo Tabora tukio lilifanyika tarehe 14/10/2018 na alijulikana kama ni mwananchi aliyetoka Mkoa wa Geita, taarifa ilifikishwa kituo cha polisi na maiti ilichukuliwa na polisi kwa hatua za mazishi.

**20. MIUNDOMBINU ILIYOPO HAPA KATANI**

**(i) BARABARA**

- Katika kata hii zipo barabara chache zilizochongwa kwa mitambo na kumwagwa vifusi mtaa wa Kichangani na baadhi ya mitaa hakuna kabisa barabara zilizochongwa.
- Mhe. Diwani wa kata hii ya Nsemulwa amewasiliana na wataalam wa TARURA kwa ajili ya kupunguza kero hiyo, na wataalamu wameahidi kufanya kazi hiyo mara tu watakapokuwa wameingiziwa fungu la matengenezo ya barabara kwa mwaka wa fedha 2018/2019.
- Pia wananchi walio wengi ndani ya kata hii wanatumia umeme wa SOLA.
- Upande wa mawasiliano ya simu wananchi ndani ya kata hii wanatumia mawasiliano ya simu za mkononi kwa kutumia mitandao ifuatayo:-
  VODACOM, TIGO, AIRTEL na HALOTEL

**21. NISHATI**

Nishati watumiayo wananchi ndani ya kata hii ni kama ifuatavyo:-

- Umeme wa TANESCO
- Umeme wa SOLA

Ambao asilimia kubwa ya wananchi wanaotumia umeme wa sola ukilinganisha na umeme wa Tanesco

**22. MAFANIKIO YALIYOPATIKANA KWENYE KATA**

1. Kata kukubaliwa mradi ujenzi wa kituo cha afya
2. Mkurugenzi kupima viwanja awamu ya pili
3. Kampuni ya MAKPANDO kubaini maeneo ya wakazi na yasiyo ya makazi kwa asilimia 90%

**23. CHANGAMOTO ZILIZOMO NDANI YA KATA**

1. Miundombinu ya barabara ni mibovu
2. Idadi ya visima na magati ya maji havitoshi
3. Kata haina kituo cha afya
4. Kata haina soko la uhakika
5. Kukosekana kwa fedha ya kumalizia miradi viporo

**24. UFUMBUZI WA CHANGAMOTO**

Wananchi wanaendelea kukusanya nguvu zao katika kutekeleza aslimia 20% ya kila mradi. Pia ofisi ya Mkurugenzi imeshaahidi kwa baadhi ya miradi kuikamilisha mara tu fedha zitakapoingizwa kutekeleza mradi ya 2018/2019.

**25. HITIMISHO**

Uongozi wa kata pamoja na uongozi wa mitaa utaendelea kuhamasisha wananchi juu ya umuhimu wa kuchangia nguvu zao katika miradi ya maendeleo pia ofisi ya Mkurugenzi inaombwa kuleta fedha kwa wakati mara tu wananchi wanapokuwa wameibua miradi hiyo na kuanza kutekeleza kwa kusogeza nguvu zao eneo la mradi.

Naomba kuwasilisha,

**MHE. DIWANI**
**BAKARI KAPONA**
**KATA YA NSEMULWA**

**KATA YA MAJENGO**
**TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 KATIKA KIPINDI CHA JULAI HADI SEPTEMBA 2018 KATIKA KATA YA MAJENGO.**

1. **UTANGULIZI**
   Kata ya Majengo ni miongoni mwa kata 15 zilizopo katika Manispaa ya Mpanda, mkoa wa Katavi . Kata hii imeundwa na mitaa 3 ambayo ni mtaa wa Paradise, maridadi na ji mwema.

2. **UONGOZI WA KATA**
   Kata ya Majengo inao uongozi kama ifuatavyo:-
   I. Ndugu Willy P. Mbogo –Mheshimiwa diwani wa kata –CCM
   II. Ndugu Caritas MAngwangwa –Mhe. Diwani viti maalum –CCM
   III. Ndugu Rhoda Mwakalenge –Mhe. Diwani viti maalum- CCM
   IV. Ndugu Stanslaus Lwambusha Mhe.Mwenyekiti wa Mtaa Mjimwema
   V. Ndugu Donatha Mpandangazi Mhe. Mwenyekiti mtaa wa Mridadi
   VI. Ndugu Margreth A. Kisanga Kaimu Mwenyekiti mtaa wa Paradise

Aidha mtaa wa paradise hauna mwenyekiti kutokana na dosari za uchaguzi zilizo jitokeza wakati wa uchaguzi bali unakaimiwa na mjumbe wa serikali ya mtaa.

3. **WATUMISHI WALIOPO KATIKA KATA:**
   Kata inaowatumishi wapatao 83 ambapo kati yao 41 ni walimu wa shule zilizopo katika kata 36 ni wafanyakazi wa kituo cha afya mwangaza 6 ni wataalamu katika ofisi ya kata.
4. **MIPAKA YA KATA :**
   Kata ya Majengo inayo mipaka kama ifuatavyo:-
   -Upande wa Maghaaaribi inapakana na kata ya Makanyagio
   -Upande wa Mashariki inapakana na kata ya Uwanja wa Ndege
   -Upande wa kaskazini inapakana na kata ya Kashaulili
   -Upande wa Kusini inapakana na kata ya Mpandahotel.

5. **IDADI YA WATU KATIKA KATA:-**
   Kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012 Kata ya majengo ina jumla ya kaya 1084 zenye idadi ya watu wapatao 5147 ambapo kati ya hao wanaume ni 2476 na wanawake 2671

6. **HUDUMA ZA JAMII**
   Kata ya Majengo inazo huduma mbalimbali za kijamii kama vile shule ambazo ziko mbili,soko moja benki ya CRDB 1, Maduka ya rejareja, M-pesa, Tigo pesa, Airtel money, Sheli ya mafuta n.k

7. **SHUGHULI ZA WAKAZI KATIKA KATA:**
   Wakazi wa kata ya majengo hujishughulisha na shughuli mbalimbali zinazo wawezesha kuishi kama vile vile kilimo, ufugaji, uchimbaji wa madini , biashara, ufundi wa fani mbalimbali , watumishi wa serikali , watumishi wa kampuni na Taasisi mbalimbali.
8. **SEKTA YA MAEDELEO YA JAMII JINSIA NA WATOTO**.

   Kata ina mtaalam wa sekta ya maendeleo ya jamii anayeratibu shughuli hizo. Katika kipindi cha mwezi Julai hadi Septemba 2018 sekta ya maendeleo ya jamii imefanya shughuli zifuatazo :-

I. Kuendelea kutoa elimu ya kujenga uwezo kwa vikundi vya wajasiliamali vilivyopo katika kata.
II. Kuendelea kusimamia uundaji wa vikundi vipya vya wajasiliamali.
III. Kuendelea Kusimamia upatikanaji wa mikopo kwa vikundi vilivyopo katika kata.
IV. Kutoa elimu ya ujasiliamali kwa vikundi vilivyopata mkopo.
V. Kufuatilia marejesho kwa vikundi vilivyopata mikopo.

## 9. SEKTA YA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI

Ofisi ya Kata ya Majengo inasimamia pia sekta ya kilimo na mifugo ambapo katika kipindi cha Julai hadi Septemba 2018 shughuli zifuatazo zimefanyika.

I. Kuendelea kutoa hamasa ya kilimo cha mazao ya bustani, juu ya matumizi sahihi ya mbegu bora zenye tija na matumizi sahihi ya viwatilifu na matumizi sahihi ya mbolea ili kuongeza kipato na kuboresha maisha.
II. Kuendelea kuutoa elimu juu ya ufugaji bora wa mifugo mbalimbali
III. Kutoa elimu ya utunzaji wa chakula kwa wananchi ili kujikinga na balaa la njaa.
IV. Kutoa elimu ya maandalizi ya kilimo cha msimu wa 2018/2019.
V. Kuhamasisha kilimo cha zao la Pamba na korosho.

## 10. SEKTA YA AFYA.

### 1) AFYA KINGA

Ofisi ya kata kwa kushirikiana na wataalamu na kamati za serikali za mitaa huratibu na kusimamia usafi wa mazingira kwa kudhibiti uchafu katika kata ambapo katika kipindi hiki cha Julai hadi Septemba 2018 kazi zifuatazo zimefanyika:-

1. Kuendelea kutoa elimu ya afya kinga kwa kuishauri jamii juu ya usafi wa mazingira katika maeneo ya kuishi na biashara
2. Kusimamia vikundi kazi vya uzoaji wa taka ngumu mitaani na kuzipeleka Dampo kuu kwa kutumia lory la manispaa.
3. Kufuatilia ulipaji tozo za taka
4. Kukagua mazingira mara kwa mara na kuhakikisha kuwa maeneo yote ya kata yanakuwa safi.

### 2) AFYA TIBA

Kata ya majengo inayo bahati ya kuwa na kituo cha afya katika kata kinachoitwa Kituo cha afya Mwangaza au Town Clinic ambapo wakazi kata hupata huduma za afya katika kituo hicho na wengine hupata huduma za afya katika hospitali kubwa ya Manispaa na katika zahanati za watu binafsi. Aidha kituo cha afya kina wodi ya wazazi ambayo inasaidia sana kwa huduma ya uzazi kwa akina mama wa kata hii pamoja na Manispaa kwa ujumla.

## 11. SEKTA YA ELIMU

Kata ya Majengo ina shule mbili (2) za msingi ambazo ni shule ya msingi Majengo na shule ya msingi Azimio. Kata hii ina haina shule ya sekondari kutokana na jiografia ya kata.

### I. IDADI YA WANAFUNZI

| NA. | SHULE | WAV | WAS | JUMLA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Azimio | 392 | 374 | 726 |
| | (Azimio maalum) | 11 | 10 | 21 |
| 2 | majengo | 605 | 983 | 1389 |

## II. IDADI YA WALIMU WALIOPO

| NA | SHULE | KABLA YA UHAKIKI | | | BAADA YA UHAKIKI | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | ME | KE | JUMLA | ME | KE | JUMLA |
| 1 | Azimio | 11 | 17 | 28 | 9 | 15 | 24 |
| 2 | Majengo | 6 | 12 | 18 | 5 | 12 | 17 |
| | | 17 | 29 | 46 | 14 | 27 | 41 |

## III. MATOKEO YA DARASA LA 1V 2017

| | shule | waliandikishwa | | | waliosajiliwa | | | Walifanya mtihani | | | waliofaulu | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | WAV | WAS | JML | WAV | WAS | JML | WAV | WAS | JML | WAV | WAS | JML |
| 1 | Azimio | 49 | 52 | 101 | 43 | 37 | 80 | 39 | 36 | 75 | 39 | 36 | 75 |
| 2 | Majengo | 20 | 46 | 66 | 39 | 34 | 73 | 36 | 34 | 80 | 36 | 34 | 70 |
| | Jumla | 69 | 98 | 167 | 82 | 71 | 153 | 75 | 70 | 155 | 75 | 70 | 145 |

### IV. MATOKEO YA DARASA LA VII 2017

| | Shule | Walioandikishwa | | | Waliosajiliwa | | | Waliofanya mtihani | | | Waliofaulu | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | WAV | WAS | JML | WAV | WAS | JML | WAV | WAS | JML | WAV | WAS | JML |
| 1 | Azimio | 36 | 47 | 83 | 45 | 51 | 96 | 44 | 49 | 93 | 43 | 42 | 85 |
| 2 | Majengo | 34 | 30 | 64 | 29 | 45 | 74 | 29 | 44 | 73 | 28 | 42 | 70 |
| | Jumla | 70 | 77 | 147 | 74 | 96 | 170 | 73 | 93 | 166 | 71 | 84 | 155 |

## V. UANDIKISHAJI WA DARASA LA AWALI NA DARASA LA KWANZA

| | SHULE | AWALI | | | DARASA LA I | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | WAV | WAS | JML | WAV | WAS | JML |
| 1 | Azimio | 24 | 29 | 53 | 46 | 45 | 91 |
| 2 | Majengo | 10 | 10 | 20 | 16 | 33 | 49 |
| | Jml Kikata | 34 | 39 | 73 | 62 | 78 | 140 |

### VI. MADAWATI, MADARASA OFISI NA VYOO NYUMBA ZA WALIMU

| | SHULE | AZIMIO | | | MAJENGO | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | mahitaji | yaliyopo | pungufu | mahitaji | yaliyopo | pungufu |
| 1 | Madawati | 245 | 250 | - | 214 | 240 | - |
| 2 | madarasa | 17 | 12 | 5 | 15 | 8 | 7 |
| 3 | Ofisi | 4 | 2 | 2 | 4 | 3 | 1 |
| 4 | vyoo | 29 | 6 | 23 | 30 | 4 | 26 |
| 5 | Nyumba za walimu | 24 | 2 | 22 | 17 | 1 | 16 |

Aidha maudhurio ya wanafunzi ni mazuri na hatuna watoro wala mimba za wanafunzi katika kipindi chote cha Julai hadi Septemba 2018.

## 12. SEKTA YA MAJI

Hali ya maji katika kata ya Majengo ni wastani. Kata inakabiliwa na changamoto kubwa ya uhaba wa maji kwani wakazi ni wengi kuliko huduma ya maji inayopatikana. Wakazi wa kata hii hupata maji katika visima 3 vilivyopo katika kata ambapo katika visima hivyo 2 ni vya watu binafsi na kimoja ndiyo cha serikali. Pia wakazi wa kata hii hutumia maji ya bomba maji ambapo hupatikana kwa mgawo kwa kufuata ratiba ya Idara ya

Maji. Maji haya hupatikana kwa shida kwani mgawo wake hauzingatii ratiba ilivyopangwa na huleta usumbufu mkubwa kwa wananchi.

**13. SEKTA YA BARABARA**

Hali ya barabara katika kata ya majengo ni nzuri kwani sehemu kubwa ni barabara za lami.

Changamoto katika barabara za kata hii ni mitaro kwani baadhi ya barabara hazijajengewa mitaro, Aidha ipo mitaro ambayo haipitishi maji kutoka na kalavati zake kuziba.

**14. ULINZI NA USALAMA**

Hali ya ulinzi na usalama katika kata ya majengo ni ya wastani. Katika kipindi cha kuanzia Julai hadi Septemba 2018 hakuna tukio lolote la ajabu lilijitokeza hivyo Kata imeendelea kuweka mikakati ya kujilinda na mali zake.

**15. HALI YA MAJANGA**

Katika kipindi cha mwaka 2018 kuanzia Julai hadi Septemba hakuna janga lolote lililotokea katika kata .

**16. UZALENDO NA UTAIFA**

Katika kipindi cha mwaka 2017 Kata ya Majengo iliwapeleka vijana kadhaa kwenda kujiunga na jeshi la kujenga Taifa (JKT) kwa ajili ya kuendeleza dhana ya ujenzi wa Taifa letu. Tunayo matumaini kuwa Kata ya Majengo inao uzalendo wa kutosha kwa Taifa lake.

**17. UTAWALA BORA.**

Ofisi ya kata ya majengo inaendeshwa kwa kufuata kanuni za utawala bora. Wananchi wa kata hii hupata huduma bora kwa maafisa watendaji na wataalamu, wenyeviti na wajumbe wa mtaa pamoja na waheshimiwa madiwani waliopo. Kila jambo linaendeshwa kwa ufinisi ikiwa ni pamoja na mapato na matumizi kusomwa katika vikao na mikutano ya hadhara. Katika kipindi cha mwezi Julai hadi Septemba 2018 vikao 2 vimefanyika katika kata ambapo 1 ni cha kikanuni na 1 ni kikao maalumu (dharula). Pia mikutano maalumu miwili (2)

Aidha vikao na mikutano iliyofanyika katika mitaa ni kama ifuatavyo:-

- Mtaa wa paradise vikao 3 na mkutano 1.
- Mtaa wa Maridadi vikao 3 na mkutano 1.
- Mtaa wa mji mwema vikao 3 na mkutano 1.

**18. UKIMWI NA MALARIA**

Kata ya majengo inapambana na kujikinga na maambukizi mapya ya virusi vya UKIMWI na Malaria kwa kusaidiana na kamati ya kudhibiti UKIMWI ya kata na **NG'O** mbalimbali kama ile Shidepha$^{+}$, Kizazi Kipya n.k. Kamati hii hufanya vikao na kuratibu namna ya kupambana na magonjwa haya hatari na kutoa elimu juu ya maambukizi ya VVU na Malaria katika kata. Katika kipindi cha Julai hadi Septemba Kata imefanya kikao cha robo na kuazimia mikakati mbalimbali na kuitekeleza kama vile kukagua nyumba za kulala wageni ili kuhakikisha kama wanatumia mipira aina ya Kondom na vyandarua kwa ajili ya kujikinga na maambukizi na kutoaa elimu katika maeneo mengi hatarishi yanayo sababisha maambukizi.

**19. MAPATO NA MATUMIZI**

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2018/2019 Kata imekisia kukusanya kiasi cha **899,597,369.36** katika vyanzo mbalimbali vya mapato kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mabalimbali za maendeleo ambapo katika kipindi hiki cha Julai hadi Septemba **2018** Kata imekusanya kiasi cha **Tshs. 25976080.92** ambayo ni sawa na **2.84%** ya

makadilio yake na kutumia kiasi cha Tsh. **16,225,925/=** na kubakiwa na **9,750,155.92** kwa mchanganuo uliopo katika jedwali lifuatalo:-

| **Na.** | **MAHALI ULIPO MRADI** | **AINA YA MRADI** | **GHARAMA ZA MRADI** | **CHANZO CHA FEDHA** | **FEDHA** | | | | **HATUA YA UTEKELEZAJI** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kata | mtaa | | | | Mapato | matumizi | salio | |
| 1 | Majengo | Paradise Maridadi Mji mwema | | -------- | Salio katika akaunti | 8,672,353/= | | 8,672,353/= | Ni salio katika akaunti |
| 2 | | Mji mwema | Ujenzi wa matundu 8 ya vyoo S/M majengo | **12,00,000/=** | -Mapato ya ndani ya H/manispaa. -Mfuko wa jumla -Nguvu za wananchi | 2,722,364/= 2,368,000/= 1,195,000/= | 6118,000/= | 167,364/= | Mradi uko hatua ya uchimbaji shimo |
| 3 | Majengo | S/M majengo | Uendeshaji wa shule | -------- | captation | 1431236.46 | 800,000/= | 631236.46 | Fedha zilitumika kuendeshea mitihani ,posho za madaraka, Photocopy n.k. |
| 4 | Majengo | S/M Azimio | Uendeshaji wa shule | -------- | | 3,401,127.66 | 3,254,925/= | 146,202.66 | Fedha zilitumika kuendeshea mitihani,posho za madaraka, Photocopy n.k. |
| 5 | Majengo | Paradise | Tozo za ta | -------- | Wananchi (jamii) | 1,491,000/= | 1,358,200/= | 132,800/= | Kulipa vibarua, Photocopy,posho za wajumbe nk. |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 6 | Majengo | Mji mwema | Tozo za taka | -------- | Wananchi (jamii) | 2,371,000/= | 2371,000/= | -------- | Kulipa vibarua, Photocopy,posho za wajumbe nk. |
| 7 | Majengo | Maridadi | Tozo za taka | -------- | Wananchi (jamii) | 2,324,000/= | 2,323,800/= | 200/= | Kulipa vibarua, Photocopy,posho za wajumbe nk. |
| | | | | | | **25976080.92** | **16,225,925/=** | **9750155.92** | |

**MCHANGANUO WA MAPATO NA MATUMIZI KATIKA KIPINDI CHA MWAKA 2018/2019 KUANZIA JULAI HADI SEPTEMBA 2018**

**CHANGAMOTO ZINAZO KABILI KATA NA UTATUZI WAKE.**

| NA | AINA YA CHANGAMOTO | UTATUZI WAKE |
|---|---|---|
| | **A: CHANGAMOTO ZA SEKTA YA AFYA.** | Elimu inaendelea kutolewa na wanaokaidi wanachukuliwa hatua za kisheria. |
| **1.** | Baadhi ya wananchi kutofanya usafi wa mazingira kwa hiari. | |
| 2. | Kata kuwa na viwanja na mapagara yanayosababisha uchafu (visivyoendelezwa) ambayo wamiliki wako nje ya kata na wengine hawajulikani. | Tumeweka mkakati wa kuwafuatilia na kuwashughulikia na kuanza kutekeleza mkakati huo. |
| 3. | Kata kuwa na maeneo mengi ya wazi ambapo baadhi ya wananchi wasio waelewa huyatumia vibaya kutupia taka hasa wakati wa usiku. | Tumeweka mkakati wa kushughulikia maeneo hayo na kuanza kutekeleza mkakati huo kwa kutumia vikundi kazi kuyasafisha mara kwa mara pia kila jumamosi ya mwisho wa mwezi. |
| 4 | Upungufu wa malori ya kuzolea taka. | Ni jukumu lililo juu ya uwezo wetu |
| | **B: CHANGAMOTO ZA SEKTA YA ELIMU.** | Ofisi ya kata imeanzisha ujenzi wa |

| | | |
|---|---|---|
| | Upungufu wa matundu ya vyoo. | matundu 8 ya vyoo ili kupunguza changamoto hiyo kwa kutumia michango ya wananchi na fedha za luzuku ya mapato ya ndani ya Halmashauri ya Manispaaa ambapo maboma yalishakamilika na hivi mradi uko hatua ya kuchiomba shimo la choo. |
| | Upungufu wa vyumba vya madarasa. | Ofisi ya kata imeanza kutatua changamoto hii kwa kuanza na mkakati wa ujenzi wa vyumba 4 vya madarasa ambapo vikao na mkutano vilishaanza kufanyika na ili kuweka mikakati ya ujenzi. |
| | Upungufu wa nyumba za walimu. | Bado hatujaanza. |
| | CHANGAMOTO ZA SEKTA YA MAJI. | |
| | Uhaba wa visima vya maji ya kunywa. | Ni changamoto iliyo juu ya uwezo wetutulishatoa taarifa katika ofisi ya mkurugenzi. |
| | Uhaba wa maji ya bomba ambayo hupatikana kwa mgawo huwa haufuati ratiba. | Ni changamoto iliyo juu ya uwezo wetu na kuhusu ratiba ya mgawo tulishafikisha taarifa katika ofisi husika kwa msaada zaidi. |
| | D: CHANGAMOTO ZA BARABARA. | |
| | Kuziba kwa baadhi ya mitaro na baadhi ya calvates. | Utatuzi umefanyika kwa kuzibua mitaro inayowezekana pia kutoa taarifa TARULA kwa hatua zaidi. |
| | Baadhi ya barabara kutojengwa mitaro. | Ni changamoto iliyo juu ya uwezo wetu na tulisha ifikisha TARULA kwa hatua zaidi. |
| | E: CHANGAMOTO ZA UTAWALA BORA. | |
| | Ukosefu wa ofisi ya Kata na mitaa. | Tulishaanza mchakato wa kutafuta kiwanja baada ya kubaini kuwa hatuna eneo lengwa kwaajili ya kujengea ofisi. |
| | Wananchi wengi kutokujua sheria. | Tunatoa elimu ili kuwawezesha wananchi kujua sheria. |

| | | |
|---|---|---|
| | Ukosefu wa usafiri - ofisi ya kata inamajukumu mengi ambayo ili yatelezwe kwa ufanisi usafiri unahitajika. | Ni changamoto iliyojuu ya uwezo wetu hivyo tumeiripoti katika ofisi ya mkurugenzi wa Manispaa kwa ufumbuzi zaidi. |
| | Ufinyu wa bajeti ya uendeshaji wa ofisi ya kata na mitaa. | Ni changamoto iliyo juu ya uwezo wetu hivyo tumeripoti katika ofisi ya mkurugenzi wa Manispaa kwa ufumbuzi zaidi. |

Naomba kuwasilisha

WILLY P. MBOGO.

MH: DIWANI KATA YA MAJENGO

**KATA YA MAKANYAGIO**

## TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2018-2019 KWA KIPINDI CHA ROBO YA KWANZA JULAI – SEPTEMBA 2018

### UTANGULIZI.

1. Kata ya Makanyagio inaundwa na mitaa mitano **(5)** ambayo ni **Makanyagio, Kigoma, Kachoma, Mwangaza** na **Mpadeco** na ni miongoni mwa Kata **9** zinazounda tarafa ya Kashaulili katika Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda Mkoa wa Katavi.
2. Kata ya Makanyagio ina jumla ya kaya **3048** zenye jumla ya wakazi wapatao **15823** kati yao wanaume **6,325** na wanawake **9498**.
3. Kata ya Makanyagio ina jumla ya Shule **2** za Msingi na **2** za Sekondari, na Zahanati **1** ya mtu binafisi.

### MIPAKA YA KATA.

- Makanyagio kwa upande wa mashariki imepakana na Kata ya Kashaulili
- Upande wa kusini imepakana na Kata ya Majengo na M/Hotel.
- Upande wa magharibi imepakana na Kata ya Misunkumilo
- Upande wa kaskazini imepakana na Kata ya shanwe.

### MCHANGANUO WA WAKAZI

| KAYA | IDADI YA WATU | | | WENYE UWEZO WA KAZI | | | WASIO NA UWEZO WA KAZI | | | WALEMAVU | | | WATOTO UMRI 0- 17 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML |
| 3048 | 6325 | 9498 | 15823 | 5870 | 8806 | 14676 | 458 | 689 | 1147 | 5 | 10 | 15 | 2385 | 3569 | 5954 |

### SHUGHULI ZA KIUCHUMI.

- Wananchi wa Kata ya Makanyagio wanajishughulisha na biashara kubwa na ndogo (wajasiriamali). Vilevile wanajishughulisha na kilimo cha mazao ya chakula kama vile **mpunga, mahindi** na **karanga** shughuli hizo hufanyika nje ya Kata kama **Kasokola, Kakese, Kabungu** n.k

### IDADI YA WATUMISHI KATA YA MAKANYAGIO.

| UTAWALA | | ELIMU YA MSINGI | | ELIMU YA SEKONDARI | | KILIMO NA MIFUGO | | AFYA | | MAENDELEO YA JAMII | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| ME | KE | ME | KE | ME | KE | ME | KE | ME | KE | ME | KE |
| 1 | 3 | 15 | 28 | 30 | 16 | - | 2 | 1 | - | - | 1 |

### HUDUMA ZA JAMII ZILIZOPO

Kata ya Makanyagio inahuduma za kijamii zinazomilikiwa na Serilikali, Makapuni na watu Binasi

**A. ELIMU**

- Shule za msingi 2 Kashato na Katavi
- Shule za sekondari 2 Mwangaza na Istiqama
-

**B. HUDUMA ZA MAWASILIANO**

Minara ya kunasia mawasiliano:-

- Voda minara 2
- Hallotel mnara 1
- Barabara

**SHUGHULI ZINAZOFANYWA NA SEKTA YA MAENDELEO YA JAMII**

- Kuelimisha na kuhamasisha jamii kuunda vikundi vya wakina mama na vijana kufanya shughuli za ujasiriamali kupitia kilimo na ufugaji
- Kutoa elimu juu ya kukopa na kufuatilia urejeshaji wa mikopo kwa vikundi
- Vikundi vimeundwa na vinaendelea kukopa na kurejesha mikopo
- Vilevile kuhamasisha wadau mbalimbali kuchangia na kusaidia shughuli za maendeleo na makundi maalumu ya wasiojiweza katika kuimalisha ubora wa huduma za kijamii

A: **KILIMO**

- Takwimu za wakulima na wafugaji zimekusanywa katika mitaa yote kwa lengo la kuhuisha daftari la wakulima.
- ushauri na elimu imeendelea kutolewa kwa wanakikundi cha **TASAF (23)** kuhusiana na shamba darasa la Bustani mfuko kwa mazao ya mbogamboga na kilimo cha uyoga.
- Elimu imetolewa kwa wakulima juu ya kilimo cha korosho na pamba kwa msimu wa kilimo **2018/2019**.
- Wakulima 16 wanaojishughulisha na kilimo cha mbogamboga wamepewa ushauri wa kilimo juu ya matumizi bora ya pembejeo hususani viwatilifu.

B: **MIFUGO**

- Jumla ya ng'ombe **41** wamepatiwa chanjo dhidi ya ugonjwa wa mapafu (CBPP)
- Ukaguzi wa nyama umefanyika ambapo jumla ya nguruwe 42 walichinjwa na kukaguliwa na Afisa ugani.
- Mifugo iliyopo mpaka sasa katika Kata ya Makanyagio:

**SENSA YA MIFUGO**

| AINA YA MIFUGO | NG'OMBE | MBUZI | KONDOO | NGURUWE | MBWA | KUKU |
|---|---|---|---|---|---|---|
| IDADI YA MIFUGO | 43 | 58 | 07 | 31 | 83 | 1013 |

**TAARIFA ZA SEKTA YA ELIMU.**

**Idadi ya wanafunzi katika shule za msingi na sekondari**

| SHULE | WALIMU | | | WANAFUNZI | | | MADARASA | | | MADAWATI | | | VYOO | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | ME | KE | JML | ME | KE | JML | MAH | YAP | PUNG | MAH | YAP | PUNG | MAH | YAP | PUNG |
| KASHATO | 86 | 15 | 21 | 572 | 558 | 1130 | 31 | 9 | 22 | 329 | 309 | 30 | 18 | 18 | - |
| KATAVI | 6 | 15 | 21 | 782 | 776 | 1558 | 38 | 9 | 29 | 460 | 460 | 0 | 28 | 7 | 21 |
| MWANGAZA | 21 | 14 | 35 | 511 | 444 | 955 | 24 | 16 | 9 | 948 | 799 | 142 | 20 | 9 | 11 |
| ISTIQAMA | 9 | 2 | 11 | 36 | 34 | 70 | 4 | 5 | - | - | - | - | 5 | 5 | - |

**WANAFUNZI WA ELIMU MAALUMU SHULE YA MSINGI KASHATO**

| S/N | WAVULANA | WASICHANA | JUMLA |
|---|---|---|---|
| 1 | 15 | 10 | 25 |

**DARASA LA AWALI SHULE YA MSINGI KASHATO NA KATAVI**

| SHULE | WALIOANDIKISHWA | | |
|---|---|---|---|
| | WV | WS | JML |
| KASHATO | 77 | 68 | 145 |
| KATAVI | 89 | 90 | 179 |

**TAARIFA ZA MAPATO YA FEDHA ZA RUZUKU SHULE ZA MSINGI NA SEKONDARI ROBO YA KWANZA YA MWAKA JULAI – SEPTEMBA 2018**

| SHULE | JULAI | MAY | SEPTEMBA |
|---|---|---|---|
| KASHATO | 888,336.92 | 888,336.92 | 2,665,010.76 |
| KATAVI | 648,675.17 | 648,675.17 | 1,946,025.51 |
| MWANGAZA | 883,366/= | 883,366/= | 2,650,098/= |

**SEKTA YA AFYA**

**HUDUMA ZINAZOTOLEWA NA SEKTA YA AFYA.**

1. Kuelimisha jamii katika shughuli za usafi wa mazingira kwa kila kaya na kujikinga na mbu waenezao malaria kwa kutumia chandaruwa kwa muda wote.

2. Kuhakikisha kila kaya inakuwa na choo safi na bora na kukitumia.

3. Kutoa elimu ya kuchemsha maji ya kunywa na kunawa na sabuni kipindi wanapotoka chooni na wanapotaka kula chakula.

4. Kuhakikisha taka ngumu zinazolewa na kupekwa kwenye Dampo kuu.

5. Kukagua biashara zote na ziwe kwenye ubora unaoridhisha kwa muda wote.

6. Kuhakikisha watoa huduma za vyakula wanapima afya zao kabla ya kuanza biashara.

7. Kutoa elimu dhidi ya kujikinga maambukizi mapya ya UKIMWI (VVU).

**ULINZI NA USALAMA**

Katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka Julai hadi Septemba 2018 hakuna matukio ya uharifu yaliyojitokeza.

**TATIZO LA VIBOKO**

Viboko kuzurula mitaani na kutishia usalama wa wananchi hivyo kamati ya ulinzi na usalama ya Kata kutoa taarifa kuangalia utaratibu wa kuondosha viboko hao wanaotoka bwawa la Milala.

**MAKISIO YA MAPATO NA MATUMIZI 2018/2019**

***i.*** **MAKISIO YA MAPATO**

Katika mwaka wa fedha Julai 2018 hadi Juni 2019 Kata imekisia kukusanya na kupokea kiasi cha Tshs. **237,336,537/=** kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo.

***ii.*** **MAPATO**

Katika kipindi cha Mwezi Julai hadi Septemba 2018, Kata kupitia vyanzo mbalimbali vya mapato imeweza kukusanya na kupokea jumla ya Tshs. **101,809,134.27**

***iii.*** **MATUMIZI**

Katika kipindi cha Julai hadi Septemba 2018, Kata imeweza kutumia jumya ya Tshs. **78,809,134.27** katika kutekeleza shughuli mbalimbali za maendeleo.

**MCHANGANUO WA MATUMIZI KATIKA KIPINDI CHA MWEZI JULAI-SEPTEMBA 2018**

- Uendeshaji wa taaluma (capitation) shule za msingi Kashato na Katavi Tshs. **6,611,036.27/=**
- Uendeshaji wa taaluma (capitation) shule ya Sekondari Mwangaza Tshs. **2,650,098.00/=**
- Umaliziaji wa vyumba vya madarasa 3 Mwangaza Sekondari Tshs.**50,000,000.00/=**
- Umaliziaji wa maabara Mwangaza sekondari Tshs. **17,000,000/=**
- Uondoshaji wa taka ngumu kupeleka dampo kuu Tshs. **1,200,000/=**
- malipo ya kaya zilizo kwenye mpango wa Tasaf III Tshs. **1,348,000/=**

**Jumla Kuu ya matumizi yote ni Tshs. 78,809,134.27/=**

**VIKAO VILIVYOFANYIKA VYA MTAA NA KATA**

| **NA** | **KATA/MTAA** | **IDADI YA VIKAO** | | | **MIKUTANO MIKUU** | | | **KAMATI YA MAZINGIRA** | | | **KAMATI YA MALALAMIKO** | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | hitajika | fanyika | % | Hitajika | fanyika | % | hitajika | Fanyika | % | hitajika | fanyika | % |
| 1 | Kata (WDC) | 4 | 1 | | 4 | 1 | | 4 | 1 | | 4 | 1 | |
| 2 | Makanyagio | 12 | 1 | | 4 | 1 | | 4 | 1 | | 4 | 1 | |
| 3 | Kigoma | 12 | 1 | | 4 | 1 | | 4 | 1 | | 4 | 1 | |
| 4 | Kachoma | 12 | 1 | | 4 | 1 | | 4 | 1 | | 4 | 1 | |
| 5 | Mwangaza | 12 | 1 | | 4 | 2 | | 4 | 1 | | 4 | 1 | |
| 6 | Mpadeco | 12 | 1 | | 4 | 1 | | 4 | 1 | | 4 | 1 | |

## MCHANGANUO WA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA ZA MIRADI KWA KIPINDI CHA JULAI – SEPTEMBA 2018

| KATA | MTAA | AINA YA MRADI | CHANZO CHA FEDHA | ILIYOPOKELEWA | ILIYOTUMIKA | ILIYOBAKI | HATUA YA UTEKELEZAJI | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| MAKANYAGIO | Kachoma | Mpango wa kunusuru kaya masikini | TASAF III | 1,348,000/= | 1,348,000/= | - | Walengwa wote wamelipwa | |
| | Shule ya msingi Kashato na Katavi | Uendeshaji wa shughuli za taaluma (Captation) | Halmashauri ya manispaa | 6,611,036.27 | 6,611,036.27 | - | Taaluma imeboreka | |
| | Mwangaza Sekondari | Uendeshaji wa shughuli za taaluma (Captation) | Halmashauri ya Manispaa | 2,650,098/= | 2,650,098 | - | Taaluma imeboreka | |
| | Mitaa 2 Kigoma na Mpadeco | Uzoaji taka ngumu | Michango ya Wananchi | 1,200,000/= | 1,200,000/= | - | Taka zinasombwa Trip 8 | |
| | Mitaa 5 | Umaliziaji wa vyumba 3 madarasa Mwangaza Secondari | Msaada wa nchi ya Uholanzi | 60,000,000/= | 50,000,000/= | 10,000,000/= | Umaliziaji | |
| | Mitaa 5 | Umaliziaji wa maabara Mwangaza Sekondari | P4R | 17,000,000/= | 17,000,000/= | - | Umaliziaji unaendelea | |
| | | **JUMLA KUU** | **TSHS** | **88,809,134.27** | **78,809,134.27** | 10,000,000/= | | |

## 1. MIRADI INAYOENDELEA KWA SASA

A. Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa shule ya Msingi Kashato
   Hatua za ujenzi michango inaendelea kukusanywa kwa wananchi na wahisani mbalimbali
B. Umaliziaji wa madarasa 2 Shule ya msingi Katavi – Hatua iliyofikia Boma limekamilika.
C. Umaliziaji wa vyumba 3 vya madarasa Mwangaza Sekondari.

**CHANGAMOTO**

- Ubovu wa barabara uliyosababishwa na mvua tunaioba mamlaka husika kukagua na kutengeneza barabara zote zilizoharibika.

- Tishio la viboko wanaozurula ovyo mtaa wa Kachoma na Kigoma mamlaka husika vilevile kuondoa viboko hao.

- Gari la Taka kutomudu kuondosha taka mtaani na kupelekea taka kuzagaa maeneo ya (Kaya) zinapohifadhiwa kabla ya kuondolewa.

- Kucheleweshwa kwa Posho za wenyeviti na wajumbe wa serikali za mitaa kunapelekea ugumu wa utekelezaji wa baadhi ya majukumu mbalimbali.

**MH. MSTAHIKI MEYA NAOMBA KUWASILISHA.**

**……………………**
**MH. DIWANI KATA YA**
**MAKANYAGIO**

## KATA YA MAGAMBA

### TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA MAENDELEO KWA KATA YA MAGAMBA ROBO YA KWANZA KUANZIA MWEZI WA 07/2018 HADI MWEZI WA 09/2018

**UTANGULIZI**

Kata ya magamba ni miongoni mwa kata zinazounda Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda, vijiji vya kata hii ya Magamba ni

1. Magamba
2. Mtakumbuka
3. Makongoro
4. Society
5. Dirifu

**Idadi ya wakazi**

Kata ya Magamba ina wakazi 7864 Me 4044 na Ke 3820 na ina kaya 1479 kwa mujibu wa sense ya mwaka 2012.

**Mipaka ya kata idadi ya vijiji,vitongoji na wakazi wake**

i. **Mipaka ya kata**

Upande wa Kaskazini inapakana na kata ya Ilembo, upande wa kaskazini Magharibi inapakana na kata ya Misunkumilo, na Magharibi inapakana na kata ya Itenka, upande wa Kusini inapakana na kata ya Machimboni upande wa mashariki Stalike inapakana na kata ya Kapalala upande wa kaskazini mashariki inapakana na kata ya Mtapenda na uwanja wa ndege.

ii. **Idadi ya vijiji na Vitongoji kata na Tarafa**

| KATA | KIJIJI | KITONGOJI |
|---|---|---|
| **MAGAMBA** | MAGAMBA | • Migazini |
| | | • Ntakata |
| | | • New-camp |
| | | • Ikulu |
| | | • Beling |
| | | • Burunga |
| | MTAKUMBUKA | • Kabatini |
| | | • Igonda |
| | | • Mtakumbuka kati |
| | | • Mkakumbuka kusini |

| | | |
|---|---|---|
| | | • Mtakumbuka kaskazini |
| | | • Mtakumbuka mashariki |
| | MAKONGORO | • Mailikumi |
| | | • Igalukilo |
| | | • Makongoro |
| | | • Kanondo |
| | | • Mlimani |
| | SOCIETY | • Njia panda |
| | | • Mwenge |
| | | • Ikulu |
| | | • Society |
| | | • Mafuanguo |
| | DIRIFU | • Msangama |
| | | • Kagela |
| | | • Kamsofu |
| | | • Ikulo |
| | | • Mkuyuni |
| | | • Lumuka |
| | **JUMLA YA VIJIJI 5** | **VITONGOJI 28** |

### iii. Idadi ya Ofisi za vijiji, Kata na Tarafa

| **IKAMA** | **KATA** | **KIJIJI** | **TARAFA** |
|---|---|---|---|
| MAHITAJI | 1 | 5 | 1 |
| ZILIZOPO | 0 | 3 | 1 |
| PUNGUFU | 1 | 2 | - |
| ZIADA | - | - | - |

### iv. Uongozi wa kata na vijiji

- Mh diwani wa kata (1)
- Afisa mtendaji wa kata (0)
- Maafisa kilimo na mifugo (3)
- Wenyeviti wa vijiji (3)
- Watendaji wa vijiji (2)

**Idadi ya watumishi, sekta mbalimbali ngazi ya kata**

| IKAMA | UTAWALA | ELIMU YA MSINGI | ELIMU YA SEKONDARI | ULINZI NA USALAMA | MAENDELEO YA JAMII | AFYA | KILIMO |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mahitaji | 6 | 50 | 20 | 4 | 6 | 16 | 6 |
| Waliopo | 2 | 36 | 16 | 2 | - | 6 | 3 |
| Pungufu | 4 | 14 | 4 | 2 | 6 | 10 | 3 |
| Ziada | - | - | - | - | - | - | - |

**v. Shughuli za Kiuchumi**

- Kilimo cha jembe la mkono
- Biashara ndogondogo
- Ufugaji mdogomdogo
- Uchimbaji wa madini aina ya Dhahabu

**B.TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KATIKA KATA**

**I. Taarifa ya fedha (mapato na matumizi)**

Katika kipindi cha robo ya kwanza mwezi wa 07/2018 hadi 09/2018 kata haijapokea fedha kutoka halmashauri .

- **Utekelezaji Wa Miradi**

Ofisi ya kata katika robo ya kwanza imeendelea kukumalizia miradi viporo iliyopo katika kata kama ujenzi wa nyumba moja ya mwalimu S/m Magamba na Matundu 14 ya vyoo S/m Magamba. Aidha kata ya Magamba imeendelea kukusanya michango mbalimbali kama fedha na tofari kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya madarasa mawili (2) Shule ya Sekondari Magamba Vyoo 2 vya walimu shule ya Msingi Mtakumbuka na ofisi moja (1) ya kijiji Mtakumbuka.

Michango inaendelea mpaka sasa tofari 21500 na fedha Tsh. 500,000/= zimekusanywa

**II. Taarifa ya kilimo na mifugo**

Kata ya magamba ina jumla ya maafisa wa kilimo na mifugo 3, katika robo ya kwanza wameweza kuwatembelea wakulima 231 na wafugaji 94 na kutoa ushauri wa kuzingatia kanuni bora za kilimo na ufugaji bora wa kuleta tija.Aidha jumla ya hekari 5108.5 zimetengwa kwaajili ya shughuli za kilimo

kwa mazao mbalimbali kama mahindi, karanga, maharagwe,alizeti, pamba nk.

Pia kata imepokea mbegu za pamba kiasi cha mifuko 166 sawa na kg 830. Kama jedwali linavyoonesha hapa chini.

| **JINA LA KIJIJI** | **KIASI CHA MBEGU[IDADI YA MIFUKO]** | **KG** |
|---|---|---|
| Magamba | 50 | 250 |
| Society | 50 | 250 |
| Makongoro | 36 | 180 |
| Dirifu | - | - |
| Mtakumbuka | 30 | 150 |

Pia maafisa ugani wameweza kufanya ukaguzi wa nyama kama inavyoonesha chini ya jedwari

| **Aina ya mifugo** | **Idadi ya waliochinjwa na kukaguliwa** | **Bei ya wastani** |
|---|---|---|
| Mbuzi | 12 | 6,000/= |
| Ng'ombe | 22 | 6,000/= |
| Nguruwe | 14 | 6,000/= |

**III. Taarifa ya vikao na mikitano**

kwa kipindi cha robo ya kwanza tumefanikiwa kufanya mikutano 01 na vikao 10 sawa na asilimia 67% ya kufanikisha lengo. Kama inavyoonesha chini ya jedwari.

| **Vijiji** | **Idadi ya mikutano** | **Idadi ya vikao** |
|---|---|---|
| Mtakumbuka | 1 | 2 |
| Makongoro | - | 2 |
| Society | 1 | 2 |
| Magamba | - | 2 |
| Dirifu | - | 2 |

Pia katika robo ya kwanza tumefanikiwa kufanya kikao kimoja (1) cha kamati ya Ukimwi kata iliyokaa na kujadili Agenda nne kama ifuatavyo;-

1. Kufungua kikao
2. Uteuzi wa wajumbe wapya wa kuzuia na kupambana na maambukizi ya[**VVU**]
3. Mengineyo
4. Kufunga kikao

Kama ilivyowasilishwa katika muhtasari wa kikao kilichoketi tarehe O5/10/2018

**IV. Taarifa ya mazingira na vyanzo vya maji**

Kata ya magamba ina jumla ya jumuiya 5 za watumia maji zenye usajiri wa watumia maji. Pia katika utafiti uliofanyika robo yakwanza tumeweza kutambua uwepo wa bwawa lililopo katika kijiji cha mtakumbuka kitongoji cha kabatini abalo kwa sasa linatumika kama bwawa la kunyweshea maji mifugo mifano ng'ombe, ufutiliaji bado unaendelea kutambua chanzo na jinsi tunavyoweza kufaidika na bwawa hilo.

**V. Maendeleo ya jamii**

Tunavyo vikundi 6 vilivyosajiliwa kata ya Magamba aidha vikundi 4 vimesajiliwa kutipia Halmashauri ya Manispaa Mpanda na vijiji 2 vimesajiliwa kupitia Halmashauri ya wilaya Nsimbo. Aidha vikundi 2 vimeweza kukopeshwa na kimoja kati ya viwili hivyo kimemaliza mkopo wake

## C. TAARIFA ZINAZOHUSU HALI YA KATA

### I. ELIMU

Kata inajumla ya shule 5 za idara ya msingi na sekondari yaani shule nne za msingi na shule moja ya sekondari.

**IDADI YA WALIMU -MSINGI**

| ME | KE | JUMLA |
|---|---|---|
| 18 | 17 | 36 |

**IDADI YA WALIMU –SEKONDARI**

| ME | KE | JUMLA |
|---|---|---|
| 12 | 4 | 16 |

## MIUNDOMBINU

### VYUMBA VYA MADARASA

| SHULE | MAHITAJI | VILIVYOPO | PUNGUFU |
|---|---|---|---|
| S/M MAGAMBA | 15 | 9 | 6 |
| S/M MTAKUMBUKA | 10 | 7 | 3 |
| S/M DIRIFU | 11 | 9 | 2 |
| S/M MAKONGORO | 5 | 2 | 3 |
| MAGAMBA SEKONDARI | 16 | 8 | 8 |

### NYUMBA

| SHULE | MAHITAJI | VILIVYOPO | PUNGUFU |
|---|---|---|---|
| S/M MAGAMBA | 21 | 6 | 15 |
| S/M MTAKUMBUKA | 18 | 5 | 13 |
| S/M DIRIFU | 16 | 4 | 12 |
| S/M MAKONGORO | 11 | 1 | 10 |
| MAGAMBA SEKONDARI | 18 | 3 | 15 |

### VYOO VYA WANAFUNZI

| SHULE | MAHITAJI | VILIVYOPO | PUNGUFU |
|---|---|---|---|
| S/M MAGAMBA | 24 | 14 | 10 |
| S/M MTAKUMBUKA | 16 | 7 | 9 |
| S/M DIRIFU | 16 | 6 | 10 |
| S/M MAKONGORO | 10 | 08 | 2 |
| MAGAMBA SEKONDARI | 28 | 18 | 10 |

### VYOO VYA WALIMU

| SHULE | MAHITAJI | VILIVYOPO | PUNGUFU |
|---|---|---|---|
| S/M MAGAMBA | 2 | 2 | - |
| S/M MTAKUMBUKA | 2 | - | 2 |
| S/M DIRIFU | 2 | - | 2 |
| S/M MAKONGORO | 2 | - | 2 |
| MAGAMBA SEKONDARI | 4 | 4 | - |

### MADAWATI

| SHULE | MAHITAJI | VILIVYOPO | PUNGUFU |
|---|---|---|---|
| S/M MAGAMBA | 256 | 220 | 36 |
| S/M MTAKUMBUKA | 166 | 107 | 59 |
| S/M DIRIFU | 182 | 148 | 34 |
| S/M MAKONGORO | 96 | 64 | 32 |

**MAABARA**

| SOMO | MAHITAJI | ZILIZOPO | PUNGUFU |
|---|---|---|---|
| CHEMISTRY | 1 | 1 | - |
| BIOLOGY | 1 | 1 | - |
| PHYSICS | 1 | 1 | - |

**VIWANJA VYA MICHEZO SHULENI**

| SHULE | MAHITAJI | VILIVYOPO | PUNGUFU |
|---|---|---|---|
| S/M MAGAMBA | 5 | 2 | 3 |
| S/M MTAKUMBUKA | 5 | 1 | 4 |
| S/M DIRIFU | 5 | 2 | 3 |
| S/M MAKONGORO | 5 | 1 | 4 |
| MAGAMBA SEKONDARI | 5 | 1 | 4 |

Aidha kamati ya maendeleo ya kata inatarajia kuanzisha mradi wa madarasa mawili (2) shule ya sekondari Magamba ambapo katika vijiji 5 vinavyounda kata hiyo michango inaendelea baada ya kufuata taratibu za vikao na mikutano ya wananchi. Ujenzi unatarajia kuanza Januari **2019**.

**Utoro**

Hali ya utoro katika shule imeendelea kuwepo mpaka sasa ofisi ya kata imepokea majina ya wanafunzi **111** kutoka katika shule 2, s/m Magamba wanafunzi 98 na s/m Dirifu wanafunzi 13. taratibu zinaendelea ikiwa ni pamoja nakuwarudisha wanafunzi hao shuleni.

**II. Afya**

Tunazo Zahanati 2 zilizopo katika kijiji cha Magamba na Mtakumbuka zinazohudumia vijiji hivyo na vijiji vingine jirani.

❖ **Idadi wa watumishi wa afya na miundombinu yake**

| | MAHITAJI | WALIOPO | PUNGUFU |
|---|---|---|---|
| Watumishi | 12 | 6 | 6 |
| Nyumba | 12 | 6 | 6 |
| Vyoo | 8 | 4 | 4 |

III. **Matukio**

Kata ya magamba ina jumla ya matukio kadhaa yaliyotokea katika robo ya kwanza yafuatayo ni watukio

a. Kuanguka kwa gari la wagonjwa eneo lagetini kijiji cha magamba na mtu mmoja kupoteza maisha ktk ajali hiyo .
b. Kutokea kwa ubakaji kijana mwenye umri wa miaka 24 alimbaka bibi wa umri wa miaka 90 katika kijiji cha magamba kesi ipo mahakamani.

IV. **Ziara za Viongozi**

- 18/09/2018 Mh mstahiki meya kufanya ziara katika kata ya magamba
- 03/09 mh mbunge alifanya ziara katika kata ya magamba
- 09/Kamati ya siasa ilifanya ziara katika kata ya magamba kijiji cha mtakumbuka

V. **Ulinzi na usalama**

Kata ya Magamba inaendelea kuimalisha hali ya usalama kwani baadhi ya vijiji vimeanzisha ulinzi wao wenyewe kwa kuunda vikundi vya ulinzi shirikishi.

**Changamoto**

- Wajumbe kutohudhuria vikao vya serikari ya kijiji kwa wakati
- Uchache Watendaji wa kudumu upelekea taarifa nyingi kutowasilishwa kwa wakati
- Bei ya dawa ya mifugo na viwatilifu kuwa juu
- Ukosefu wa usafiri kwa watumishi

VI. **Utatuzi wa changamoto.**

i. Vyama vione haja ya kutoa adhabu/maelekezo kwa wenyeviti hao.
ii. Kuendelea kutoa elimu juu ya faida ya ulinzi shirikishi katika maeneo husika

**NB**

Kupitia maagizo ya mstahiki MEYA katika ziara yake tar 18//09/2018 naomba kutoa majibu kama ifuatavyo;
hakuna mwanafunzi yeyote anayefanyishwa kazi shuleni
kinyume na utaratibuwa wa muongozo wa elimu
kama ilivyolalamikiwa katika mkutano huu.

**Naomba kuwasilisha,**

**MHE.PHILIP J. KALYALYA**
**DIWANI KATA YA MAGAMBA**

## KATA YA MWAMKULU

## TAARIFA ZA ROBO YA KWANZA YA MWAKA 2018/2019 YA JULAI HADI SEPTEMBA 2018 YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA MAENDELEO NA MAPATO NA MATUMIZI

### UTANGULIZI

Kata ya Mwamkulu ni moja ya Kata zinazounda Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda, Kata hii imeundwa na Mitaa mitano, hiyo ni **Kabwaga, Mkokwa, Mkwajuni**, **Nguvumali** na **Nseso** kwa mujibu wa sensa ya **mwaka 2012** Kata hii ina kaya **1544** zenye wakazi **7277,** wakiwa wanaume **3576** na wanawake **3701.**

### HALI YA HEWA

Kwa kipindi hiki **Julai** hadi **Septemba** hali ya hewa ni nzuri na wananchi wameweza kuvuna mazao yao vizuri na tayari wameweka mazao yao gharani.

### VIKAO VYA KISHERIA

Katika Kata ya Mwamkulu kuna vikao vya kisheria vilivyofanyika kwenye Mitaa yote mitano na Kata pamoja na vikao hivyo kumefanyika mikutano ya kisheria pamoja na mikutano ya dharura kama inavyoonekana kwenye jedwali.

| S/N | MITAA | MAHITAJI | VILIVYO FANYIKA | UPUNGUFU | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Kabwaga | 3 | 3 | 0 | - |
| 2 | Mkokwa | 3 | 1 | 2 | - |
| 3 | Mkwajuni | 3 | 1 | 2 | Mtendaji mtoro kazini |
| 4 | Nguvumali | 3 | 2 | 1 | - |
| 5 | Nseso | 3 | 2 | 1 | - |

### MAENDELEO YA SHULE ZA MSINGI

Wanafunzi wa Shule ya Msingi Mwamkulu na Shule shikizi za Kabwaga, Mkokwa, Mkwajuni na Nseso zinaendelea vizuri kama zinavyoonekana kwenye jedwali.

### IDADI YA WANAFUNZI

| JINA LA SHULE | WAV | WAS | JUMLA |
|---|---|---|---|
| Mwamkulu | 675 | 615 | 1290 |
| Nseso | 49 | 53 | 102 |
| Kabwaga | 382 | 353 | 735 |
| Mkokwa | 288 | 273 | 561 |
| Mkwajuni | 103 | 90 | 193 |
| **JUMLA KUU** | **1497** | **1386** | **2881** |

**MADARASA**

| SHULE | LENGO | YALIOPO | PUNGUFU | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|
| Mwamkulu | 15 | 7 | 8 | - |
| Nseso | 5 | 2 | 3 | Madarasa mawili yapo kwenye jatua ya upauwaji |
| Kabwaga | 10 | 7 | 3 | - |
| Mkokwa | 10 | 3 | 7 | - |
| Mkwajuni | 7 | 5 | 2 | - |

Pamoja na upungufu huo wa madarasa tayari kwa shule ya Msingi Mkwajuni madarasa mawili, Ofisi na matundu matano ya vyoo yamekamilika hii ni kwa ufadhiri wa EQUIP Tanzania vilevile madarasa matatu mengine yameezekwa.hii ni kwa michago na nguvu za wananchi sambamba na shule hiyo shule ya Msingi Nseso nayo wananchi wa mtaa wa Nseso wanaendelea na michango kwa ajili ya kumalizia madarasa hayo mawili na Ofisi moja hii ni pamoja na michango inayoendelea ya kukamilisha ujenzi wa darasa moja na ofisi Shule ya Msingi Mkokwa.

**NYUMBA ZA WAALIMU**

| S/N | SHULE | LENGO | ZILIZOPO | PUNGUFU | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | KABWAGA | 7 | - | 7 | |
| 2 | MKOKWA | 7 | - | 7 | |
| 3 | MKWAJUNI | 7 | - | 7 | |
| 4 | MWAMKULU | 19 | 2 | 17 | |
| 5 | NSESO | 5 | - | 5 | |

Juhudi za ufyatuaji wa tofari na michango ya fedha zinaendelea kwa ajili ya kupunguza upungufu huo.

**WAALIMU**

| S/N | SHULE YA MSINGI | LENGO | WALIOPO | PUNGUFU | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | MWAMKULU | 19 | 13 | 6 | |
| 2 | KABWAGA | 7 | 4 | 3 | |
| 3 | MKOKWA | 7 | 3 | 4 | |
| 4 | MKWAJUNI | 6 | 1 | 5 | |
| 5 | NSESO | 6 | 1 | 5 | |

A. Pamoja na kupata waalimu hao Kata bado inaendelea na kua na waalimu wa kujitolea ambao wanalipwa na wazazi mpaka hapo upungufu huo wa waalimu utakapo kwisha.

**MADAWATI**

Katika Kata ya Mwamkulu hatuna upungufu wa madawati yapo ya kutosha changamoto ni vyumba vya madarasa.

## ELIMU YA SEKONDARI

Kata ya Mwamkulu inathamini elimu ya Shule ya Msingi na Sekondari imejiwekea mikakati ya kujenga madarasa matano ya Sekondari kila Mtaa ujenge darasa moja la Sekondari na makubaliano hayo kwa kipindi hiki ni ujenzi wa madarasa hayo kwa kukamilisha maboma tayari eneo la hekali kumi na mbili zimetengwa kwa ajili ya ujenzi huo wa shule ya Sekondari na tayari kwa kila Mtaa michango ya tofari na michango ya fedha inaendelea vizuri ili kufanikisha zoezi hilo.

## IDADI YA MIFUGO KWA KATA YA MWAMKULU

| NG'OMBE | MBUZI | KONDOO | PUNDA | NGURUWE | MBWA | PAKA | KUKU | BATA | KANGA | NJIWA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 7847 | 2017 | 357 | 35 | 39 | 701 | 260 | 19797 | 2291 | 43 | 1100 |

## KILIMO

Kwa kipindi hiki cha **Julai-Sept** wakulima wanaendelea na maandalizi ya kilimo kwa msimu huu.

## CHAMA CHA UMWAGIRIAJI

Chama hicho cha umwagiliaji kinaendelea lakini kumekuwa na baadhi ya wakulima kugoma kuchangia gunia moja kwa kila hekali la maji na shughuli za chama pia kinaendelea kuwahamasisha wakulima wenye mbuga za mpunga ndani ya Kata ya Mwamkulu waende kujisajili kwenye chama hiki ili wawe wanachama katika chama hicho.

## BIASHARA

Wakazi wa Kata hii wanaendelea na shughuli za biashara mbalimbali kama vile **vibanda, migahawa, maduka, biashara ndogondogo** vilevile kuna **mashine** za **kukoboa** na **kusaga nafakamashine za kukoboa mpunga,** biashara nyingine ni mafundi baiskeli ,biashara za vinywaji, vinyozi na biashala hizi kwa sasa zinakwenda vizuri kwa sababu ni wakati wa kiangazi.

## MAJI

Kata hii ya Mwamkulu kwa kipindi hiki cha **Julai** hadi **Sept** Serikali inaendelea kuchimba visima virefu tayari kuna visima tisa vimechimbwa baadhi havija fungiwa pampu ili vianze kutoa huduma kwakupitia kasi hii ya uchimbaji wa visima hatuna budi kuishukulu Serikali kwa kuliangalia tatizo la maji kwa macho mawili, hivyo baada ya kufungwa Pampu tatizo la maji kwa Kata hii litapungua kwa asilimia **75** kutokana na mgao wa kuchimbiwa visiwa kumi na kisima kimoja cha ahadi ya Mbunge wa Mpanda Mjini ambacho tayali kimechimbwa hivyo, Kata hiyo kua na visima kumi na moja na tayali vimechimbwa visima tisa **(9)** bado **2.**tunaiomba Serikali iendelee kuchimba visima hivyo viwili vilivyobaki ili kuondoa kabisa tatizo hili la maji kwa Kata hii ya Mwamkulu.

**HUDUMA YA AFYA**
Huduma ya Afya zinaendelea vizuri kwa zahanati ya Mwamkulu kuendelea kutoa huduma kikamilifu na kutokua na upungufu wa dawa kwa kipindi hiki cha Julai hadi Septemba shughuli zinaendelea vizuri pamoja na zahanati hii ya mwamkulu kua inaendelea kufanyakazi kwa sasa muda wowote kuanzia sasa zahanati ya Mlima kipara ambayo ipo Kata ya Mwamkulu itaanza kufanya kazi hatua zinazo endelea ni kutafuta vyumba vya kukaa waganga kwa kua mganga Mkuu tayari ameleta waganga kwa ajili ya kuanza huduma hapo zahanati ya Mlima Kipala.

**TASAF**
Kwa kipindi hiki cha robo ya kwanza ya mwaka walengwa wa TASAF wameweza kufanya mkutano na vikao kwa ajili ya kuibua miradi itakayotekelezwa kwa miezi minne kuanzia **Julai** hadi **Septemba 2018**. Miradi iliyoibuliwa ni uchimbaji wa visima, upandaji wa miti ya matunda na uchimbaji wa mabwawa. Na miradi hiyo inaendelea vizuri.

**ULINZI NA USALAMA**
Katika Kata ya Mwamkulu tumekua tukipanga vikao vya kamati ya ulinzi na usalama ya mitaa na kata pamoja na mikutano ya hadhara kwa polisi Kata na Polisi mitaa kuja kutoa elimu juu ya ulinzi shilikishi na tumekua tunamuunganiko mkubwa kati ya serikali sungusungu na Polisi kwa matukio yote yaliyojitokeza ndani ya robo ya kwanza ya mwaka na tayari tuna kituo kidogo cha polisi na tayari Mkuu wa kituo yupo na tunategemea kupata polisi wengine.

**MAPATO NA MATUMIZI KATA YA MWAMKULU**

| NA | MTAA | AINA YA MRADI | CHANZO CHA FEDHA | LENGO | ZILIZOKUSANYWA | ZILIZOTUMIKA | SALIO | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | MKWAJUNI | a.Ujenzi wa madarasa mawili ofisi na vyoo<br><br>b. Ugawaji wa viwanja<br><br>c.Ujenzi wa madarasa matatu<br><br>d.Ujenzi wa sekondari | Fedha toka serikalini<br><br>-Kuuza viwanja vya makazi<br><br>-Michango nguvu za wananchi<br><br>-Nguvu za wananchi | 60,000,000<br><br>-1,000,000/<br><br>-8,000,000<br><br>-2,000,000 | 60,000,000/<br><br>-600,000/=<br><br>- 6,000,000/<br><br>- 1,600,000/ | 60,000,000/=<br><br>-<br><br>-6,000,000<br><br>-1,400,000 | -<br><br>-600,000/=<br><br>-<br><br>- 200,000/= | Kazi imekamilika<br><br>-ununuzi wa tofali za sekondari<br><br>-Madarasa matatu yamekamilika<br><br>-kazi ya kusomba tofali na mchanga zinaendelea |
| 2 | KABW | a.Mchango | -Nguvu | - | - | -4,450,000 | -50,000/= | -Michango |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | AGA | wa sekondari<br><br>b.Mchango wa Shule ya msingi<br><br>c. ugawaji wa viwanja vya soko<br><br>d. Usafi wa mazingira<br><br>e. Patroo | za wananchi<br><br>-Nguvu ya wananchi<br><br>-Ada ya viwanja<br><br>-Faini<br><br>-Faini | 4,800,000<br><br>-200,000/=<br><br>-2,000,000<br><br>-275,000/=<br><br>-400,000/- | 4,500,000/<br><br>-180,000/=<br><br>-1,150,000/=<br><br>-135,000/=<br><br>-230,000/= | -180,000<br><br>-320,000<br><br>-125,000/=<br><br>-200,000/ | -<br><br>-830,000/=<br><br>-10,000/=<br><br>-30,000/= | inaendelea<br><br>-<br><br>-ugawaji unaendelea<br><br>-zoezi inaendelea |
| 3 | NGUVUMALI | Ujenzi wa darasa la sekondari | Nguvu za wananchi | 4,000,000/ | 2,500,000/= | 1,000,000 | 1,500,000/= | Michango inaendelea |
| 4 | NSESO | a.Umaliziaji wa madarasa mawili na ofisi<br><br>b. Patroo | Nguvu za wananchi<br><br>-Faini | 3,500,000/<br><br>-200,000 | 3,400,000/=<br><br>-140,000 | 3,200,000<br><br>-140,000 | 200,000/=<br><br>- | Kazi ya upauaji inaendelea<br><br>-kazi ya patroo inaendelea |
| 5 | MKOKWA | a.Ujenzi wa darasa shule ya sekondari | -Nguvu za wananchi | -4,000,000 | -3,000,000 | 2,500,000 | 500,000 | -Kazi zinaendelea |
| 6 | | a.Ujenzi wa ofisi ya Kata | -Fedha kutoka Halmashauri na | -4,550,000 | -4,550,000 | -3,300,000 | 1,250,000/= | -Jengo limefikia hatua ya lenta |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | KATA YA MWAMKULU | b.Ujenzi wa nyumba ya Afisa Ugani<br><br>c.Makosa mbalimbali<br><br>d.Baraza la Kata | nguvu za wananchi<br><br>-Fedha kutoka halmashauri<br><br>-Faini<br><br>-Faini | 57,000,000<br><br>-350,000<br><br>-800,000 | -17,000,000<br><br>150,000<br><br>- | 17,000,000<br><br>140,000<br><br>- | -<br><br>10,000/=<br><br>-800,000/= | **-Fedha zimekwisha tunaomba H/Mashauri ituimhizie ili tuendelee na mradi**<br>-<br><br>-kesi zimekuwa ni za kusuluhisha |
| 7 | | Ukarabati wa kivuko mto mafunsi Mwamkulu Inteka | Michago ya wananchi | -3,000,000 | 700,000 | - | 700,000/= | Tunaomba msanda wa Serikali |

**UKIMWI**

Kata ya Mwamkulu kwa kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka hakijafanya kikao chochote, hii ni kutokana na muingiliano wa shughuli na hivyo tunaahidi kufanya kikao ndani ya robo ya pili vikao viwili cha robo ya kwanza na ya pili

**MIRADI INAYOTEKELEZWA KWA KUPINDI HIKI CHA ROBO YA KWANZA YA MWAKA**

| NA | KATA | MRADI | HATUA YA UTEKELEZA | MTAA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | MWAMKULU | Ujenzi wa nyumba ya Afisa Ugani | Nyumba imeezekwa | Mkwajuni |
| 2 | - | Ujenzi wa madarasa mawili ,ofisi na matundu ya vyoo | yamekamilika | Mkwajuni |
| 3 | - | Ukamilishaji/umaliziaji wa madarasa | Madarasa mawili na ofisi moja zimekamilika | Nguvumali |
| 4 | - | Uchimbaji wa visima virefu | Kazi za ufungaji wa pampu unaendelea | Mkokwa,Nguvumali, Nseso na Mkwajuni |
| 5 | - | Ujenzi wa Ofisi ya Kata | Boma lipo kwenye hatua ya lenta | Mkwajuni |

**HIFADHI YA BONDE LA MTO KATUMA**
Katika kipindi hiki cha robo ya kwanza ya mwaka, kazi ya ulinzi wa hifadhi ya mazingira ndani ya bonde la mto Katuma zinaendelea vizuri kwa kufanya doria ndani ya bonde

**MIUNDOMBINU**
Kata ya Mwamkulu haina barabara ya uhakika ususa ni kutoka Kata ya Mwamkulu hadi barabara inakwenda Karema, vilevile haina barabara zinazounganisha mitaa ndani ya Kata.

**CHANGAMOTO**
1. Wakulima kutokuwa na uelewa juu ya kujiunga na chama cha umwagiliaji
2. Miundombinu ya barabra kutopitika wakati wa masika.
3. Upungufu wa Maafisa Ugani/Watendaji mitaa.
4. Mifereji wa skimu ya umwagiliaji kutokamilika kwa wakati

**MWISHO.**
Nawashukuru wale wote waliotoa mchango wao wa mawazo ili kufanikisha uandaaji wa taarifa hii ya robo ya kwanza ya mwaka Julai hadi Septemba **2018**

**Mheshimiwa Mwenyekiti**
Naomba kuwasilisha

**KALIPI S. KATANI**
**MHE. DIWANI KATA YA MWAMKULU**

**KATA YA MISUNKUMILO**

**TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA JULAI - SEPTEMBA 2018**

**<u>UTANGULIZI:</u>**-

Kata ya Misunkumilo ni miongoni mwa Kata sita (6) zinazounda Tarafa ya Misunkumilo, Kata ya Misunkumilo kwa upande wa Mashariki imepakana na Kata ya Makanyagio na Kata ya Mpanda Hotel, Magharibi imepakana na Kata ya Kabungu, Kaskazini imepakana na Kata ya Shanwe, Kusini imepakana na Kata ya Kakese.

**<u>IDADI YA WATU NA KAYA:-</u>**

Kiutawala Kata ya Misunkumilo ina jumla ya Mitaa mitatu (3)na Kijiji kimoja chenye Vitongoji kumi (10). Kata hii ina jumla ya Kaya **2026 na Wakazi wapatao 10,522 kati ya hao Wanaume ni 5154 Wanawake 5368.**

**<u>WATUMISHI:-</u>**

Watumishi wafuatao 1. Afisa Mtendaji wa Kata, Afisa Afya, Afisa Kilimo, **Afisa DHANA**, Mratibu Elimu, Afisa Mtendaji wa Mtaa mmoja jumla wapo watumishi sita (6).

**<u>MAPUNGUFU:-</u>**

Mapungufu yapo mapungufu ya Watendaji watatu (3).

**<u>MAPATO:-</u>**

Katika mwaka wa fedha **2018/2019** Kata ya Misunkumilo imekisia kukusanya na kupokea **Tshs. 10,248,498.40** toka katika vyanzo vyake vya mapato kwa mchanganuo ufuatao:-

1. Posho za Wenyeviti wa Mtaa 4............... Tshs. 800,000.00
2. Posho za Wajumbe wa Mitaa na Vitongoji………. Tshs.2,000,000.00
3. Fedha ya kuendeshea ofisi ya Kata …… Tshs. 200,000.00
4. Fedha ya kuendeshea ofisi za Mitaa …….. Tshs. 712,982.40
5. Fedha ya Miradi ya Maendeleo ngazi ya Kata …………..Tshs. 883,000.00
6. Malipo ya Mnara wa simu AIRTEL ….. Tshs.1,200,000.00
7. Michango ya wananchi kwa shughuli za M/leo …………..Tshs.1,800,000.00

   **<u>JUMLA TSHS. 10,248,498.40</u>**

**MATUMIZI KWA KIPINDI CHA JULAI – SEPTEMBA 2018:-**

Jumla ya Tshs. 100,000/= zimetumika kulipa walichimba shimo la choo ya Shule ya Msingi Milala.

**MAPATO YA HALMASHAURI YA MANISPAA:-**

Jumla ya Tshs. 749,400/= zimekusanywa eneo la maegesho ya magari Misunkumilo kwa ajili ya ushuru wa choo na kuoga.

**CHANGAMOTO:-**

Wateja ni wachache wengi wameanza kurudi Mjini na hasa wenye magari na hata mafundi Seremala.

**UJENZI WA VYUMBA VYA MADARASA:-**

Kwa kipindi cha Julay – September 2018 jitihada zimefanyika za kukusanya mawe tripu 10 na trip 1 ya kokoto na fedha Tshs. 300,000/= kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa shule ya Msingi Misunkumilo michango inaendelea.

Aidha, jumla ya matofari 9000 na tripu 10 za mawe na tripu 5 za mchanga zimekusanywa katika shule ya Msingi Milala. Pia bati chakavu zimeuzwa kiasi cha Tshs. 2,608,300/= kimepatikana ambacho kulipa fundi wa kujenga madarasa. Aidha tunahitaji kukusanya tofari asilimia 7% toka kwa wafyatuaji wote waliochukua vibari na wasiochukua vibari.

**HALI YA USALAMA:-**

Hali ya Usalama katika Kata siyo mbaya sana yapo matukio madogo madogo ambayo hayawezi kuzuilika.

**HALI YA UTAWALA BORA:-**

Kutokana na uhaba au upungufu wa Watendaji wa Mitaa unasababisha kutofanyika kwa vikao kwa muda muafaka na hasa Mitaa yote isiyokuwa na Watendaji wa Mitaa.

## TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA JULAI – SEPTEMBA 2018

| KATA | KIJIJI/ MTAA | AINA YA MRADI | CHANZO CHA FEDHA | FEDHA ILIYOPOKELEWA | FEDHA ILIYOTUMIKA | FEDHA ILIYOBAKI | HATUA YA UTEKELEZAJI | MAELEZO |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| M/NKUMILO | KAMPUNI | 1.UJENZI WA VYUMBA VYA MADARASA 2. OFISI NA VYOO 2 | MANISPAA YA MPANDA | 60,564,000 | 60,564,000 | - | UJENZI UMEKAMILIKA | MRADI UMEKAMILIKA |
| M/NKUMILO | MIS/MILO | UJENZI WA VYUMBA VYA MADARASA SEKONDARI 2 | MANISPAA YA MPANDA | 40,000,000 | 40,000,000 | - | UJENZI UMEFIKIA 100% | MRADI UMEKAMILIKA |
| | MIS/MILO | UKAMILISHAJI WA MAABARA | MANISPAA YA MPANDA | 9,000,000 | 9,000,000 | - | SHUGHULI IMEKAMILIKA | MRADI UMEKAMILIKA |
| **JUMLA** | | | | **109,564,000** | **109,564,000** | - | - | - |

**KILIMO CHA PAMBA:-**

Jumla ya wakulima 26 wamechukua mbegu za pamba sawa na kilo 1065 za mbegu na wanaendelea kuchukua.

**ZAO LA KOROSHO:-**

Zao la korosho linaendelea kutunzwa licha ya changamoto za mifugo, wafugaji wanakumbushwa kuangalia mashamba ya korosho na wakulima waendelee kufanya usafi mashamba yao. Jumla ya ekari 68 zilipandwa zao msimu uliopita.

**CHANJO YA HOMA YA MAPAFU:-**

Kata ya Misunkumilo ina jumla Ng'ombe 1989. Ng'ombe 510 wamechanjwa na Ng'ombe 1479 hawakuchanjwa. Na Kata ina jumla ya wafugaji 69, wafugaji 32 ndiyo waliochanja chanjo ya kuzuia Homa ya mapafu.

**CHANGAMOTO:-**

Wafugaji wengi hawaelewi umuhimu wa chanjo.

**SEKTA YA MAJI:-**

Kwa kipindi cha Julai – September 2018 visima vimechimbwa eneo la Milala na Mpanda Girls bado havijafungwa pampu na kufanya Kata nzima kuwa na visima 15 visima virefu.

**CHANGAMOTO:-**

Wananchi wengi wanashindwa kuchangia maji na kufanya ugumu wa matengenezo ya visima vikiharibika.

**VIKAO VYA KISHERIA:-**

Kwa kipindi cha Julai – September 2018 vikao vya WDC kimefanyika kikao kimoja, kikao cha Kamati ya kudhibiti Ukimwi kikao kimoja na vikao vya dharura 2 vya WDC.

**MAJANGA:-**

Hakuna majanga yaliyolipotiwa katika Kata

**SEKTA YA AFYA:-**

Kwa kipindi cha Julai – Septemba 2018 jumla ya Kaya 1730 zimefanyiwa ukaguzi (kutembelewa na Afisa Afya) kwa kukagua vyoo na usafi wa mazingira. Jumla ya Kaya 33 zilipatikana hawana vyoo bora Kaya 27 wamefikishwa Baraza la Kata na wamelipa faini Tshs. 80,000/= na kesi zinaendelea kusikilizwa.

Aidha nyumba za biashara zilizokaguliwa ni 4 na zimefungiwa, Baa 1 ya pombe za kienyeji na Mama lishe 3.

**UTORO SHULENI:-**

Kwa kipindi cha Januari – Septemba 2018 wanafunzi watoro 72 toka Shule ya Msingi Milala walifikishwa Baraza la Kata, wote walirudi shuleni baada ya kufikishwa Baraza la Kata na Wazazi walilipa faini.  Baadhi yao Jumla ya Tshs. 25,000/= wengine walipewa msamaha kutokana na idadi ya siku walizokosa, wengine ni Wazee walipewa onyo.

**MATUKIO:-**

Kwa kipindi cha Julai – Septemba 2018 Mwananchi mmoja alipata ajari ya kugonjwa na gari na kupoteza uhai wake.

**MIGOGORO YA ARDHI:-**

Jumla ya migogoro 5 imepatiwa ufumbuzi na migogoro 2 inashughulikiwa kusikilizwa na mmoja imepelekwa Manispaa kwa hatua zaidi.

**WANYAMA WAHARIBIFU:-**

Wanyama waharibifu Viboko wanaendelea kuharibu mazao ya Wananchi na hali ni mbaya sana kwa wanyama hawa, Wananchi wengi wanaendelea kulalamika bila mafanikio.  Tuombe Serikali isaidie kilio cha Wakulima.

Naomba kuwasilisha,

**Mhe.Matondo Kanyepo**
**Diwani kata ya Misunkumilo**

**KATA YA MPANDA HOTEL**

**TAARIFA YA UTEKELEZAJI SHUGHULI ZA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA 2018/2019 KATA YA MPANDA HOTEL IKIWA NI ROBO YA KWANZA JULAI HADI SEPTEMBA 2018**

**A.UTANGULIZI.**

Kata ya Mpanda Hotel ni miongoni mwa kata **15** zinazounda manispaa ya mpanda. Ambayo ipo tarafa ya Misunkumilo Wilaya ya Mpanda

B. **MIPAKA YA KATA.**

- Upande wa Mashariki imepakana na Kata ya Majengo
- Upande wa Kaskazini imepakana na Kata ya Makanyagio
- Upande wa Magharibi imepakana na Kata ya Misunkumilo
- Upande wa Kusini imepakana na Kata ya Ilembo

C**. UONGOZI WA KATA**

Kata ya Mpanda Hotel ina viongozi wa kuchaguliwa na wa kuajiriwa kama ifuatavyo:

i. Mhe. Diwani wa Kata- CCM- WILLIAM K. LIWALI
ii. Wenyekiti wa mitaa 3 wa CCM
iii. Mtendaji wa Kata -1
iv. Mtendaji wa Mtaa -1
v. Wataalam ngazi ya Kata-6, Elimu,Afya,Maendeleo ya jamii,Kilimo,Mifugo na uvuvi

**D.IDADI YA VIKAO NA MIKUTANO VYA ROBO JULAI-SEPTEMBA**

| **VIKAO VYA WDC HITAJIKA** | **VILIVYO FANYIKA** | **PUNGUFU** |
|---|---|---|
| 1 | 2 | - |

**IDADI YA VIKAO NA MIKUTANO YA ROBO YA KWANZA JULAI –SEPTEMBA**

| **MTAA** | **VIKAO HITAJIKA** | **VILIVYO FANYIKA** | **VIKAO VYA MITAA** | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **PUNGUF** | **MIKUTANO** | **ILIYOFANYIKA** | **PUNGUFU** |
| MPANDA HOTEL | **3** | **5** | ***-*** | ***1*** | ***3*** | **-** |
| MSASANI | **3** | ***5*** | ***-*** | ***1*** | ***3*** | ***-*** |
| TAMBUKARELI | **3** | ***5*** | ***-*** | ***1*** | ***3*** | ***-*** |

**IDADI YA KAYA NA WAKAZI WAKE**

| JINA LA KATA | JINA MTAA | IDADI YA KAYA | IDADI YA WATU | | | WENYE UWEZO WA KUFANYA KAZI | | | WASIO NA UWEZO WA KUFANYA KAZI | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | MPANDA HOTEL | 780 | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML |
| | | | 1348 | 1437 | 2785 | 513 | 623 | 1201 | 770 | 814 | 1584 |
| | MSASANI | 431 | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML |
| | | | 1424 | 1460 | 2884 | 692 | 691 | 1383 | 732 | 769 | 1501 |
| | TAMBUKA RELI | 545 | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML |
| | | | 1463 | 1495 | 2958 | 731 | 747 | 1478 | 746 | 797 | 1543 |

**TAARIFA ZA ZIARA ZA VIONGOZI KATIKA KATA**

Kwa kipindi cha Julai-Septemba, Kata imepokea viongozi mbalimbali waliofanya ziara ndani ya Kata kama ifuatavyo:-

1. Tarehe 08/08/2018 ziara ya Mbunge wa Mpanda Kati
2. Tarehe 17/09/2018 ziara ya Meya Mhe. **WILLIAM MBOGO**
3. Tarehe 8/9/2018, 11/9/2018 na 12/9/2018 ziara ya Mhe. Diwani kwenye mitaa yote.

**SHUGHULI ZA KIUCHUMI ZA WANANCHI**

- Wakulima na wafugaji wadogo wadogo
- Uchimbaji mdogo mdogo wa madini
- Wafanya biashara wakumbwa na wadogo
- Wafanyakazi wa sekta mbalimbali
- Mafundi wa fani mbali mbali

**TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA KIPINDI CHA JULAI HADI SEPTEMBA 2018**

| MTAA | JINA MRADI | CHANZO FEDHA | FEDHA TOLEWA | FEDHA TUMIKA | SALIO | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| MPANDA HOT | Posho ya Mwenyekiti na Wajumbe | H/manispaa Mapato ya ndani | - | - | - | Haijapokelewa kwa kipindi cha julai hadi Septemba 2018 |
| | Ujenzi wa choo cha shule ya Mpanda | wananchi | 308,500 | - | 308,500 | Mchango unaendelea. |
| | Ujenzi wa choo cha shule | wananchi | 115,000 | - | 115,000 | Mchango unaendelea |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Muungano | | | | | |
| MSASANI | Posho ya Mwenyekiti na Wajumbe | Halmashauri mapato ya ndani | - | - | - | Fedha haijatolewa |
| | Ujenzi wa shimo la choo cha wanafunzi matundu 20 | wananchi | 115,000 | - | 115,000 | Mchango unaendelea |
| TAMBUKA RE | Posho ya Mwenyekiti na Wajumbe | Halmashauri mapato ya ndani | - | - | - | Fedha haijatolewa |
| | Ujenzi wa shimo la choo | wananchi | 65,000 | - | 65,000 | Mchango unaendelea |

**MADENI YA FEDHA**

Kata ya Mpanda Hotel inadaiwa jumla Tshs kwa matumizi ya kununua vifaa vya kutumia kama ifuatavyo.

i. 12/7/2018 limu 2 za karatasi @12000=24000
ii. Kuchapa taarifa print 14 @1000 =14000
iii. Photocopy ....56@ 100 =5600
iv. Steplar mashine 1@ 3500 =3500
v. Punching mashine 1@ 3500 = 3500
vi. Mafaili ya ofisi 10@ 1000 = 10000
vii. Kununua kaunta book 1@3500 =3500

**JMLA TSHS. 64,100/=**

Mkutano wa mbunge tarehe **8/8/2018 Tshs 26,000**

Malipo umeme ulotumika **Tshs 5000**

**8/9/2018- matumizi ya mikutano ya Mh.Diwani kuanzia tarehe 8/9/2018 hadi tarehe 12/9/2018**

i. Matangazo mitaa 3 @ 8000 =24000
ii. Kubeba viti na meza =15000
iii. Kulipia umeme wa mkutano =5000
iv. Maji kwa vingozi walioshiriki 3 catoni@4500 =13500

**Jmla ndogo 62500/=**

**Mkutano wa Mhe. Meya tarehe 17 /9/2018**

i. Kuchapa taarifa printing 3@1000=3000
ii. Kutoa copy 6 @100 =600
iii. Maji ya kunywa ya vingozi 3caton @ 4500=13500
iv. Umeme wa vipoza sauti =5000

**Jmla ndogo 22,100/=**

**Matumizi kikao cha maendeleo ya kata cha tarehe 18/9/2018**

i. Chakula cha wajumbe 20 Tsh. 40,000
ii. Maji katoni 2 @4500 = Tsh. 9,000

**JUMLA NDOGO 49,000/=**

**Jumla ya deni lote ni Tshs 224,500**

**SEKTA YA ELIMU**

TAARIFA ZA SHULE ZA MSINGI NA SEKONDARI

HABARI ZA WANAFUNZI

| **JINA LA SHULE** | **JINSIA** | ***MADARASA*** | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **AWALI** | **I** | **II** | **III** | **IV** | **V** | **VI** | **VII** | ***JUMLA*** |
| SHULE YA MSINGI MPANDA | WAS | 72 | 157 | 165 | 170 | 120 | 78 | 57 | 72 | *891* |
| | WAV | 99 | 133 | 162 | 155 | 140 | 91 | 62 | 72 | *1914* |
| | JML | 171 | 290 | 327 | 325 | 260 | 169 | 119 | 144 | *1805* |
| SHULE YA MUUNGANO | WAV | 83 | *104* | *109* | *121* | *109* | *74* | *62* | *56* | *718* |
| | WAS | 77 | *101* | *123* | *120* | *101* | *83* | *61* | *49* | *715* |
| | JMLA | *160* | *205* | *232* | *241* | *210* | *157* | *123* | *105* | *1433* |

**HABARI ZA WALIMU**

| **JINA SHULE** | **MAHITAJI** | | | **WALIOPO** | | | **PUNGUFU** | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| S/ MSINGI MPANDA | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML |
| | *18* | *11* | 29 | *7* | *12* | 19 | *4* | *6* | *10* |
| S/MSINGI MUUNGANO | ME | KE | JML | ME | KE | JML | ME | KE | JML |
| | *24* | *18* | *42* | *4* | *12* | *16* | *20* | *6* | *26* |

**SEKTA YA MAJI**

Kata ya Mpanda Hotel ina upungufu wa upatikanaji wa maji safi na salama kwani maji yanayopatikana hayatoshelezi kwa wananchi.

- Mpanda Hotel ina kisima kimoja kifupi ambacho ni kibovu.
- Mpanda Hotel ina magati matatu ambayo yote mabovu

- Msasani kuna kisima kirefu kimoja ambacho bado hakijaanza kutoa huduma.
- Tambukareli ina kisima kimoja kifupi kinachotoa maji na gati moja la TASAF.

Katika kutatua shida ya maji kunahitajika visima kama ifutavyo:-

- Mpanda Hotel visima virefu vitatu (3)
- Msasani ina hitaji kisima kirefu kimoja (1)
- Tambukareli ina hitaji visima virefu viwili (2)

Katika kutatua shida ya maji kwa wananchi wa Kata ya Mpanda Hotel vina hitajika visima virefu sita (6).

**SEKTA YA KILIMO.**

Katika Kata ya Mpanda Hotel wakulima wamehimizwa kulima mazao ya biashara kuongeza kipato na kujiwekea akiba kwa kulima mazao ya korosho, pamba na alizeti pamoja na mazao ya chakula kwa msimu wa **2018/2019.**

- Mazao ya chakula yanapatikana kwa bei nafuu.

**USAFI WA MAZINGIRA.**

Usafi wa maeneo kwa kuwahamasisha wananchi kufanya usafi kwenye maeneo yao ambayo timu ya Kata imefanikisha kusimamia maeneo ya stesheni, eneo la viwanda kuondoa taka zilizokuwa zinazagaa na kuona eneo hilo lina kuwa safi.

Eneo linalosumbua kwa usafi ni eneo la ujenzi ambako wafanyakazi wanaokutwa pale wanadai eneo hilo husafishwa na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya kwa kupeleka vibarua kufanya usafi eneo hilo. Pili eneo linalosemekana la ujenzi na viongozi wa CCM wanasema lao

Viongozi hao wa ccm kata hawapatikani ku fanyas usafi eneo hilo
Katika kuhahakikisha mpanda hotel inakuwa safi tunaendelea kugawa maeneo madogo madogo ya usimamizi kwa viongozi wa Kata wote na Mtaa kuhakikisha Mpanda hotel inakuwa safi mgawanyo wa eneo utatolewa taarifa baada ya kukamilika kugawa.

**SEKTA YA MAENDELEO YA JAMII**

Sekta ya maendeleo ya jamii imekuwa ikihamasisha wananchi kujiunga na vikundi vilinyoundwa ni.

i. Makini Group –Mpanda Hotel -14 – wameomba mkopo
ii. Tulye Group-Mpanda Hotel – 5 – Bado Kuomba
iii. Tulihamwe Group -Mpanda Hotel
iv. Tubagile Group -5 – bado kuomba
v. Mapinduzi Group -10 – bado kuomba
vi. Wauza Mahindi -16 – bado kuomba

**TASAF III**

- **UIBUAJI MIRADI YA MUDA MFUPI.**

Miradi iliyoibuliwa kupitia mradi huu ni.

(a) Uchimbaji wa bwawa la samaki.
(b) Mradi wa maji
(c) Bustani jiko

**ULINZI NA USALAMA.**

Katika kusimamia ulinzi na usalama wananchi wameendelea kuelimishwa juu ya kuunda vikundi vya ulinzi shirikishi ili kuimarisha ulinzi na kupunguza matukio ya uhalifu. Pamefanyika mikutano kwa mitaa yote mitatu kwa tarehe.

i. 8/9/2018 Mkutano ulifanyika Mpanda Hoteli
ii. 11/9/2018 Mkutano ulifanyika mtaa wa msasani
iii. 12/9/2018 Mkutano ulifanyika Tambukareli

Mikutano hii iliendshwa na Mhe. Diwani wa Kata pia OC-CID alihudhuria mkutano hii yote kwa kuhamasisha suala la ulinzi shirikishi.

**UKIMWI.**

Kata ya Mpanda Hotel imeendelea na jukumu kuielimisha jamii ambapo vikao na mikutano vimekuwa vikiendeshwa kwa kuelimisha wananchi kuepuka vitendo ambavyo vinaweza kuwafanya kuambukizwa ukimwi kwa kuacha ngono zembe.

Pia wajumbe wa kamati ya ukimwi wamesisitizwa kuendelea kuelimisha jamii kupitia vikao na makongamano mbalimbali.

**CHANGAMOTO**

- Upungufu wa vyumba sita (6) vya madarasa sekondari Kashaulili.
- Upungufu wa matundu 13 ya vyoo Kashaulili sekondari.
- Ukosefu wa uzio eneo la Kashaulili sekondari.
- Wananchi kutochangia michango ya maendeleo japo wanapitisha kwenye mikutano.

**UTATUZI.**

- Vikao vimefanyika kuhamasisha wananchi kuchangia michango ili kukabiliana na changamoto hizo.
- Mpango wa Kata ni kujenga vyumba viwili (2) kila mwaka.

**Naomba kuwasilisha.**

Mhe. Wiliam Liwali

Diwani wa Kata

Kata ya Mpanda Hotel

**KATA YA SHANWE**
**TAARIFA YA UTEKELEZAJI YA MIRADI YA MAENDELEO KATA YA SHANWE YA ROBO YA KWANZA YA JUALI – SEPTEMBA 2018.**

## 1. UTANGULIZI.

Kata hii ya Shanwe ni miongoni mwa kata kumi na tano (15) zinazounda Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda na iko kaskazini magharibi mwa Manispaa ndani ya Tarafa ya Kashaulili na ina mitaa mine (4) ambayo ni Shanwe, Kigamboni, Kivukoni na Kilimahewa. Kwa mujibu wa sense ya watu na makazi ya mwaka 2012 Kata hii ina jumla ya wakazi.

| **Na** | **MTAA** | **KAYA** | **WATU** | **ME** | **KE** |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | KIGAMBONI | 1000 | 5100 | 2300 | 2800 |
| 2 | SHANWE | 270 | 900 | 430 | 470 |
| 3 | KIVUKONI | 950 | 4788 | 2245 | 2543 |
| 4 | KILIMAHEWA | 238 | 602 | 290 | 321 |
| | **JUMLA** | **2462** | **11590** | **5265** | **6125** |

## 2. SHUGHURI ZA WAKAZI.

1. Wakulima
2. Watumishi wa serikali na kwenye mashirika mbalimbali
3. Wafanyabiashara ndogondogo.
4. Wafugaji wadogowadogo.

## 3. VIKAO VYA KISHERIA.

1. Ngazi ya Kata.
   Imefanyika **WDC** moja ya tarehe **28/9/2018** ya robo ya kwanza (1) ambayo kazi yake ni kupitia na kujadili taarifa ya mapato na matumizi ya Kata na pia kujadili na kupitisha taarifa mbalimbali za vikao vya mitaa na mikutano mikuu ya mitaa.

2. Ngazi ya mitaa.
   Vimefanyika vikao vya ndani (7) kati ya (9) imefanyika mikutano ya hadhara (4) kwa mitaa yote.

4. **MAPATO NA MATIMIZI.**

**(a) Ngazi ya Kata.**

(i) Salio **Tsh. 61,000/=**
(ii) Mapato **Tshs. 300,000/=** toka kwa wadau wa NIDA.
(iii) Matumizi **Tshs. 300,000/=** posho ya wasimamizi wa NIDA.
(iv) Salio **Tshs. 61,000/=**

**(b) Ngazi ya Mtaa.**

(i) Mtaa wa Kilimahema wana **Tshs. 1,000, 000/=** za ujenzi wa zahanati fedha hizi ni kati ya kukusanya **Tshs.8,000,000/=** kwa kaya **1600** kila kaya itachangia **Tshs. 5,000/=** na WDC iliagiza fedha hizi zipelekwe Benki kwenye Akanti ya mtaa au ya Kata.

(ii) Mtaa wa kigamboni – hakuna mapato

(iii) Mtaa wa Shanwe – hakuna mapato.

(iv) Mtaa wa kivukoni **– Tshs. 200,000/=**

## 5. MAMBO YALIYOFANYIKA KWA KIPINDI CHA MIEZI 3.

1. Tumefanikiwa kusimamia ukusanyaji wa fedha kiasi cha **Tshs.1,000,000/=** katika mtaa wa Kilimahewa kwa ajili ya ujenzi wa zahanati ambapo matarajio ni kukusanya **Tshs. 8,000,000/=** kwa kaya **1600** na kila kaya imetegemea kutoa T**shs. 5,000/=**

2. **WDC** imeagiza kuwa kila mtaa ushiriki katika zoezi la kuchagia ujenzi wa Zahanati ambapo mchago utakuwa **Tshs 8,000,000**/= na kila kaya itachangia **Tshs. 5,000/=** ambapo kwa mitaa yote minne tunategemea kupata **Tshs. 32,000,000/=**

3. Pia WDC imeagiza kuwa mchago wa ujenzi wa madarasa mawili kila shule ambapo kila mtaa utachagia **Tshs. 8,000,000/=** na kwa kila kaya **Tshs. 5,000/=**

## 6. HUDUMA ZA JAMII.

(a) Elimu ya sekondari na msingi .miundombinu.

| **Na** | **shule** | **madarasa** | | | **madawati** | | | **vyoo** | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | **Mah** | | **yal** | | **pung** | |
| | | **Mah** | **yal** | **pung** | **Mah** | **yal** | **pung** | **me** | **ke** | **me** | **ke** | **me** | **ke** |
| 1 | S/S Shanwe | 24 | 12 | 12 | 821 | 561 | 260 | 12 | 12 | 6 | 6 | 6 | 6 |
| 2 | S/Msingi Shanwe | 30 | 5 | 25 | 490 | 290 | 200 | 12 | 12 | 4 | 4 | 6 | 6 |
| 3 | S/M/Kivukoni | 27 | 5 | 22 | 489 | 148 | 141 | 12 | 12 | 3 | 3 | 9 | 9 |
| 4 | S/M/Mkanyagio | 32 | 8 | 24 | 435 | 274 | 161 | 12 | 12 | 6 | 6 | 6 | 6 |

**(c) Walimu na wanafunzi.**

| **Na** | **Shule** | **Walimu** | | | **wanafunzi** | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **Me** | **Ke** | **Jumla** | **Me** | **Ke** | **Jumla** |
| 1 | S/S Shanwe | 18 | 18 | 27 | 406 | 473 | 880 |
| 2 | S/M Shanwe | 7 | 10 | 18 | 552 | 623 | 1175 |
| 3 | S/M Kivukoni | 7 | 7 | 14 | 517 | 532 | 1049 |
| 4 | S/M Makanyagio | 5 | 9 | 14 | 664 | 697 | 1361 |

## (d) Maji

| Na | Mtaa | Visima vilefu | | | Magati | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Visima | Vibovu | Jumla | Mazima | Vibovu | Jumla |
| 1 | Shanwe | 1 | 0 | 1 | 3 | 0 | 3 |
| 2 | Kivukoni | 1 | 1 | 1 | 4 | 0 | 4 |
| 3 | Kigamboni | 1 | 0 | 1 | 5 | 0 | 5 |
| 4 | Kilimahewa | 0 | 0 | 0 | 4 | 0 | 4 |

Suala la maji siyo tatizo sana kwa Kata ya Shanwe na mitaa yake yote minne kwa sababu pipa zote za maji toka Ikolongo na manga na Bwawani zimepitia hapa Shanwe, kwa hiyo ni suala la kuunganisha mabomba kwa gharama za wananchi wenyewe.

7. **AFYA**

**(a) AFYA TIBA**

Kwa sasa wananchi wa kata hii ya Shanwe wanaendelea kupata huduma za afya tiba pamoja na huduma za mama na mtoto katika Hospitali ya Wilaya na Hospitali ya Mwangaza lakini maandalizi ya ujenzi wa Zahanati yamesha anza na kwa sasa tuko kwenye hatua ya michango na tumekusanya **Tshs. 1,000,000/=** kati ya Tshs. **32,000,000/=** zinazohitajika.

(b) **AFYA KINGA.**

Wananchi wanaendelea kuelimishwa juu ya usafi wa mazingira yao hususani kuwa na vyoo na kuvitumia ikiwa ni pamoja na kufyeka nyasi.

8**. UTAWALA BORA.**

**a.** Utawala Demokrasia unaendelea kutumika kupitia vikao vya WDC ambapo wajumbe wake ni wenyeviti wa serikali za mitaa, wataalamu wote ngazi ya kata. Viongozi wa chama Tawala na viongozi na viongozi wa dini kadhalika katika mitaa utawala wa Demokrasi unatumika kupitia vikao vya ndani ya mikutano ya hadhara.

**b. UTAWALA WA KISHERIA.**

Unatumika kupitia baraza la Kata ambapo watu wote huelekezwa kupeleka malalamiko yao na kusikilizwa na maamuzi kutolewa kwa kufuata sheria.

9. **ULINZI NA USALAM.**

Swala la ulinzi na usalama linaendelea kufanyiwa kazi ka usimamizi wa kamati ya ulinzi na usalama wa Kata pamoja na Polisi wa Kata na viongozi wote wa chama na Serkali pamoja na viongozi wa dini.

**10. KILIMO/MIFUGO/UVUVI.**

Yamelimwa mashamba darasa heka tatu **(3)** ambayo ni **(i)** shule ya msingi Kivukoni wamepata gunia **sita** za mahindi (ii) shule ya msingi Shanwe walipata gunia **sita** na debe moja, **(iii)** ofisi ya mtendaji wa Kata **hawakupata kitu**, pia zinatarajiwa kulimwa heka **100** za zao la korosho na pamba ikiwa ni pamoja na Taasisi za Serikali

Imetolewa chanjo ya ng'ombe **301**, mbuzi **80** mbwa **68**, kuku **1778.**

11. **BIASHARANA MASOKO.**

Wananchi wa kata ya Shanwe wanaendelea kufanya shughuli zao za biashara ndogondogo kwenye maeneo yao na kwenye maeneo ya wazi ya mtaa wa Kilimahewa na kigamboni wakati wanasubiri Muwekezaji atakaye chimba choo kwenye Soko la Kilimahewa, na pia wakati tunasubili kibari cha kubadilisha maeneo ya wazi kuwa maeneo soko.

**12. ARDHI.**

Tayari maeneo ya kilimahewa yameshapimwa kuwa viwanja na wahusika wanaendelea kugawimwa viwanja hivyo.

13. **MAENDELEO YA JAMII.**

**a. VIKUNDI.**

Katika sekta hii kuna vikundi viwili ambavyo havijalejesha mkopo, ambapo agizo la **WDC** mtendaji wa Kata afatilie vikundi hivyo ili walejeshe mkopo wanaodaiwa.

b. **TASAF** vilevile Nyanja hii ya maendeleo ya jamii kaya **49** za mtaa wa Kivukoni zinaendelea kunufaika na malipo ya **CCT** pamoja na malipo yanayotokana na ajira za muda wanazofanya kazi walengwa.

14. **MIGOGORO**

Ipo migogoro miwili kama ifuatavyo:-

a. Mgogoro wa zamani huo ni mgogoro wa kuvamiwa kwa eneo la shule ya msingi shanwe na familia ya Mzee Mwanameli bado unaendelea pamoja na kwamba mzee huo ameshafaliki na kwamba bado shauli liko kwenye mahakama ya rufaa la kijiji bado familia yake wanaendelea kumega maeneo ya shule na kuunza kwa kisingizio cha kwamba Baba yao ndiye aliyeuza kabla hajafaliki. Kwahiyo mgogoro bado unaendelea mpaka sasa.

b. Mgogoro mpya ni ule wa wananchi mmoja mgeni alinyehamia hivi kalibuni kutoka Shirati kuja mta wa Kigamboni aitwae **MBWANA** wananchi wa mtaa huo wa Kigamboni walivamia nyumba yake siku ya tarehe **10/10/2018** asubuhi kwa madai yakuwa amekuwa mkorofi kwa wananchi wa Kigamboni ambapo waliharibu baadhi ya mali kama sola na mirango na madirisha na baadae wananchi hao kuja kuvamia ofisi ya mtendaji wa Kata ili mtendaji wa Kata akamuondoe, kwa bahati nzuri vulugu hizi zilizimwa na Polisi, na baadae mtuhumiwa kuhifadhiwa Polisi.

15. **CHANGAMOTO.**

(i) Uchelewaji wa kibali cha kubadili matumizi ya ardhi kwa ajiri ya masoko kwa mitaa ya kivukoni na kigamboni.

(ii) Kwa muda mrefu hatujapokea fedha za ruzuku kwa ajiri ya miradi ya maendeleo na uendeshaji ofisi na kwenye viti wa serikai za mita.

(iii) Ofisi ya kata ta shanwe kutokuwa na chombo cha usafiri (pikipiki) kwa sababu kata ya shanwe iko mbali na makazo makuu zaidi ya kilometa 7.

(iv) Upungufu wa watumishi (Watendaji wa mitaa) kwa mitaa ya Kigamboni na Shanwe hivyo kufanya kazi kuwa ngumu.

Naomba kuwasilisha

**KANONI LUCAS**
**MHE. DIWANI KATA YA SHANWE**

## KATA YA UWANJA WA NDEGE

## TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA ROBO YA KWANZA JULY-SEPT 2018 KATA YA UWANJA WA NDEGE

### 1 A: UTANGULIZI

Kata ya Uwanja wa ndege ni miongoni mwa Kata 15 zilizopo katika Manispaa ya Mpanda katika Wilaya ya Mpanda Mkoa wa Katavi.

### B: MIPAKA YA KATA

Kata ya Uwanja wa ndege imepakana na Kata zifuatazo:-

*i.* Upande wa Kusini imepakana na Kata ya Ilembo
*ii.* Upande wa Kaskazini imepakana na Kata ya Nsemulwa
*iii.* Upande wa Magharibi imepakana na Kata ya Kashaulili na Mpanda Hotel
*iv.* Upande wa Mashariki imepakana na Kata ya Mtapenda.

### C: MAENEO YA UTAWALA

Katika Kata ya Uwanja wa ndege una mitaa mitatu (3) ambayo ni:-

*i.* Mtaa wa Mnazi mmoja
*ii.* Mtaa wa Msufini
*iii.* Mtaa wa Airtel

### D: IDADI YA WATU

Kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka **2012**, Kata ya Uwanja wa ndege ina jumla ya watu na kaya zenye mchanganuo ufuatao:-

| S/N | JINA LA MTAA | IDADI YA KAYA | IDADI YA WATU | ME | KE |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | MSUFINI | 463 | 2425 | 1185 | 1240 |
| 2 | MNAZI MMOJA | 588 | 2538 | 1233 | 1305 |
| 3 | AIRTEL | 493 | 2682 | 1259 | 1323 |
| | JUMLA | 1545 | 7540 | 3677 | 3863 |

### E. SHUGHULI ZA KIUCHUMI

Wakazi wa Kata ya Uwanja wa ndege wanajishughulisha na shughuli zifuatazo:-

*i.* Wafanyabiashara na wajasiriamali
*ii.* Wakulima wadogo na wafugaji
*iii.* Watumishi wa serikali na watumishi wa mashirika
*iv.* Wachimbaji wadogo wa madini mbalimbali

### F: HUDUMA ZA KIJAMII

Kata ya Uwanja wa ndege ina huduma za kijamii kama zifuatazo:-

*i.* Shule ya Msingi – S/M Kasimba
*ii.* Shule ya Sekondari – S/Sekondari Nsemulwa
*iii.* Uwanja wa ndege
*iv.* Huduma ya maji mitaa yote
*v.* Genge soko moja
*vi.* Makanisa na misikiti

## G: UONGOZI NA UTAWALA

Kata ya Uwanja wa ndege ina viongozi wa kuchaguliwa kama ifuatavyo:-

*i.* Mhe. Diwani wa Kata (1)
*ii.* Wenyeviti wa mitaa (3)
*iii.* Wajumbe wa serikali za mitaa (15)

Viongozi hao kwa pamoja wanatokana na chama tawala CCM.

**WATAALAM**

Kata ya Uwanja wa ndege ina wataalam wafuatao wanaotekeleza majukumu yao ya kiserikali wafuatao:-

| S/N | CHEO/NAFASI | NGAZI | IDADI | IDARA | ENEO LA KAZI |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | MTENDAJI KATA | KATA | 1 | UTAWALA | UWANJA WA NDEGE |
| 2 | AFISA MAENDELEO | KATA | 1 | MAENDELEO JAMII | UWANJA WA NDEGE |
| 3 | AFISA AFYA | KATA | 2 | AFYA | UWANJA WA NDEGE |
| 4 | AFISA UVUVI | KATA | 1 | MIFUGO/UVUVI | UWANJA WA NDEGE |
| 5 | AFISA KILIMO | KATA | 1 | KILIMO | UWANJA WA NDEGE |
| 6 | MRATIBU ELIMU | KATA | 1 | ELIMU | UWANJA WA NDEGE |
| 7 | WATENDAJI MITAA | KATA | 2 | UTAWALA | AIRTEL/M/MMOJA |
| 8 | WALIMU S/M | KATA | 24 | ELIMU | AIRTEL |
| 9 | WALIMU SEKONDARI | KATA | 21 | ELIMU | UWANJA WA NDEGE |

**VIKAO NA MIKUTANO**

Katika Kata ya Uwanja wa ndege kuna vikao vya kisheria vilivyofanyika pamoja na mikutano ya hadhara kwenye Mitaa yote ndani ya Kata kama inavyoonekana kwenye jedwali lifuatalo:-

| S/N | MTAA/KATA | AINA YA KIKAO | TAREHE YA KIKAO | MAHALI | MKUTANO |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | AIRTEL | SERIKALI YA MTAA | -27/7/2018<br>-28/8/2018<br>-26/9/2018 | OFISI YA KATA | 28/9/2018 |
| 2 | MSUFINI | SERIKALI YA MTAA | 01/10/2018 | OFISI YA KATA | |
| 3 | MNAZI MMOJA | SERIKALI YA MTAA | - /7/2018<br>-26/8/2018<br>-7/10/2018 | OFISI YA M/KITI | 8/10/2018 |
| 4 | UWANJA WA NDEGE | -ULINZI NA USALAMA<br>-KAMATI YA UKIMWI<br>-KAMATI YA MALALAMIKO<br>-KAMATI YA MAZINGIRA<br>-WDC | -5/9/2018<br>-22/9/2018<br>-28/9/2018<br>-5/10/2018<br>-17/10/2018 | OFISI YA KATA | |

## TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI

Kwa kipindi cha July-Sept **2018**, taarifa ya mapato na matumizi ni ifuatavyo kama ilivyosomwa na serikali za mitaa

| S/N | MTAA | CHANZO CHA FEDHA | KIASI POKELEWA | KIASI TUMIKA | SALIO |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | AIRTEL | -Fedha za MMEM(Msingi) fedha za MMES<br>-Tozo mbalimbali<br>-Ruz | -2,592,682.98<br>-7,640,226.58<br>-120,000 | -2,334,021.88<br>-4,594,220.00<br>-120,000 | -258,662.10<br>-3,046,006.58<br>- |
| 2 | MNAZI MMOJA | -Tozo mbalimbali (vibari) | 15,000/= | 15,000/= | - |
| 3 | MSUFINI | -Fedha za maendeleo toka Halmashauri | 100,000/= | 60,000/= | 40,000/= |
| 4 | UWANJA WA NDEGE | -Fedha za miradi ya maendeleo toka Halmashauri na Manispaa | 800,000/= | 650,000/= | 150,000/= |

## MAENDELEO YA UJENZI WA MIRADI MWAKA WA FEDHA 2018/2019

| S/N | AINA YA MRADI | MTAA | CHANZO CHA FEDHA | | GHARAMA YA MRADI |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | **SEKTA HUDUMA YA JAMII**<br>UJENZI WA OFISI YA KATA U/NDEGE | AIRTEL | HALMASHAURI 29,600,000/= | WANANCHI 7,400,000/= | 37,000,000/= |
| 2 | UJENZI WA SOKO | AIRTEL | 37,600,000/= | 9,400,000/= | 47,000,000/= |
| 3 | **SEKTA ELIMU**<br>-UJENZI WA MATUNDU 4 VYOO NSEMULWA SEKONDARY<br>-UJENZI WA MATUNDU 6 YA VYOO S/M KASIMBA | AIRTEL<br>AIRTEL | 4,000,000/=<br>4,000,000/= | 1,200,000/=<br>2,000,000/= | 6,000,000/=<br>6,000,000/= |
| 4 | UJENZI WA ZAHANATI | | 27,000,000/= | 5,000,000/= | 32,000,000/= |

## UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA MAENDELEO

### *I.* SEKTA YA ELIMU

Kata hii ina jumla ya shule 2, S/Msingi moja na sekondari moja.

**TAARIFA YA WANAFUNZI**

**S/M KASIMBA**

| DRS | I | II | III | IV | V | VI | VII | JML |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **WAV** | 208 | 279 | 182 | 173 | 101 | 72 | 54 | 1233 |
| **WAS** | 243 | 300 | 185 | 146 | 104 | 88 | 87 | 1325 |
| **JML** | 451 | 579 | 368 | 319 | 205 | 160 | 141 | 2558 |

**SEKONDARI NSEMULWA**

| KIDATO | I | II | III | IV | JML |
|---|---|---|---|---|---|
| **WAV** | 78 | 72 | 59 | 42 | 251 |
| **WAS** | 75 | 79 | 50 | 30 | 234 |
| **JML** | 153 | 151 | 109 | 72 | 485 |

**IDADI YA WALIMU**

| S/N | SHULE | MAHITAJI | WALIOPO | PUNGUFU |
|---|---|---|---|---|
| 1 | NSEMULWA SEK | 25 | 21 | 04 |
| 2 | KASIMBA S/M | 68 | 24 | 44 |
| **JUMLA** | | **93** | **45** | **48** |

**MAJENGO YA SHULE**

| SHULE | MADARASA | | | VYOO | | | OFISI | | | STOO | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | MAH | VIP | PUNG | MAH | VIPO | PUNG | MAH | VIP | PUN | MAH | VIP | PUN |
| S/M KASIMBA | 68 | 08 | 60 | 115 | 10 | 105 | 04 | 02 | 02 | 04 | 01 | 03 |
| S/K NSEMULWA | 12 | 08 | 04 | 18 | 12 | 06 | 02 | 02 | - | - | - | - |

Taarifa ya wanafunzi waliofanya mtihani wa darasa la saba ni wahitimu **143** kati yao wavulana ni **56** na wasichana ni **87**, wavulana **11** hawakufanya mtihani kutokana na utoro.

**TAALUMA**

Shule zimeendelea kufanya vizuri katika suala la elumi, hali ya ufaulu wa wanafuzni umekuwa ukiongezeka mwaka hadi mwaka. Hii inatokana na hali ya kujituma ya walimu na wanafunzi pamoja na wazazi katika kuchangia nguvu zao na mali kwa ajili ya kufaniisha suala la elimu.

**CHANGAMOTO KATIKA SEKTA YA ELIMU**

*i.* Upungufu wa vyumba vya madarasa
*ii.* Umbali wa wanafunzi kutoka nyumbani hadi shuleni
*iii.* Ukosefu wa umeme vyumba vya madarasa.

**UTATUZI**

*i.* Wazazi wamejitoa kuchangia tofali kila mtoto tofali 10 ili kuongeza madarasa.
*ii.* Hamasa inaendelea kutolewa kwa maeneo yaliyopo mbali na shule kuanza ujenzi wa shule na kuandikisha wanafunzi shule jirani
*iii.* Shule imefanikiwa kuingiza umeme katika chumba kimoja cha darasa

## *II.* MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO

Katika kipindi cha robo ya kwanza kuanzia July-Sept 2018 kazi zilizofanyika ni:-

*i.* Kutembelea kaya za watu wanaoishi katika mazingira magumu na kaya za wanaoishi na virusi vya UKIMWI kuwapa elimu katika Mtaa wa Mnazi mmoja

*ii.* Kukutana na wanavikundi wanaosuasua kurejesha mkopo. Vikundi vya Amakwao, pamoja na kikundi cha wanawake cha Tumaini.

*iii.* Kufuatilia marejesho ya mikopo yote

*iv.* Kuhudhuria vikao vya Kata vya uibuaji wa miradi ya maendeleo, kikao cha kamati ya **UKIMWI**, malalamiko pamoja na **WDC**.

*v.* Kutatua kesi mbalimbali zilizofika ofisini

*vi.* Kuhudhuria mafunzo ya miradi ya **LGDG** manispaa Mpanda.

**TAARIFA YA WAZEE, WATOTO NA WALEMAVU WANAOISHI MAZINGIRAHATARISHI**

| MTAA | IDADI YA WAZEE | | WALEMAVU | | WATOTO | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | ME | KE | ME | KE | ME | KE |
| MSUFINI | 41 | 68 | 5 | 1 | 56 | 36 |
| AIRTEL | 60 | 62 | 4 | 2 | 52 | 34 |
| M/MMOJA | 70 | 74 | 1 | 3 | 18 | 20 |
| JUMLA | 171 | 204 | 15 | 6 | 126 | 90 |

**TAARIFA YA MAREJESHO YA VIKUNDI VINAVYODAIWA**

| S/N | JINA LA KIKUNDI | MTAA | SHUGHULI WANAZOFANYA | MKOPO NA RIBA | MAREJESHO | DENI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | ROGERS GROUP | M/MMOJA | BIASHARA | 1,560,000/= | 1,375,000/= | 275,000 |
| 2 | TUJIVUNE | MSUFINI | KILIMO CHA BUSTANI | 2,200,000/= | 220,000/= | 1,980,000 |
| 3 | TUMAINI | MSUFINI | BIASHARA NDOGONDOGO | 1,100,000/= | 987,000/= | 113,000 |
| 4 | FIKIRIA | MSUFINI | BIASHARA NDOGONDOGO | 2,750,000/= | 446,000/= | 2,304,000 |
| 5 | TUJINASUE | M/MMOJA | BUSTANI | 2,200,000/= | 780,000/= | 1,420,000 |
| 6 | HATANGIMANA | AIRTEL | BUSTANI | 2,200,000/= | 65,000/= | 2,135,000 |
| 7 | CHABYORONDA | MSUFINI | MBOGAMBOGA | 2,000,000/= | 170,000/= | 1,830,000 |
| 8 | MAARIFA | AIRTEL | KUUZA MAZAO | 4,400,000 | 735,000/= | 3,665,000 |

## *III.* SEKTA YA AFYA, KINGA NA NJAA

**TAARIFA YA UTEKELEZAJI JULY-SEPT 2018 KWA KAZI ZILIZOFANYIKA IDARA YA AFYA, KINGA KATA YA UWANJA WA NDEGE**

| NA | SHUGHULI | HALI YA UTEKELEZAJI | CHANGAMOTO | MPANGO MKAKATI |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa kampeni ya Kitaifa ya usafi wa mazingira | i.Nimetoa elimu ya afya juu ya umuhimu wa kila kaya kuwa na choo bora kwa mtaa wa | i.Eneo la kutoa elimu ni kubwa kwa kuwa ninahudumu Kata 2 na unahitajika | i.Ufuatiliaji wa ujenzi wa choo bora kila kaya unaendelea na sasa tunataka kuwafikisha katika |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | Mnazi Mmoja<br>ii. kufanya ukaguzi kwa wasiokuwa na vyoo katika mitaa yote 3 | muda wa kutosha kukamilisha zoezi hili<br>ii. Zoezi bado linaendelea sababu ya ukubwa wa Kata na pia kuhudumu Kata 2 | mabaraza ya Kata na mahakamani wote ambao hawana choo. |
| 2 | Ukaguzi kwenye majengo ya biashara na viwanda | Sehemu karibu zote zimekaguliwa na taratibu za kuendesha biashara ya chakula salama wamepewa | Hali yao wengi ni wajasiriamali na taratibu nyingi zinahitaji mtaji mwingi katika uwekezaji | Wote wanaofanya biashara ya chakula kuzingatia taratibu na sheria za vyakula |
| 3 | Kudhibiti uchafu na uchafuzi wa mazingira | Kuihamisha madampo yote na kuyaondosha mitaani | Usafishaji wa taka hizo kwani hali ya magari ya manispaa ni mabovu | Kuondoa hali hiyo mara moja magari yatakapotengamaa |
| 4 | Kuzuia magonjwa ya mlipuko | Elimu kwa wananchi juu ya matumizi sahihi ya maji salama na kunawa mikono mara watokapo chooni | Uelewa mdogo wa wananchi juu ya matumizi sahihi ya maji ya kunywa | Kuwaelimisha na kuwasimamia juu ya matumizi ya maji salama ya kunywana unawaji wa mikono mara watokapo vyooni |
| 5 | Kusimamia usafi wa kila Jumamosi ya mwisho wa mwezi | Kujitokeza kwa wananchi wengi zaidi katika siku hiyo | Baadhi ya wananchi kutohudhulia katika zoezi hilo | Kuwachukulia hatua wananchi wote wasiojitokeza kwenye zoezi |

## *IV.* UTEKELEZAJI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA JULY-SEPT 2018

**TAARIFA YA SHUGHULI ZA KILIMO ROBO YA KWANZA YA MWAKA KUANZIA JULY HADI SEPTEMBA 2018**

| S/N | SHUGHULI ZILIZOFANYIKA | MAHALI | WAHUSIKA |
|---|---|---|---|
| 1 | Vikundi vitatu vya kilimo cha bustani vimetembelewa na kupewa ushauri wa kitaalamu | -Mtaa wa Airtel<br>-Mtaa wa Mnazi Mmoja | Afisa Kilimo |
| 2 | Uhamasishaji kwa wakulima kulima mazao ya korosho na pamba msimu wa kilimo 2018/2019 ambapo wakulima 8 wamejitokeza | -Kata nzima ua Uwanja wa ndege | -Afisa kilimo<br>-Watendaji wote wa Kata na wataalamu<br>-Serikali zote za mitaa |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | kulima pamba na korosho | | |
| 3 | Kutembelea maeneo yote ya Kata yanayotumika kwa kilimo cha bustani na kubaini changamoto zinazowakabili | Kata yote ya Uwanja wa ndege | Afisa kilimo |
| 4 | Kuandaa semina kwa wakulima ambayo itawaandaa kwa msimu wa kilimo 2018/2019 ili kukumbushana mambo mbalimbali juu ya kilimo bora chenye tija | Kata yote ya Uwanja wa ndege | -Afisa kilimo<br>-wakulima wote |

**CHANGAMOTO**

Ukosefu wa usafiri kwa Afisa kilimo

***V.* UTEKELEZAJI WA MIFUGO NA UVUVI**

Shughuli zilizoanyika

*i.* Ongezeko la idadi ya wafugaji kufikia wafugaji 3 na mabwawa 8
*ii.* *Kuhamasisha wafanyabiashara wa samaki kukata leseni za kuuzia samaki na* wafanyabiashara 2 wamekata leseni
*iii.* Kuendelea kuhamasisha wenye mabwawa kufuga samaki

**CHANGAMOTO**

*i.* Ukosefu wa fedha za kununulia vifaranga vya samaki
*ii.* Ukosefu wa usafiri

**TAARIFA YA BARAZA LA KATA KIPINDI CHA JULY-SEPT 2018**

Baraza la Kata Uwanja wa ndege kwa kipindi hiki cha mwezi July-Sept **2018** limepokea mashauri yafuatayo:-

i. Nda mashauri 3 kesi inaendelea
ii. Madai
iii. Mgogoro wa ardhi
iv. Usafi wa mazingira watu 06

Mapato ya baraza la Kata kwa kipindi cha robo hii kwa ajili ya kufungua kesi na pesa zote zimetumika.
-Faini za usafi hakuna pesa walipewa adhabu ya kusafisha eneo la ofisi na kupanga tofali.
-Faini za kufungua kesi zimetumika kununua stationary

**ULINZI NA USALAMA**

Hali ya ulinzi na usalama katika Kata ya Uwanja wa ndege ni nzuri kwani hakuna matukio ya uvunjifu wa amani yaliyojitokeza.
Vikao vya ulinzi na usalama vimefanyika katika mitaa yote na mikutano ya hadhara. Pia vikundi vya ulinzi shirikishi vinaendelea na ulinzi katika maeneo yote ya Kata.

**UKIMWI**
Katika Kata ya uwanja wa ndege wananchi wanaendelea kupatiwa elimu juu ya kujikinga na **VVU** na **UKIMWI** kupitia vikao na mikutano ambavyo vinafanywa na kamati za UKIMWI kwa kuzingatia kalenda za vikao na kupitia vikundi mbalimbali kama **SHIDEPHA** na **ANGUEANA** wa Kizazi kipya wanaopita kwenye kaya moja kwa moja na kutoa elimu juu ya kujikinga na **VVU** na **UKIMWI**.

**CHANGAMOTO KATA YA UWANJA WA NDEGE**

i. Kukosekana kwa ofisi ya Kata
ii. Uhaba wa watumishi hasa kukosekana kwa Mtendaji wa Mtaa Msufini
iii. Upungufu wa magati ya maji hasa Mtaa wa Msufini kuna gati moja tu.
iv. Ongezeko kubwa la watoto walioandikishwa darasa la kwanza ni tatizo hasa yanapelekea uhaba wa madarasa.
v. Kutopimwa viwanja hasa eneo la Mnazi Mmoja kunapelekea wananchi kujenga kiholela.

**UTATUZI NA MAFANIKIO**

i. Tumefanikiwa kukusanya tofali **20,000** (elfu ishirini) kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi ya Kata
ii. Kwa kushirikiana na wazazi tumefanikiwa kujenga vyumba 2 vya madarasa na kujenga boma moja shule ya Msingi Kasimba.
iii. Kuendelea kufanya vikao na wadau mbalimbali wa maendeleo ili tuweze kujengewa magati ya maji.
Tumefanikiwa kuongeza magati matatu, Mnazi mmoja magati 2na Msufini gati 1.
Naomba kuwasilisha

**STEPHANO A. MWAKABAFU**
**MHE. DIWANI KATA UWANJA WA NDEG**